# Nipashe

Alhamisi Mei 2, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579907

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US








## Gharama za uchaguzi wa serikali mitaa Oktoba hizi

UKURASA 2



# JPM aeleza sababu za kutopandisha mishahara

UKURASA 2



Wafanyakazi wakiwa katika shamrashamra za maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), jijini Mbeya jana. **Picha zaidi Uk. 7**. **PICHA: IKULU**

## Vitambulisho wamachinga kaa la moto kwa ma-DC

UKURASA 2

## KCMC, Mawenzi zatajwa kunyanyasa wagonjwa

UK. 3

**MICHEZO** **TAIFA STARS YA AFCON HII HAPA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Vitambulisho wamachinga kaa la moto kwa ma-DC

**Na Wandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella, amewatahadharisha wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ambao hawajakamilisha ugawaji wa vitambulisho vya Rais zilivyotolewa kwa ajili ya wajasiliamali na kuwapa wiki moja kukamilisha kazi hiyo.

Aidha, Shigella alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Gondwin Gondwe, kwa kukamilisha kabla ya wakati uliyopangwa katika awamu zote mbili na hivyo kukusanya Sh. milioni 180 za vitambulisho hivyo.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya juma la elimu yaliyofanyika kimkoa mjini Handeni, Shigella alisema mbali na Handeni, wilaya zilizobaki zinaendesha zoezi hilo kwa kusuasua.

"Nimpongeze Mkuu wa Wilaya hii kwa uchapakazi na umakini anaouonyesha na kuongoza awamu zote kumaliza kabla ya wakati... sasa natoa wiki moja kwa wale wasiokamilisha, kama hamtavimaliza baada ya hapo hamna nafasi tena itakuwa mwisho wa kazi hii," alisema Shigela.

Hata hivyo alieleza kuwa awamu ya kwanza zoezi hilo lilingiza jumla ya milioni 400.47 ambapo pia Wilaya ya Handeni iliongoza kumaliza ikifuatiwa na Korogwe, Tanga, Muheza, Mkinga na Pangani.

Wakati huo huo, Diwani wa Kambarage Manispaa ya Shinyanga, Hassani Mwendapole, ameingiwa na wasiwasi juu ya zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya wamachinga huenda likashusha mapato ya ndani ya halmashauri hiyo, kutokana na wafanyabiashara wengi wamekimbilia kuvinunua na kukwepa kodi zingine za Serikali.

Alitolea mfano kwenye soko la Kambarage, akisemawafanyabiashara wengi walikimbia kufanyiabiashara zao sokoni humo kwa ajili ya kukwepa utozwaji wa ushuru kila siku, lakini baada ya kuanza ugawaji wa vitambulisho kwa Shilingi 20,000 kwa mwaka, wamerudi kwa wingi kwenye soko hilo wakiwa navyo.

Mwendapole alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha baraza la madiwani wakati wakijadili taarifa ya mkurugenzi wa halmashauri hiyo, kuwa anahofia zoezi hilo huenda likaathiri ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri.

Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Magedi Magezi, alisema zoezi linaendelea, hivyo kwa sasa hawawezi kufanya tathmini ili kujua kama ukusanyaji wa mapato utapungua kwa kiasi gani ama umeongezeka.

**Imeandikwa na Dege Masoli (Tanga) na Marco Maduhu (Shinyanga)**

# Magufuli ataja sababu kutopandisha mishahara

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli, amewataka watumishi wa umma kuwa wavumilivu wakati huu ambao anautumia kujenga uchumi wa nchi na kusisitiza atatoa nyongeza ya mishahara kabla hajaondoka madarakani.

Alitoa kauli hiyo jana katika maadhimisho ya sherehe za kitaifa za Mei Mosi yaliyofanyika katika viwanja vya Sokoine jijini Mbeya.

Maadhimisho hayo yalibebwa na kauli mbiu isemayo, 'Tanzania ya uchumi wa viwanda inawezekana, wakati wa mishahara na maslahi bora ni sasa'.

Rais Magufuli aliwaeleza watumishi wa umma kuwa hajapandisha mishahara kwa sababu ya mfumuko wa bei ambao endapo angetamka kuwa amependisha, bei za bidhaa na vitu mbalimbali nazo zingepanda.

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu imemkumbusha ahadi yake aliyoitoa mwaka jana wakati wa sherehe kama hizo zilizofanyika Iringa kuwa kabla ya kuondoka madarakani ataongeza mishahara.

"Ni kweli nilitoa ahadi hiyo ya nyongeza ya mishahara lakini ni lazima tuelewe hadi sasa sijaondoka madarakani" aliwaeleza wafanyakazi.

Aliongeza:"Naomba muamini, subira yavuta heri ningeweza kupandisha ila muda wangu bado haujaisha, ningeweza kutamka napandisha mishahara nikaongeza Sh. 5000 au 10,000 kwenye mishahara yenu, ningetamka hivyo kesho (leo) bidhaa zingeanza kupanda, matufa ya taa yangepanda, ukitaka mahindi yangepanda, usafiri ungepanda lazima tujenge uchumi imara."

"Bado ndugu zangu sijaondoka madarakani kwa maelezo niliyoyaeleza yanaonyesha uchumi wetu unakwenda vizuri kwenye uchumi wa kati, hatua tulizochukua na tunazoendelea kuchukua zinawanufaisha wafanyakazi na Watanzania wote," alisema.

Aliwaeleza wafanyakazi kuwa ahadi yake bado haijaisha muda na kwamba mwelekeo wa mambo yanavyokwenda anaamini yatafanikiwa kadri ya uchumi unavyokwenda ambao sasa umekua kwa asilimia saba.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi tano ambazo uchumi wake unakua kwa asilimia za juu, kwa miradi inayotekelezwa na uchapakazi wa wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara, tunaelekea pazuri," alisema na kuongeza:

"Nimeamua kuwaeleza ukweli, kwa sababu ukweli utabaki kuwa kweli, wafanyakazi tuvumilie, sikutaka niwapake uji kwa kutamka hapa nimepandisha mishahara halafu mkute hazipo, lazima tujipange vizuri na nafikiri tupo kwenye mwelekeo mzuri, nitaboresha maslahi kulingana na uwezo wa serikali."

Alisema kinachoendelea ni kikubwa kwa sababu yapo baadhi ya mataifa duniani baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, ziliamua wafanyakazi wao wasilipwe mshahara ili fedha zijenge nchi.

"Tumeamua kuanzisha miradi mikubwa mbalimbali ambayo inawanufaisha wafanyakazi, wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara wote," alisema.

Alisema ameamua kueleza hivyo kwa sababu yeye ni mtumishi wa wafanyakazi na ni lazima nchi ijengwe kwa kuwa hakuna baba au shangazi wa kuijenga.

"Hatua zinazochukuliwa na serikali ni kwa faida ya leo na kesho, serikali inawapenda wafanyakazi ndio maana tumechukua hatua

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli, akikabidhi cheti cha mfanyakazi bora kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA), Giliard Ngewe, wakati wa Sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana. **PICHA: IKULU**

# Gharama za uchaguzi wa serikali za mitaa Oktoba hizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kutumia Sh. bilioni 92 kuendesha uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, ndiye aliyetaja makadirio hayo alipozungumza na Nipashe jijini mwishoni mwa wiki.

Nipashe ilihitaji kujua gharama halisi za uchaguzi huo baada ya wiki iliyopita serikali kulieleza Bunge kuwa kunahitaji rasilimali fedha kuuendesha.

"Makisio ya gharama zote za uchaguzi wa serikali za mitaa ni Sh. bilioni 92," Waitara alibainisha. Aprili 25, mwaka huu, Waitara aliliambia Bunge kuwa uchaguzi huo unahitaji rasilimali fedha ili kuwezesha upatikanaji wa mahitaji mbalimbali.

Alisema rasilimali fedha inahitajika kwa ajili ya mafuta ya magari, matengenezo ya magari na posho mbalimbali kwa watu watakaoshughulikia mchakato mzima wa uchaguzi.

Waitara alitoa kauli hiyo alipokuwa anajibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Aida Khenan (Chadema), aliyehoji sababu za serikali kutenga na kutuma fedha katika uchaguzi huo.

Katika majibu yake siku hiyo, Waitara alisema madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyotajwa kwenye Ibara ya 146(2) (a)-(c), ni kuimarisha demokrasia na kuitumia kuharakisha maendeleo.

Alisema katika kutekeleza jukumu hilo muhimu, viongozi wanaoongoza vyombo vya serikali za mitaa huchaguliwa kwa njia ya kidemokrasia kupitia uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Uchaguzi wa serikali za mitaa unahitaji rasilimali fedha ili kuwezesha upatikanaji wa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi vikiwamo vifaa vya uchaguzi kama vile masanduku, lakiri na fomu pamoja na gharama zingine mbalimbali za mafuta na posho,"alisema.

Vilevile, Waitara alisema ziko taratibu za kisheria ambazo zinapaswa kufuatwa katika uchaguzi huo kama vile kutoa matangazo ya serikali yanayohusu uchaguzi.

Pia alisema kunahitajika kufanyika vikao mbalimbali na wadau wa uchaguzi, kuhakiki maeneo au majimbo ya uchaguzi na kuandaa daftari la wapigakura, shughuli zote hizo zikihitaji rasilimali fedha.

"Hivyo, ili kukamilisha uchaguzi wa serikali za mitaa ni lazima serikali itenge fedha za kugharamia shughuli za uchaguzi huo kama ilivyo kwa Uchaguzi Mkuu wa rais, wabunge na madiwani," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, akionyesha almasi yenye ukubwa wa karati 521, ambayo imepatikana kwa mchimbaji mdogo wa madini wilayani Kishapu. Almasi ya ukubwa huo, haijawahi kupatikana mkoani humo tangu kuanzishwa wa uchimbwaji wa madini hayo miaka 87 sasa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri Mpango awajibu kisomi wanaohoji kushuka bajeti elimu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Philip Mpango, amewajibu 'kisomi' wabunge wa upinzani wanaohoji kupungua kwa bajeti ya maendeleo ya elimu kuwa kilichopungua ni bajeti ya matumizi ya kawaida kwa miaka miwili iliyopita.

"Si kweli kuwa bajeti ya maendeleo imekuwa na mserereko wa kupungua, uki-compose (kuzinyambua) hizi namba unaona kwamba kilichopungua ni bajeti ya matumizi ya kawaida na imepungua kwa miaka miwili iliyopita.

Dk. Mpango ameeleza: "Ni kweli ukiangalia takwimu zinaonyesha bajeti ya elimu inapungua katika asilimia kutoka asilimia 17 ya bajeti yote ya 2015/16, asilimia 16 mwaka 2016/17, asilimia 15 mwaka 2017/18, asilimia 14 mwaka 2018,19 na asilimia 14 ya mwaka ujao wa fedha 2019/20."

Alikuwa akijibu hoja za baadhi ya wabunge walioigusa wizara yake wakati wakichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Baadhi ya wabunge walihoji sababu za Wizara ya Fedha na Mipango kushindwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya elimu katika bajeti inayoishia Juni 30, mwaka 2019.

"Kulikuwa na hoja kwamba fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha unaoisha zitolewe zote kabla ya Juni 30, 2019 naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba fungu hili litengewa Sh. trilioni 1.4 na mpaka kufikia tarehe 29 Aprili, fungu hili lilikuwa limepewa Sh. bilioni 890.58 ambayo ni asilimia 63 ya bajeti kwa fungu hili," alisema Dk. Mpango.

Akifafanua, Waziri Mpango alieleza kuwa kwa kutambua umuhimu wa pekee wa elimu kwa maendeleo ya nchi, serikali inawahakikishia Watanzania kwamba katika kipindi kilichobaki cha Mei na Juni, 2019 itatoa fedha kwa fungu 46 kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti na hususani kifungu cha '45 b' kinavyoelekeza.

Aidha, alieleza kuwa mwaka 2015/16, bajeti ya wizara hiyo ilikuwa bilioni 3.2 kwa matumizi ya kawaida (re-current budget), ikaongezeka kwenda bilioni 3.7 mwaka 2016/17, 2017/18 na ikashuka kidogo na kuwa bilioni 3.5 na Sh. bilioni 3.4 kwa mwaka huu wa fedha ambayo pia kwa mwaka ujao wa fedha itashuka kidogo na kuwa bilioni 3.1

"Hii inatokana na hatua ambazo serikali ilichukua ikiwamo kuwaondoa watumishi hewa kutoka katika sekta ya elimu, lakini restructuring (mabadiliko) ambayo imefanyika katika taasisi mbalimbali ambayo imeondoa baadhi ya watumishi kutoka kwenye taasisi mbalimbali katika fungu hili.

"Lakini ukiangalia upande wa fedha za bajeti ya maendeleo, hizi zimeongezeka kutoka bilioni 0.6 mwaka 2015/16 kwenda bilioni moja 2016/17, bilioni 1.1 mwaka 2017/18, bilioni 1.2 mwaka 2018/19 na bilioni 1.3 kwa mwaka ujao wa fedha 2019/20. Kwa hiyo ni vizuri kufanya composition (mnyambulisho) ili uweze kusema kweli bajeti inateremka."

Kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kwamba ipewe fungu lake linalojitegemea, aliishauri bodi hiyo kuandaa andiko la maombi ya kuwa na fungu lake binafsi linalojitegemea baada ya kushauriana na wizara mama.

Alisema ni vyema pia utaratibu wa kuanzisha fungu hilo ukazingatia majukumu na muundo uliopitishwa na Ofisi ya Rais, (Utumishi) ili kuweza kubainisha mnyororo wa mamlaka za utendaji na wizara yake ijiridhishe kwamba fedha ya umma itasimamiwa vizuri.

# Mambo 10 yaliyotikisa bajeti Wizara ya Elimu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBINYO unakuja kwa shule zinazoendeshwa kwa kutumia lugha ya Kingereza nchini (English Medium Schools), baada ya serikali kusema imekamilisha kazi ya kuunda vitabu vya kiada kwa shule zinazotumia lugha hiyo kama lugha ya kufundishia kwa darasa la kwanza, la pili na la tatu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, akizungumza bungeni jijini Dodoma juzi, wakati akihitimisha mjadala wa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20 ya wizara hiyo, alisema vitabu hivyo vipo tayari na vinapatikana katika maktaba ya mtandao.

Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imekamilisha kazi ya kuunda vitabu vya kiada kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia kwa darasa la kwanza, la pili na la tatu na vitabu hivyo nilishasema vipo, kwamba tumeshaanzisha maktaba ya mtandao," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, mitaala na mihtasari kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza ilishaandaliwa tangu mwaka 2016 na inapatikana Taasisi ya Elimu Tanzania, duka la vitabu la Taasisi ya Elimu Tanzania na maduka ya mawakala wa taasisi hiyo ambayo yanapatikana katika mikoa yote nchi nzima.

Kuhusu malalamiko ya kubadilika mitaala ya elimu mara kwa mara, alisema tangu nchi imepata uhuru 1961, mtaala wa elimu umebadilika mara nne.

"Mara ya kwanza ni baada ya kupata uhuru, mara ya pili ni baada ya kupitishwa Azimio la Arusha 1977, mara ya tatu ulibadilika mwaka 1979 kwa kuingiza masomo ya michepuo na mara ya nne ulibadilika 1997 baada ya mfumo wa vyama vingi vya siasa, kwa hiyo kulikuwa na context (maudhui) ambazo zilibadilika," alieleza.

Katika majibu yake, Waziri Ndalichako ameeleza kwamba wakati mwingine serikali inakuwa inafanya maboresho ya mitaala, kwa mfano mwaka 2015 Kiswahili kilizaliwa Sudan Kusini, hivyo ilikuwa ni lazima ifanye maboresho hayo na sio

INAENDELEA UK. 4

# KCMC, Mawenzi zatajwa kwa kunyanyasa wagonjwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro, imezitaja hospitali za rufani KCMC na Mawenzi kutoa huduma mbovu zenye ubaguzi na gharama kubwa kwa wageni.

Zimedaiwa kuwatoza wageni hasa watalii wanaoingia mkoani humo kwa shughuli za kitalii gharama kubwa ya matibabu hali inayowafanya wakimbie na kwenda kutibiwa nchi jirani.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alitoa shutuma hizo katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), mkoani hapa.

Akitoa mfano, alisema mtalii anapougua wakati akiwa mkoani humo na kwenda kupata matibabu kwenye hospitali hizo, hutozwa Dola za Kimarekani 250 (zaidi ya Sh. 500,000), kumuona daktari pekee.

Alisema kutokana na gharama hizo kuwa kubwa wageni hao hulazimika kukimbilia Kenya kupata matibabu na kuikosesha nchi mapato.

"Nasikitika kila mara wanaanza siku kwa kusali na kumaliza kwa kusali, lakini wanawanyanyasa wagonjwa kwa kuwapatia huduma zisizo na tija na kuwapandishia matibabu mara kwa mara bila kuwaelimisha," Dk. Mghwira alisema.

"Taasisi za afya zimezidi kuwa bomu zaidi na wananchi wamekuwa wakizilalamikia mara kwa mara kwa uonevu na unyanyasaji na hata wengine kupoteza maisha kwa ukatili unaotendeka, ipo haja ya watumishi katika taasisi hizi kubadilika," alisema.

Baadhi ya wananchi waliohudhuria sherehe hizo, Fadhila Ibrahimu, alikiri kuombwa rushwa katika moja ya hospitali iliyotajwa na kuwapo kwa ubaguzi kwa watu wenye kipato cha chini, hali inayosababisha baadhi yao kupoteza maisha.

"Tunaiomba serikali kuangalia namna ya kudhibiti hospitali hizi, watu wamekuwa wakiachwa na mikasi baada ya operation (upasuaji) na majibu machafu wanapoenda kulalamikia bili zinapokuwa kubwa," alidai.

Aidha, Ester Msofe, alisema kuwa bado kunachangamoto kubwa katika utoaji wa huduma hasa

INAENDELEA UK. 8

## Mambo 10 yaliyotikisa bajeti

INATOKA UK. 3

mabadiliko ni maboresho katika mitaala kuonyesha kwamba nchi za Afrika, idadi imeongezeka kwa sababu kuna nchi mpya imezaliwa, huwezi ukasema ni mabadiliko.

Akijibu hoja iliyotolewa na Mbunge wa Vunjo (NCCR-Mageuzi), James Mbatia, kwamba kuna tatizo la kukosekana kwa baadhi ya vitabu vya elimu ya msingi vya darasa la tano, Prof. Ndalichako alisema suala la kutokuwapo kwa vitabu vya baadhi ya masomo sio la kweli.

Alisema madai ya kutokuwapo kwa baadhi ya vitabu vya elimu ya msingi vya darasa la tano, si sahihi kwa kuwa vitabu vya darasa la tano vilishasambazwa shuleni nakala milioni 2.864 na walichelewa kupata walipata mwezi Februari, 2019.

Akipangua hoja kwamba mfumo wa elimu nchini unakwenda ndivyo sivyo, Waziri Ndalichako alisema serikali inatambua bila mfumo imara wa elimu, mambo hayawezi kwenda vizuri na ndio maana serikali ilifanya uhakiki wa watu wenye vyeti feki.

Alisema jumla ya watumishi 15,536 waliondolewa kwenye utumishi, lakini pia serikali kwa kutambua kwamba ukimweka mtu mahali asipokuwa na sifa hawezi kufanya vizuri, zaidi ya watumishi 5,300 ambao walikuwa wameajiriwa katika fani ambazo hawana ujuzi nazo, wameondolewa.

Akionyesha kutofurahishwa na michango ya baadhi ya wabunge kuwadhihaki washirika wanaotoa fedha za maendeleo, Prof. Ndalichako ameeleza kutofurahishwa na hali hiyo akisema haipendezi, mtu mstaarabu ambaye ni muungwaa ameshirikiana na wewe katika maendeleo, wanatumia maneno ya ajabu ajabu ya kuwasema washirika wao wa maendeleo.

Prof. Ndalichako ameeleza: "Hii dhana ya kusema serikali imekuwa tegemezi sana si sawa, ukiangalia bajeti ya wizara kwa miaka mitatu iliyopita 2017/18 mchango wa serikali ulikuwa asilimia 66.2 na mchango wa wafadhili 33.8, lakini katika mwaka huu wa fedha 2019/20 ambao naomba kwa unyenyekevu wabunge muidhinishe mchango wa serikali ni asilimia 67.6 na mchango wa wafadhili ni asilimia 32.4 kwa hiyo

INAENDELEA UK. 26

# Mbinu mpya ya ukeketaji yabainika

**Na Salome Kitomari**

MASHIRIKA 12 yasiyo ya kiserikali yanayopinga ukeketaji yamekutana jijini Da es Salaam na kubaini kuwapo kwa mbinu mpya za kuendeleza mila hiyo iliyopitwa na wakati.

Aidha, mashirika hayo yamekubaliana kuunganisha nguvu kwa kuunda umoja wa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayopinga ukeketaji na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, ambao watakwenda maeneo mbalimbali nchini kutoa elimu.

Katika mjadala wa mashirika hayo ilibainika upo uwezekano mkubwa wa ukeketaji kuhusishwa na imani za kishirikiana kutokana na wazee wa mila kuandaa mambo yao na kuyahusisha na ukeketaji, jambo linaloisukuma jamii kuendelea na ukeketaji.

Mkutano huo ulifanyika katika ofisi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Meneja Miradi wa shirika la kuondoa ukeketaji wanawake (ATFGM), Valerian Mgani, alisema upo uwezekano mkubwa wa ukeketaji kuhusiana na ushirikina kwa kuwa baadhi ya wazee wa kimila hutumia mbinu ya kutangaza janga fulani kwenye jamii na linapotokea huaminika.

Alisema mkoani Mara kinachofanyika ni wazee wa mila kutoa kauli au amri fulani ambayo ikitokea kuwa kweli jamii huamini na haikubali kuacha mila hiyo kwa kuogopa kupata madhara ya kimila.

Alisema mkoani humo ukoo wa Bwirege umeendelea kushikilia mila hiyo kwamba binti akipata mimba kabla hajakeketwa hutupwa mto Mara, ili aliwe na mamba na kupotea na akifanikiwa kupona hataruhusiwa kuungana na familia yake kwa kuwa amekwenda kinyume na mizimu yao.

"Kuna binti mmoja wa eneo la Nyamwanga aliokolewa akiwa katika hatua za mwisho za kutupwa mto mara, alichukuliwa usiku na wazee wa kimila bahati nzuri tulipata taarifa tukafuatilia tukiwa na

INAENDELEA UK.8



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akizungumza na Naibu Gavana wa Benki Kuu Tanzania (BoT), Bernard Kibese (katikati), na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Ally Laay, katika mkutano wa wawekezaji jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Hatua za serikali kuelekea uchumi wa kati zasifiwa

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI Kazi cha Viwanda kilichoundwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kimetambua na kufurahishwa na hatua zilizochukuliwa na serikali kuelekea uchumi wa kati na wa viwanda.

Wenyeviti wenza kutoka sekta ya umma na binafsi wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasilisha taarifa za awali kwa Kamati ya Utendaji ya TNBC, kwa pamoja wamesifu hatua ambazo mpaka sasa serikali imechukua ili kuiwezesha Tanzania kuwa na uchumi wa kati ifikapo 2025.

"Tumepita na kujadili changamoto zinazolikabili taifa katika kutekeleza azima hii; tumepitia historia ya nchi yetu katika ujenzi wa viwanda. Ili kuimarisha majumuisho yetu sekta binafsi tumewasilisha andiko ambalo tumependekeza lichukuliwe kama rasimu ya sera mpya ya viwanda na tumegusa mambo tunayoanimi ni ya msingi," alieleza Mwenyekiti Mwenza (sekta binafsi), Ali Mufuruki.

Kuhusu sera ya viwanda waliyoipendekewa, Mufuruki alisema: "Tumekuwa na majadiliano mazuri

pande zote mbili na tumeshirikisha watu wengi. Katika andiko hili tumependekeza tuaangalie kwa makini uwezo wa watu, fursa zilizopo, suala la Watanzania kuwajengea uwezo kiuchumi na suala la masoko kwa bidhaa za viwanda tunavyokusudia kujenga."

Amedokeza pia kwamba katika andiko vimependekezwa aina ya viwanda ambavyo vinastahili kupewa kipaumbele, umuhimu wa kufanya tafiti na kubadilisha mfumo wa elimu ili uwepo uwiano kati ya masomo wanayofundishwa wanafunzi na kile wanachotarajia kukifanya mitaani.

"Viwanda Tanzania sio kitu kipya, vilikuwepo huko nyuma, kwa sasa tunachofanya ni kuangalia mambo mengi ambayo safari hii yanaweza kutukwamisha katika utekelezaji wa sera ya viwanda. Andiko letu limejikita hapa," amefafanua Mufuruki.

Mwenyekiti Mwenza (sekta ya umma), Joseph Simbakalia, ameungana na Mufuruki na kusema kikozi kazi kimependekeza kwa TNBC kwamba safari hii taifa liepuke makosa ya nyuma.

"Viwanda kwa Tanzania siyo ndoto. Tumekuwa na viwanda huko nyuma, hasa viwanda vya nguo na utekelezaji wake ulionekana. Kwa sasa tunachokifanya ni kuhimiza taifa kuchukua tahadhari ili kuepuka makosa yaliyoharibu viwanda mbali mbali ikiwemo viwanda vya nguo," alisema Simbakalia.

Aligusia hatua ambazo serikali imezichukua ili kuelekea kwa uhakika uchumi wa viwanda, kwa kutaja taja hatua hizo kuwa ni pamoja na kuwekeza katika miundombinu ambayo amesema ndiyo msingi wa viwanda endelevu.

Pia alisema serikali imeimarisha utendaji ndani ya serikali, utawala bora na kupambana na rushwa na kutolea mfano wa Singapore kuwa ilidumazwa na rushwa. Lakini ilipoidhibiti rushwa maendeleo ya viwanda yalichipuka na sasa Singapore ni nchi ya kupigiwa mfano.

Kikosi Kazi cha Viwanda ni miongoni mwa vikosi kazi vilivyozinduliwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, hivi karibuni.

HABARI KITAIFA



Wafanyabiashara wa vitafunio wakisubiri wateja katika Mtaa wa Mbaruku na Msimbazi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hofu ya tetemeko la ardhi yasababisha taharuki kubwa

**Na Waandishi Wetu**

TAHARUKI kubwa iliwapata wakazi wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, baada ya usiku wa kuamkia jana kupita tetemeko la ardhi.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba serikali kupitia mamlaka husika kutoa elimu ya tetemeko la ardhi kwa jamii kutokana na tukio hilo kuonyesha kuwa watu wengi hawana ufahamu kuhusu tetemeko la ardhi linavotokea na tahadhari.

Tetemeko hilo limetokea maeneo mbalimbali ya wilaya ya Masasi majira ya saa 3:00 usiku wakati watu wengi wakiwa amejipumzisha majumbani, na baada ya kupita tetemeko hilo walitoka nje ya nyumba zao.

Wakizungumza na Nipashe jana mara baada ya tetemeko hilo kupita, baadhi ya wakazi hao walisema walishikwa na taharuki kubwa waliposikia nyumba zao zikitetemeka, kuta zikitingishika na kudodosha baadhi ya vipande vya matofali.

Salumu Bakari, mkazi wa Masasi Mtaa wa Kambarage, alisema hakufahamu kuwa kilichotokea ni tetemeko la ardhi bali akiwa nyumbani kwake na familia yake wamepumzika, walisikia kuta na paa za nyumba yao zikitikisika, huku nyumba yao ikitetemeka kwa nguvu.

INAENDELEA UK. 8

# JPM awashangaa Mbeya kutokukopa benki kilimo

**Na Nerbart Msokwa,** MBEYA

RAIS John Magufuli amewataka wakulima mkoani Mbeya kuchangamkia fursa ya Mikopo yenye riba nafuu inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kuimarisha shughuli zao kwani benki imeanzishwa kwa ajili ya kuwahudumia. Hata hivyo, Rais Magufuli aliwashangaa kwa kusuasua katika uchukuaji wa mikopo pamoja na kuwa vinara wa uzalishaji katika mazao mbalimbali ya kilimo.

"Mpaka Machi mwaka huu, TADB ambayo ni benki yenu nyinyi wakulima ilikuwa imeshatoa Mikopo ya thamani ya Sh. bilioni 102 kwa wakulima nchi nzima ambapo wakulima Mbeya wamekopa Sh. milioni 779.9 tu," alisema Magufuli kwa masikitiko.

Rais Magufuli ambaye pia aliipongeza Benki ya Kilimo kwa ufanisi na utendaji wake katika kuwahudumia wakulima, alisema wakulima mkoani Mbeya hawanabudi kuitumia benki hiyo kujiletea maendeleo katika sekta ya kilimo.

"Tumeendelea kuimarisha Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo na sasa imeanza kutoa mikopo kwa wakulima. Na hii ndiyo fursa pekee kwenu kuchangamkia Mikopo yenye riba nafuu," alisema.

Alisema serikali ilitambua umuhimu wa kuwapo kwa benki ya kilimo nchini na ndiyo maana ikaamua kuianzisha ili kuinua sekta ya kilimo ikiwamo kutatua changamoto mbalimbali ya upatikanaji wa mitaji kwa wakulima hapa nchini.

Akielezea na kufafanua zaidi kuhusu hizo bilioni 102, Rais Magufuli alisema wakulima mkoani Kagera kwa mfano wamekopa Sh. bilioni 38.3.

"Fikiria wakulima wa mikoa ya Mtwara na Lindi Regions wamekopa Sh. bilioni 33 ambapo Mwanza wamekopa Sh. bilioni 11.2 na nyinyi Mbeya ambao ni wazalishaji wakubwa mmekopa pungufu ya Sh. bilioni moja," alisema.

Aligusia pia mkopo wa dola za Kimarekani milioni 110 sawa na bilioni 250 pesa ya Kitanzania kutoka Serikali ya Poland kwa ajili ya kiwanda cha kuunganishia matrekta Kibaha mkoani Pwani kwa ajili ya kuchochea kilimo.

# ATE yaomba mazingira bora ya biashara

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimeiomba serikali kupunguza gharama na kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi na kukuza uchumi wa nchi.

Akitoa salamu za waajiri katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani yaliyofanyika kitaifa jijini Mbeya, Mwenyekiti wa ATE, Jayne Nyimbo, alisema pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuhakikisha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini yanakuwa bora, matokeo yake bado yanakabiliwa na changamoto.

Alisema waajiri nchini wameendelea kukumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo gharama kubwa za kufanya biashara hapa nchini.

"Moja ya changamoto hizo ni tozo kubwa ya kuendeleza ujuzi mahala pa kazi (SDL), kwa sasa waajiri wanatozwa asilimia 4.5, hivyo tunaiomba serikali ipunguze tozo hii kutoka asilimia 4.5 ya sasa mpaka asilimia mbili na gharama nyingine ni pamoja na kodi ya kipato kwa wafanyakazi." alisema Nyimbo.

Alisema ATE wameiomba serikali kufanya sheria za kazi zilizopo ili ziweze kuendana na mazingira ya kufanya biashara na kusaidia kuongezeka kwa uzalishaji na ukuzaji wa uchumi wa taifa.

"Sheria zetu za kazi za sasa zinalea uzembe, ubadhirifu na wizi mahala pa kazi. Sisi waajiri tungependa kupata ushirikiano wa dhati kutoka kwa wadau wa Utatu katika kufanya marekebisho ya sheria hizi ambazo zitafanya kuwapo kwa mazingira rafiki ya uwekezaji nchini ambayo yatachochea ukuaji wa haraka wa uchumi wa taifa letu," alisema Nyimbo.

Aidha, ATE imempongeza Rais John Magufuli kwa kuwa mstari wa mbele katika kukemea suala la urasimu kwenye masuala ya uwekezaji unaofanywa na baadhi ya idara na taasisi za serikali na kusisitiza kwamba suala hilo lisipokemewa litakwamisha juhudi na azma ya kuelekea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.




MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fursa biashara ya saa 24 Dar ichangamkiwe

**MPANGO** unaoandaliwa na uongozi wa serikali mkoani Dar es Salaam wa kuweka utaratibu wa wafanyabiashara kufanya biashara usiku, ni fursa ya kiuchumi kwa wananchi na kwa Serikali.

Mkoa huo umesema kwamba mpango wa biashara mbalimbali zikiwamo za baa kufanyika kwa saa 24 katika jiji hilo upo katika hatua za mwisho za kukamilika na unatarajiwa kuzinduliwa mwezi ujao na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Mkoa huo, Paul, Makonda, alipokuwa akizungumza na wakuu wa wilaya, makatibu tawala, wakurugenzi na watendaji wa Wilaya zote za jiji hilo, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Makonda alisema taratibu za kufungua biashara kwa saa 24 jijini humo zimekamilika isipokuwa baadhi ya mambo ya usalama ambayo yanakamilishwa na Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa.

Kati ya mambo ambayo yalikuwa yanafanyiwa kazi na watendaji wa mkoa huo ili kufanya kazi kwa saa 24, ni kuwa na taa maeneo yote ya biashara na kuimarishwa kwa usalama wa maeneo hayo.

Miongoni mwa biashara ambazo Makonda alisema zinapaswa kufanywa kwa saa 24 ni za baa, maduka na usafiri ili kuongeza mzunguko wa fedha na makusanyo.

Kubuni mpango huo ni hatua nzuri, ambayo ni fursa ya pekee kwa wananchi ambao wana kiu ya maendeleo na nia ya dhati ya kujiongezea kipato.

Kwa kuanzisha mpango huo, wananchi wengi bila shaka watachangamkia fursa hiyo kwa kuwa hakutakuwapo na hofu ya usalama, kwa kuwa serikali inaandaa mikakati ya kuimarisha usalama wakati wa usiku.

Huko nyuma, watoa huduma na wafanyabiashara walikuwa wanashindwa kuongeza kipato kutokana na sheria kuelekeza shughuli za biashara kufungwa saa 5:00 usiku.

Kimsingi, shughuli za biashara usiku ni fursa kwa kuwa kuna watu wengi ambao wakati huo wanakuwa wanahitaji huduma. Kwa mfano, kuna watu ambao wanatoka katika maeneo yao ya kazi muda wa usiku, hivyo kukuta maeneo ya huduma na biashara yakiwa yamefungwa.

Lakini pia kuna huduma muhimu kama za usafiri wa mabasi ya umma (daladala), bajaj na pikipiki ambazo zinahitajika kuwapo kwa muda wote bila kujali kama ni usiku au mchana.

Kwa hiyo kuwapo usafiri wakati wote kutawawezesha watu kutopata usumbufu kama ambavyo wamekuwa wakihangaika, ikiwamo kulipa gharama kubwa kutokana na usafiri kutokuwa wa uhakika wakati wa usiku.

Tunaamini kwamba mamlaka zimejipanga vya kutosha hususan suala muhimu la ulinzi na usalama wa uhakika wakati wote kwa saa 24.

Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wamepata fursa adhimu ya kupata huduma za uhakika kwa wakati wote. Lakini kwa wanaojipatia kipato kwa kufanya biashara wanatakiwa kuichangamkia fursa hiyo.

Suala la msingi ni kila mkazi kujenga utamaduni wa ustaarabu na kuitumia vizuri fursa hiyo, ili wachache wasije kuilazimisha serikali ikaamua vinginevyo itakapobaini kuwa inatumika vibaya hususan kuongezeka kwa uhalifu na mambo mengine.

Tunawapongeza walioubuni mpango huo na tunawashauri waendelee kubuni mipango mingine ambayo itasaidia kuongeza pato la mtu mmoja mmoja na serikali kwa ujumla sambamba na kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa kitovu cha biashara nchini.

Tunasema hivyo kwa sababu Dar es Salaam sasa limebakia kuwa Jiji la biashara baada ya serikali kuhamia jijini Dodoma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mambo haya yarekebishwe kufikia Uchumi wa Viwanda

Na Salome Kitomari

**TANZANIA** inajinasibu katika dhamira ya kufikia Uchumi wa Viwanda, ifikapo mwaka 2025. Si miaka mingi kuanzia sasa.

Tangu kuingia madarakani kwa Rais Dk. John Magufuli, msisitizo umekuwa uanzishaji, ufufuaji na uendelezaji wa viwanda nchini.

Ripoti ya Hali ya Ufanyaji Biashara (Doing Business Report 2018) inayotolewa na Benki ya Dunia kila mwaka, inaonyesha Tanzania inakabiliwa na vikwazo vinne katika kuboresha mazingira ya biashara, ambavyo inavitaja kuwa ni: Vikwazo vya kiserikali, utitiri wa kodi na vikwazo mpakani.

Eneo la kodi linalolamikiwa na wawekezaji wengi ni kilio cha muda mrefu cha, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), ambayo tangu serikali iliyopita, walilia kodi kuwa kikwazo kikubwa na kuiomba serikali kuunganisha baadhi ya mifumo na taasisi zake, kuepusha usumbufu na kodi nyingi.

Mara kadhaa, kilio hicho kimetolewa na wawekezaji wanaofika wakinuia kuwekeza, kwamba kodi zimekuwa nyingi na siyo rafiki, jambo linalotajwa kinawakwaza wawekezaji wengi.

Katika kudhihirisha kwamba bado ni tatizo kubwa linalowaathiri walio serikalini na sekta binafsi, hivi karibuni Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kililalamikia maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kufunga biashara za wawekezaji.

Mkurugenzi wa TIC, Geoffrey Mwambe, alinukuliwa akisema kitendo cha kuwafungia wafanyabiashara na viwanda sababu ya kodi au vibali vingine, kinafifisha hamasa ya uwekezaji nchini.

Anashauri hatua ya kufunga biashara au viwanda, ingekuwa ya mwisho badala ya inavyofanyika sasa.

Kilio hicho siyo cha bure. Maana yake ni kwamba, kuna jambo kubwa lenye madhara makubwa kwa wawekezaji na taifa kwa ujumla, kwa kuwa wawekezaji watashindwa kufanya biashara. Maana yake ni kwamba, watu watakosa ajira na hawatachangia pato la taifa.

TIC na TRA ni asasi za serikali. Hivyo, inapofikia hatua zikalalamikiana hadharani, maana yake kuna kitu hakijakaa sawa, kwa kuwa kilichotarajiwa watoto wa baba mmoja kuyazungumza ya ndani ya familia na kuyamaliza kimya kimya.

Inapofikia Mkurugenzi wa TIC, anakwenda mbele ya vyombo vya habari 'kulia' dhidi ya ndugu yake TRA, maana yake kunahitajika mamlaka zinazowasiomamia, kusaidia kuweka mambo sawa katika familia hiyo.

Tanzania inajitangaza kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, lakini kilio cha kodi kimekuwa cha wote na kila wanapopata nafasi huimba serikali, kuliangalia hilo kwa jicho la kipekee.

Yapo maboresho yameshafanyika, ikiwamo kuondoa riba kwa wafanyabiashara walioukuwa na madeni makubwa ya kodi, walitakiwa kulipa kodi kamili kwa muda uliotengwa na TRA.

Ni vyema TIC na TRA wakafanya kazi kwa kushirikiana, kuhakikisha vikwazo vyote vya wawekezaji kuwekeza nchini, katika sekta mbalimbali vinaondolewa.

Katika miaka ya 1990, serikali ilibinafsisha mashirika mengi ya umma yanayomilikiwa na serikali na wawekezaji mbalimbali wa nje na ndani, walimilikishwa kwa asilimia 100 na wengineo hisa mbalimbali kuanzia wastani wa asilimia 51 na zaidi.

Viwanda vingi vilikufa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ongezeko la kodi, ulafi na wawekezaji kuvitumia kujinufaisha kutokana na udhaifu wa usimamizi uliokuwepo.

Kiwanda kimojawapo kilichomilikiwa kwa hisa nyingi na serikali, ni cha kutengeneza matairi mkoani Arusha au maarufu General Tyre, ambacho Serikali ilimiliki hisa asilimia 74 na mwekezaji asilimia 26.

Kiwanda kilikufa kwa sababu nyingi, mwekezaji kuwa na nguvu katika 'mazingira tata' kuliko mwenye hisa nyingi na hata kufa kwake, mazingira yake hayakuwa wazi kwa wengi wetu.

Upo umuhimu mkubwa, kwa TIC na TRA kukutana na kujadiliana kwa kina changamoto za kodi kwa wawekezaji ili kuhakikisha malalamiko ya wawekezaji yanasikilizwa na kufanyiwa kazi.

Tanzania ya viwanda itawezekana, ikiwa pande zote mbili zitakutana na kujadili changamoto zilizopo, ili kujenga mazingira rafiki kwa wawekezaji ambao wataitangaza vyema nchi.

# SHEREHE ZA MEI MOSI KATIKA PICHA



Rais John Magufuli, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Job Ndugai, Naibu Spika, Tulia Ackson, Waziri wa Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Jenista Mhagama na viongozi wa wafanyakazi wakishuhudia maandamano ya wafanyakazi wakati wa sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), jijini Mbeya jana. **PICHA: IKULU**



Muonekano wa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, wakati wa sherehe za Mei Mosi jana. **PICHA: IKULU**




Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), wakishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani zilizofanyika kimkoa katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mbunge wa  Kuteuliwa, Salma Kikwete, akisalimiana na baadhi ya walimu wa Mkoa wa Dodoma, katika maadhimisho ya  Siku ya Wafanyakazi Duniani katika uwanja wa Jamhuri, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




Baadhi ya wafanyakazi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), wakiingia katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, kwenye maandamano ya sherehe za Mei Mosi. **PICHA: MNH**




Wafanyakazi wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), wakipita mbele ya Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (hayupo pichani), wakati wa sherehe za Mei Mosi, katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Magufuli ataja sababu kutopandisha mishahara

INATOKA UK. 2

zote na kulibeba suala la kikokotoo ili wastaafu wapate haki zao," alisema.

Alisema nchi za jirani zinaishangaa Tanzania kwa kuamua kutekeleza suala la kikotoo kwa sababu hata Ulaya hawana.

Aliwaeleza wafanyakazi kuwa serikali imeanza kulipa mabilioni na kuchangiwa Sh. bilioni 1.5 kwenye mifuko ya pensheni ambazo zilikuwa hazichangwi muda mrefu.

Aliwataka wafanyakazi waendelee kuchapa kazi ili kuliletea taifa maendeleo kwa sababu wazee wa zamani walijitoa muhanga kulikomboa kisiasa na sasa ni jukumu la kizazi cha sasa kujitoa muhanga kulikomboa kiuchumi.

"Kwa takwimu za jana tumeajiri walimu na watumishi 19,000 na upande wa sekta ya afya tumeajiri madaktari manesi 11,000 bado sekta nyingine," alisema.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana nao na kuzishughulikia changamoto zinazowakabili wafanyakazi.

Pia alisema serikali imezibeba kero na mapendekezo ya Shirikisho Huru la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) waliotoa kwa serikali.



Awali, Katibu Mkuu wa Tucta, Dk Yahaya Msigwa, aliiomba serikali itekeleze kwa vitendo suala la punguzo la kodi kwenye mishahara kwa asilimia tisa kama ilivyopitishwa na kuomba bodi za mishahara kukutana ili kupanga viwango halisi vya vima vya mishahara.

Rais Magufuli alimtaka waziri mwenye dhamana ahakikishe bodi za mishahara zinakutana lakini vikao vyao visiwe vya kutumia fedha za serikali vibaya.

Kuhusu ombi la Tucta kuhusu watumishi wenye elimu ya darasa la saba, Rais Magufuli alisema serikali haina ubaguzi na kwamba takwimu zilizipo kati ya wafanyakazi 525,509, wenye elimu hiyo ni 98,615.

"Mmeomba kuhusu usalama sehemu za kazi na vyama vya wafanyakazi kwenye maeneo ya kazi, waajiri toeni mikataba ya ajira, mruhusu hivi vyama maeneo yenu, mamlaka hakikisheni sheria hizi zinafuatwa," alisema.

**CHANGAMOTO SERIKALI**

Rais Magufuli alisema changamoto iliyopo ni gharama za kuendesha serikali ambapo kila mwezi Sh. bilioni 580 hutumika kulipa mishahara kila inapofika tarehe 19, suala ambalo alieleza kuwa halikuwapo.

"Kiasi kilichobaki cha fedha kinalipa madeni ya mikopo, kushughulikia miradi hivyo mnaweza kuona tunabakia na kiasi gani kulipa madeni na kwenye miradi. Kiasi kidogo kinachobaki huwa tunajiuliza tukipeleke wapi, kama ambavyo mwenye mbegu anavyojiuliza wakati wa njaa atunze mbegu au azile au mfanyabiashara anavyojiuliza wakati wa mtikisiko wa uchumi atafune fedha zote au azitunze," alisema.

# KCMC, Mawenzi zatajwa kwa kunyanyasa wagonjwa

INATOKA UK. 3

katika kitengo cha bima za afya. Alisema zipo tabia za madaktari kuwachukua wagonjwa kwenye viti na kuongea nao hali inayoashiria mazingira ya rushwa.

"Kwa sasa tunaiomba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kulitazama upya suala hili kwa kuwa asilima 90 ya wananchi wenye hali ya kipato cha hali ya chini hunyanyasika na hata wengine kupoteza maisha," alisema Faustine Mroso.

Dk. Mghwira, aliitaja taasisi nyingine iliyokuwa mzigo kwa mkoa wa huo kuwa ni Jeshi la Polisi kitengo cha usalama barabarani, ambacho alidai kuwa ni kinara wa kula rushwa na kuwabambikizia makosa madereva hata pasipokuwa na kosa.

Alisema, kitengo hicho hakifanyi ukaguzi wa kina wa magari kama inavyotakiwa na badala yake wanaomba rushwa kwa madereva na kisha kuyaachia magari hayo, jambo linaloweza kuleta madhara kwa watumiaji wa vyombo hivyo.

"Ni lazima tufikie mahali tuone umuhimu wa kujituma tuwapo kazini na si kuomba rushwa kila mara kwa wananchi...Kamanda wa Polisi Mkoa fuatilia hawa, weka mitego yako ya siri katika kuhakikisha wanabainika vinara wa kupokea rushwa," alisema.

# Mbinu mpya ya ukeketaji yabainika

INATOKA UK. 4

polisi, siku ya pili tulimkuta amefichwa kwenye kichaka kando ya mto huo akiwa hajitambui na ameshapakwa dawa maalum na wazee wanatambika upande mwingine ili wakimaliza anatupwa kwenye mto wenye mamba," alisema.

Alisema walimuokoa binti huyo ambaye walimuweka kituo cha Masanga ambaye wiki iliyopita alijifungua mtoto wa kiume.

Mgani alisema mkoani humo ukeketaji hufanyika kila mwaka unaokagwanyika kwa mbili na ni msimu maalum, na kwamba kabla ya msimu upo ushirikiano mkubwa na jamii, lakini wakishapakwa dawa za kimila huwa wakali kiasi kwamba ni rahisi kujeruhi anayepingana na mila yao.

Aidha, alisema kabla ya msimu wa ukeketaji ambao ni mwezi wa 12 wanachaguliwa watoto wa kike na wakiume ambao wanatairiwa na kukeketwa mwezi wa 10, ikitokea wa kwanza kufanyiwa hivyo amefariki hupakwa madawa kwa ajili ya kuondoa mkosi na kutupwa ili mwili wake uliwe na fisi.

Kwa mujibu wa Meneja hiyo, kutoka mwaka 2008 hadi 2018 jumla ya mabinti 3,055 na ngariba 82 waliacha kazi hiyo ambayo huwaingizia Sh. milioni 27 hadi 28 kwa mwaka mmoja, na kwamba ni lazima kuwatafutia shughuli mbadala.

Alisema kuna wakati Waziri aliwakutanisha wazee wa kimila ambao walisaini makubaliano maalum, lakini msimu wa ukeketaji ulivyofika walitoa maelekezo jambo hilo kuendelea na wao wakaenda upande wa Kenya na baada ya msimu kwisha walirudi na walipoulizwa wakasema wamefanya wenyewe wazee wa kimila hawajahusika.

Alisema wakati mwingine huvizia nyakati za sherehe za kitaifa kama Mwenge, na wanafanya hivyo kwa kuwa wanajua polisi hawataweza kugawanywa pande zote, na kwa wakati huo walikeketwa zaidi ya wasichana 300.

Naye, Mkurugenzi wa Shirika la Empower Society Transform Lives (ESTL), Joshua Ntandu, alisema mkoa wa Singida kwa sasa wanakeketa watoto wachanga na kinyama kinachotolewa hutupwa kwenye zizi la mifugo wakiamini itaongezeka.

Alisema wanavyokeketa hutibu kidonda husika kwa kutumia mkojo wa ngariba ambaye ameshaacha kufanya mapenzi ambao huhifadhiwa kwenye kibuyu kwa siku saba, na baada ya hapo hutumika kusafishia kidonda cha mtoto mchanga.

Naye, Mkurugenzi wa Sauti ya Jamii Kipunga, Selemani Bishagazi, alisema eneo hilo linakaliwa na watu wengi kutoka mkoani Mara ambao wanaendelea na mila hiyo, na kwamba wanasiasa wengi waliogopa kuunga mkono ili wasikosane na wapigakura.

Alisema upo uhusiano mkubwa wa ukeketaji na umaskini kwa kuwa mtoto wa kike anaangaliwa kama ng'ombe (mali) na kwamba anatakiwa akue alete mali ili mtoto wa kiume akitaka kuoa aweze kupata mali za kwenda kuoa.

Alisema kwa mwaka jana wameokoa mabinti 34 wasikeketwe na mwaka huu wanawaandaa kutoa elimu ili wanawake

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga, alisema wamefikia uamuzi wa kuwa na umoja huo ili kuunganisha nguvu kutokana na ukweli kuwa kila mmoja anatoa elimu peke yake.

# Hofu ya tetemeko la ardhi

INATOKA UK. 5

Alisema hali hiyo ilitokea ndani ya dakika kama 3 hadi 4, lakini mpaka hali hiyo inatoweka hakuweza kujua kama ni tetemeko la ardhi kwa vile hajawahi kupata elimu ya tetemeko la ardhi linavyotokea na namna ya kujikinga.

Faraji Kimbeo, mkazi wa Ndanda mjini Masasi, alisema akiwa nyumbani ghafla alisikia mshtuko wa ardhi ukitokea ndani ya nyumbani yake lakini hata hivyo, hakufahamu kama ilikuwa ni tetemeko la ardhi, hivyo anaiomba serikali kutoa elimu hiyo kwa jamii.

Kimbeo alisema baada ya tukio hilo, alitoka nje na kuona baadhi ya watu wakikimbia ovyo bila kujua nini kimetokea na hata alipowauliza kilichotokea hawakujua ni tetemeko la ardhi.

Zanaibu Rajabu, mkazi wa Masasi Mtaa wa Wapiwapi, alisema akiwa nyumbani, huku watoto wake wakiwa wamelala chumbani kwao, ghafla alishtushswa na mtikisiko, huku bati za nyumba zikitikisika kwa kishindo.

Alisema aliona watoto wake wakikimbia kutoka chumbani hadi sebuleni, na kumueleza kuwa wamesikia kitanda chao kikitemeka na kuingiwa na hofu.

Alisema baadae alipigiwa simu na watu mbalimbali wakimuuliza kama nyumba yake imenusurika kutokana na tetemeko, ndipo alipofahamu kuwa lilikuwa tetemeko.

Naye Thumani Mussa, mkazi wa Mtaa wa Rest Camp mjini Masasi, alisema alihisi ni kimbunga aina ya Keneth kwa kuwa alishikwa na hofu kubwa baada ya nyumba yake kutetereka kwa zaidi ya dakika 10 hadi 15, na kwamba hakufahamu kama ni tetemeko la ardhi.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, alisema hakuna madhara yoyote kutokana na tetemeko hilo.

Alisema hajapokea taarifa yoyote kutoka sehemu yoyote kama kulikuwapo madhara.

Nipashe lilipomuuliza Mtaalamu wa matetemeko kutoka katika Idara ya Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST), Gabriel Mbogoni, alisema mitambo yao iliyopo Mtwara haikubaini tukio hilo isipokuwa wanafuatilia kujua nini kilitokea.

"Kwa kweli na mimi nimesikia tu watu wanazungumza katika mitandao, na mashine yetu ya kunakiri iko Mtwara kwa hiyo inamaanisha kwamba hata kama lilitokea Masasi halikuwa kubwa sana, ila tunafuatilia na tukipata taarifa kamili tutawajulisha," alisema Mbogoni..

**Imeandikwa na Hamisi Nasiri (Masasi) na Elizabeth Zaya (Dar)**

## HABARI KITAIFA

# NIC yatangaza uhakiki wa bima ya maisha

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC), limesema litahuisha taarifa za wateja wake wa bima za maisha kwa lengo la kuboresha huduma zake kwa wateja hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Sam Kamanga, alisema jijini Dar es Salaam kuwa, uhuishaji huo unatarajiwa kuanza keshokutwa na kumalizika Julai Mosi, mwaka huu.

"Madhumuni ni kuongeza ufanisi ili kutoa huduma nzuri zaidi kwa wateja wetu," Kamanga alisema.

Aliongeza kuwa wateja wote wa NIC wa bima za maisha zilizoiva na zinazoendelea, wanapaswa kufika kwenye ofisi za NIC zilizoko nchini kote ili shirika lihakiki taarifa zao.

Alisema uhakiki huo utafanyika kwa siku za Jumatatu hadi Ijumaa ndani ya kipindi cha miezi miwili iliyotengwa kwa ajili ya uhakiki.

Alisema ili kufanikisha uhakiki huo, wateja wanapaswa kuwasilisha nyaraka muhimu zinazohusu taarifa za mteja.

Alizitaja nyaraka hizo kuwa ni pamoja na fomu ya uanachama, picha mbili za passport, kitambulisho cha taifa au cha mpigakura na nakala ya kadi ya benki.

NIC ni shirika la umma lililoanzishwa mwaka 1963. Baadhi ya huduma za bima zinazotolewa na shirika hilo ni bima za maisha, bima ya mali na bima ya ajali.



Mama mchuuzi wa vitafunwa akiandaa chapatti kwaajili ya wateja wake, kando ya Barabara ya Uhuru, eneo la Buguruni Malapa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Tanzania yaahidi uhuru vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Prof. Palamagamba Kabudi, amehakikishia Jumuia za Kimataifa kuwa Tanzania itaendelea kulinda uhuru wa vyombo vya habari ambao umejikita katika misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukuza demokrasia na haki za binadamu kwa mujibu na muktadha wa nchini.

Prof. Kabudi aliyasema hayo jijini Dar es Salaam juzi, alipokutana na kufanya mazungumzo na Naibu Msaidizi wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Balozi Malika James, na kuongeza kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika na pengine duniani kuwa na vyombo vingi vya habari ambavyo vingi vinamilikiwa na watu binafsi na kwamba itaendelea kuuheshimu uhuru huo huku akivitaka vyombo vya habari kuheshimu uhuru na haki za watu wengine.

"Tutaendelea kuulinda uhuru wa vyombo vya habari, lakini uhuru ambao umejikita katika misingi ya katiba yetu, pia uhuru ambao utaheshimu haki za watu wengine," alisema.

Kuhusu suala la demokrasia nchini, Prof. Kabudi alisema kuwa Tanzania itaendelea kukuza demokrasia kwa mujibu wa muktadha na mazingira ya nchi ambayo huenda ikawa ni tofauti na nchi nyingine ikiwamo kutoruhusu ukabila, udini na ubaguzi wa aina yoyote na kuongeza kuwa vitu hivyo ni muhimu katika kukuza demokrasia ya nchi.

"Pamoja na kwamba sisi sote ni Waafrika, ziko nchi zaidi ya 50 huku kila nchi ikifanya na kujiamulia mambo yake tofauti na nchi nyingine hivyo wasitumie vigezo na muktadha wa nchi nyingine katika kuitathmini Tanzania," alisema.

Aidha, alisema licha ya Tanzania kuhakikisha inaimarisha uhuru wa vyombo vya habari na kukuza demokrasia pia inaimarisha haki za binadamu nchini kwa kutumia taasisi zilizopo na kuruhusu uhuru wa mahakama.

Katika mazungumzo hayo, Prof. Kabudi na Balozi James, wamekubaliana kuwa mataifa hayo mawili yaendelee kujadiliana, kuzungumza, kutembeleana na kushirikiana katika nyanja mbalimbali za maendeleo kwa faida ya wananchi wa mataifa yote mawili na kumuomba Balozi James kuhamasisha wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Marekani kuja kuwekeza na kufanya biashara hapa nchini kwa kuwa mazingira ya biashara na uwekezaji yameboreshwa zaidi.

# Kampuni ya Kitanzania yaula

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Kiluwa Group, imesaini makubaliano ya ushirikiano na uwakilishi na Kamisheni ya Uchumi na Biashara kati ya China na Afrika katika nchi nane za Afrika.

Lengo la kusaini makubaliano hayo ni kusimamia ujenzi wa maeneo maalum ya viwanda kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji barani Afrika na kutoa fursa za kukuza na kurahisisha mazingira ya uwekezaji hasa katika miundombinu.

Akizungumza wakati wa kusaini makubaliano hayo yaliyofanyika jijini Beijing, nchini China, Rais wa Kamisheni Uchumi na Biashara kati ya China na Afrik, Huan Zhaojin, alisema kampuni ya Kiluwa Group itakuwa muwakilishi na kiungo muhimu wa shughuli za uwekezaji zinazosimamiwa kamisheni hiyo katika nchi nane kwa Afrika.

Alisema Kiluwa Group itaiwakilisha kamisheni kusimamia ujenzi wa maeneo ya viwanda katika nchi nane kwa Afrika ambazo ni Tanzania, Uganda, Rwanda, Msumbiji, Malawi, Congo-DRC, Burundi pamoja na Zimbabwe.

"Tunataka kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji wa viwanda barani Afrika sambamba na kutoa fursa za kukuza na kurahisisha mazingira ya uwekezaji hasa katika miundombinu," alisema Zhaojin.

Aliongeza kwa nchi nyingi za Afrika zina uhitaji mkubwa wa mazingira mazuri ya uwekezaji wa viwanda, urahisi katika uwekezaji hasa ya miundombinu, hivyo ni wakati sahihi sasa kwa nchi za Afrika kuanza kujenga maeneo ya viwanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kiluwa Group, Mohamed Kiluwa, alisema yuko tayari kuanza kazi hiyo ya ujenzi wa maeneo ya viwanda kwa haraka.

Alisema ni wakati mwafaka kwake kuanza ujenzi wa miradi hiyo katika nchi hizo nane Afrika kwa sababu tayari amekuwa na uzoefu mkubwa katika suala zima la uwekezaji na wawekezaji.

"Nimeingia makubaliano ya kujenga 'industrial parks' za kisasa katika nchi hizo nane, baada ya Kamisheni hiyo kuona Kampuni ya Kiluwa Group inafaa kulibeba jambo hili na kwa uzito mkubwa katika masuala mazima ya uwekezaji na sisi tupo tayari kuianza kazi hiyo mara moja na tayari tumeishakubaliana kwa pamoja, Kiliwa alisema.

Alisema baada ya kumaliza makubaliano hayo, anarudi nchini kujipanga na kuianza kazi hiyo mara moja kulingana na uhitaji mkubwa wa wawekezaji na uwekezaji katika nchi za Afrika kwa kuanza na nchi nane zilizotajwa.

Kamisheni ya China-Africa Economic and Trade Commission yenye makao yake jijini Beijing nchini China, ilianzishwa mwaka 1991 chini ya Wizara ya Mambo ya Nje kwa kuunganisha kampuni mbalimbali za kichina na wakurugenzi wake.

Lengo la kuanzishwa kwake ni kusimamia na kuzitafutia fursa kampuni mbalimbali za uwekezaji nje ya China.

# Kampuni tatu zajitokeza kuwekeza kusindika chai

**Na George Tarimo,** IRINGA

KAMPUNI tatu kubwa za chai kutoka nchi za Afrika Mashariki, zimejitokeza kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika chai katika wilaya ya Kilolo mkoani Iringa.

Kampuni hizo ni Dl group ya Kenya, Rwandan Mountain tea Ltd ya Rwanda, na E- vision Consulting ya Tanzania Ltd ambayo yamekuja Iringa baada ya mkoa kuwaita wawekezaji wa chai wilayani humo ili kuwanusuru wakulima wa chai wa wilaya hiyo.

Ni mkutano ambao uliwakutanisha wawekezaji hao na uongozi wa mkoa wa Iringa ikiwa ni moja ya juhudi za serikali za kufufua kiwanda cha chai kilichopo wilayani humo kilichosimamisha uzalishaji kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita na kuwasababishia wakulima hasara kubwa.

Katibu Tawala wa mkoa wa Iringa, Hapiness Seneda, aliwashukuru wawekezaji walioijitokeza, akisema hatua hiyo inaashiria nia ya dhati ya kuwasaidia wakulima wa chai wa wilaya hiyo.

Seneda alisema baada ya majadiliano ya muda mrefu walikubaliana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kwamba watafute namna iliyo wazi ya kumpata mwekezaji ambaye anaweza kuendeleza zao la chai.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, aliwahakikishia wawekezaji hao mazingira wezeshi ya kuwekeza ikiwamo umeme wa uhakika, barabara zinazopitika na maji katika maeneo watakayowekeza.

"Ni wahakikishie kwamba haya mliyoyasema ya barabara yatakwenda kufanyika hivi sasa tunavyozungumza mkandarasi yupo barabarani kilometa 32 Iringa-Kilolo inafanyiwa kazi na tumeamua kufanya kwa wazi ili wawekezaji wasishindwe kufanya uwekezaji," alisema Hapi.

Kwa upande wao wawekezaji hao walisema wana matumaini makubwa ya kufanya biashara na serikali ya Tanzania, huku wakitoa bei nzuri kwa wakulima wa chai.

Dk. David Langat, Mwenyekiti Mtendaji kampuni ya Dl, alisema wapo tayari kufanya kazi kama wakipewa huku wakishukuru uongozi wa mkoa na serikali kwa kuwahakikishia miundombinu rafiki.



Kaimu Mwenyekiti Kikosi kazi upande wa Umma, Joseph Simbakalia akizungumza kwenye kikao cha Kikosi kazi cha Viwanda ambacho ni moja ya kikosi kilichoundwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kujadili changamoto na masuluhisho mbalimbali kuelekea Tanzania ya uchumi wa kati jijini Dar es Salaam. (Kushoto) ni Mwenyekiti mwenza Kikosi cha Viwanda kwa upande wa Sekta Binafsi, Ali Mufuruki. **MPIGAPICHA WETU**

# Sababu RC kugoma kuweka jiwe la msingi

**Na Rose Jacob,** KWIMBA

MKUU wa mkoa wa Mwanza, John Mongella, jana aligoma kuweka jiwe la msingi katika mradi wa maji katika kijiji cha Kadashi Kata ya Maligisu wilayani Kwimba mkoani humo, kufuatia malalamiko ya wananchi kukosa maji kwa muda mrefu.

Mongella alikataa kufanya hivyo akiwa katika ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo katika wilaya za Kwimba na Magu, baada kuweka jiwe la msingi katika Shule ya Msingi Maligisu ambapo vyumba vitatu vya madarasa vyenye thamani ya Sh. milioni 60 vilikuwa vimejengwa na serikali na hapo akakumbana na kero za wananchi katika eneo hilo.

"Mradi huu ulikuwa wa miezi sita na ulianza kutekelezwa Oktoba katika mwaka wa fedha 2013 hadi 2014, lakini mpaka sasa ni miaka sita haujakamilika, hivyo sitoufungua, siwezi kuona uzembe mkubwa katika miradi ukiendelea wakati Rais anatoa fedha za maendeleo kwa ajili ya wananchi, halafu watendaji wanafanya mizaha, mimi siwezi kukubali kuona udanganyifu huu," alisema Mongella. Aidha, Mongella alimtaka mhandisi aliyepatiwa kazi hiyo Mapengu Juma na mkandarasi M/S D4N Co Ltd anayetekeleza mradi huo kwa gharama ya Sh.540,848,924 kuhakikisha ifikapo Julai Mosi, mradi huo uwe umeshakamilika, huku akimwagiza mhandisi aliyekuwa akisimamia mradi huo, Boaz Pius, akabidhi ofisi haraka na leo awe amesharipoti ofisi kwake.

Aidha, Mongella alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Pendo Malabeja, kuainisha fedha anazodai mkandarasi wa mradi huo ili waweze kuwasiliana na mamlaka husika imlipe na aendelee na kazi. Kijiji cha Kadashi ni kati ya vijiji 119 vinavyounda Wilaya ya Kwimba na kati ya vijiji 12 vilivyo katika utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini, wakazi wapatao 7,360 ambao wako katika kaya 1,227 watanufaika na huduma hiyo utakapokamilika.

Naye Mkuu wa wilaya hiyo, Senyi Ngaga, alisema mkandarasi anatekeleza mradi huo kwa gharama ya Sh. 986,253,345.00 ambayo inajumuhisha vijiji viwili vya Kadashi na Isunga.

Hadi sasa mkandarasi ameshalipwa Sh. 283,189,896.00 na utakapokamilika utaendeshwa na jamii yenyewe kupitia chombo cha watumia maji.

# Walengwa wa Tasaf wahimizwa usimamizi

**Na Elizabeth Zaya**

WANUFAIKA wa Mpango wa Kunusuru Kaya maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umewasisitiza wanufaika wa mpango huo kutumia vizuri miradi wanayoanzishiwa ili kujiongezea kipato.

Kauli hiyo ilitolewa na Afisa Ufuatiliaji wa miradi ya TASAF, katika Halmashauri ya Njombe na Wanging`ombe, Edwin Mlowe, katika ziara maalum ya kukagua miradi inayotekelezwa na mfuko huo katika mkoa wa Njombe.

Mlowe alisema mbali na mpango wa uhawilishaji fedha ambao umekuwa ukiwapatia fedha kaya masikini kwa ajili ya kujikimu, pia wamewanzishia miradi mbalimbali ambayo lengo lake ni kuwasadia kujiongezea kipato na kuwaondoa katika hali hiyo ya umasikini.

Mlowe alisema miongoni mwa miradi ambayo kaya hizo zimeanzishiwa ni pamoja na kilimo cha parachichi, mahindi, maharage na alizeti.

Miradi mingine alisema ni ufugaji wa Kuku, Ng`ombe, na Nguruwe, mifugo ambayo kila mlengwa alipewa kwa ajili ya kufuga mwenyewe kwa ajili ya kujiongezea kipato.

"TASAF pamoja na kuwapatia fedha walengwa hawa wa kaya maskini, lakini pia huwa tunawatembelea mara kwa mara kufanya tathmini kuangalia hali ya maisha yao, kama kuna mabadiliko au laa, kwa sababu lengo letu ni kuona familia hizi zinabadilika na siyo kubaki vile vile," alisema Mlowe na kuongeza:

"Kwa hiyo katika tathmini hiyo tulibaini wanahitaji miradi mingine ya ziada kwa ajili ya kuinua kipato chao, na ndiyo maana tukawaanzishia miradi na mpaka sasa tumeshaanza kuona matunda, wengi wameanza kunufaika na miradi hiyo na ndiyo maana tunaendelea kuwasisitiza waisimamie vizuri kwa sababu ndiyo itakuwa mkombozi wao katika hali ya umasikini."

Mnufaika wa miradi hiyo, Getrude Mgihirwa, alisema TASAF ilimsaidia kumpatia mradi wa kuku na Ng`ombe ambao mpaka sasa umemwezesha kununua shamba hekta tatu, kujenga nyumba moja na kugharamia ada ya mtoto wake.

# Waiomba TRA kuanzisha dawati kushughulikia changamoto

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

UMOJA wa Mawakala wa Forodha (TAFFA), Kanda ya Kaskazini, umeishauri Mamlaka ya Mapato (TRA), kuanzisha dawati maalumu la kushughulikia changamoto zinazowapata zikiwamo za mifumo ya mawasiliano ili kuwapunguzia gharama za kwenda mara kwa mara jijini Dar es Salaam.

Katibu wa umoja huo Kanda ya Kaskazini, David Koyya, akizungumza katika mkutano mkuu wa mwaka alisema, kumekuwa na mkanganyiko wa namna ya kuwasiliana na taasisi za serikali, wanapokuwa katika majukumu ya kuwahudumia wateja wao ambao wanapenda mizigo yao ifike kwa wakati. "Umoja wetu unalenga kuwahudumia wateja wetu vizuri, lakini sisi ni sehemu katika mchakato huo, ili ukamilike kuna upande wa taasisi za serikali ambazo ni Shirika la Viwango nchini (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Mamlaka ya Mapato (TRA), ambao tunatarajia watimize wajibu wao kwa wakati," alisema.

Alisema umoja huo una wanachama wanaofanya kazi katika vituo vya forodha kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), kituo cha forodha Namanga wilayani Longido na kituo cha forodha cha Holili Mkoa wa Kilimanjaro, vilivyopo mpakani na nchi ya Kenya.

Katibu Msaidizi wa Taffa, Michael Kwai, aliwataka watoa huduma za forodha katika mikoa ya kanda ya kaskazini, kujiunga na umoja huo ili uwe na nguvu katika kuwasiliana na serikali, ili kazi yao ifanyike kwa njia ya kitaalamu na kujenga imani kwa wateja.

"Tunataka tuwe na umoja wenye nguvu, mikoa yetu ina wafanyabiashara waliosajiliwa na TRA kufanya kazi za forodha, ambao kimsingi kila mmoja alikuwa akikutana na changamoto alikuwa akikabiliana nazo binafsi na kwa gharamu zaidi, lakini tukijiunga wengi umoja unakuwa na nguvu," alisema Kwai. Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Arusha Freight and Transport Agency Ltd, Aloyce Kilasara, alisema shughuli za upokeaji na usafirishaji wa mizigo zinapaswa kufanywa kwa weledi na kwa wakati, ili kuwawezesha wateja wao kufikia malengo yao.

Alisema wakati mwingine wateja wao wamekuwa wakiwalalamikia kuchelewesha mizigo yao, wakati tatizo linakuwa ni ucheleweshaji wa nyaraka mbalimbali unaosababishwa na mifumo ya mawasiliano ya kompyuta kutokufanya kazi kwa ufanisi muda wote.

Kuhusu ucheleweshaji wa mizigo kutokana na nyaraka kutotolewa kwa wakati, Meneja Msaidizi wa TRA, anayeshughulikia Forodha, Godfrey Kitundu, alisema lengo la mamlaka hiyo ni kushughulikia mizigo kwa wakati, ili kukusanya kodi na pale wanapokutana na changamoto za kimfumo, wamekuwa wakizipatia ufumbuzi kwa wakati.

Alisema mizigo yote yenye thamani ya zaidi ya dola 2,000 imekuwa ikifanyiwa tathmini jijini Dar es Salaam na kwakuwa mizigo mingi ina thamani hiyo kumekuwa na mlolongo wa kuichakata kwa kasi inayoridhisha na mawakala wa forodha wamekuwa wakiona tofauti ya kushughulikia mizigo yao na kwamba wapo tayari kuanzisha madawati kwaajili hiyo.

Katika mkutano huo walichaguliwa viongozi wataongoza umoja huo kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo, ambao ni Anschar Mushi (Mwenyekiti), Ramadhani Lema (Makamu Mwenyekiti), David Koyya (Katibu), Michael Kwai (Katibu Msaidizi), nafasi za wajumbe ni Dickson Lyimo, James Mwacha, David Msigwa, Geoffrey Mboya, Ben Mushi na Aloyce Kilasara.



Mamia ya wananchi kutoka kata tano za Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, wakiwa wamekusanyika katika mkutano wa hadhara, uliofanyika katika Kijiji cha Shiboro, Kata ya Sambasha juzi, kupinga hatua ya halmashauri hiyo, kuchukua chanzo cha maji cha mto Ngarenarok bila ya kuwashirikisha. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Wananchi Simanjiro waneemeka mradi wa maji

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MANYARA

WANANCHI wa vijiji vya Olchoronyori na Lorbene wilayani Simanjiro mkoani Manyara, walioukuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji na kufuata huduma hiyo kilomita 20 kwa punda, wameondokana na adha hiyo baada ya kupatiwa mradi wa maji.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. milioni 30, umewezeshwa na mdau wa maendeleo, Said Nassoro, maarufu kama Mzee Mwarabu na kuwapunguzia mwendo wa kufuata maji kwenye vyanzo vilivyopo milimani.

Nassoro (mzee mwarabu) alisema ataendelea kusaidia jamii hiyo ili kuondoa adha ya maji kwenye eneo hilo.

Alisema kwa kadiri atakavyoweza kwa kuangalia mahitaji muhimu ya kibinadamu ya maji, atahakikisha jamii hiyo ya kifugaji inapata huduma hiyo.

Alisema alishachimba visima viwili vya maji vyenye urefu wa mita 180 vya gharama ya Sh. milioni 60 na kuvikabidhi serikalini kwenye Kijiji cha Kitwai, wilayani Simanjiro. Kiongozi wa kimila wa jamii ya kifugaji wa kimasai wa eneo hilo, Laigwanani Kipara Simangu, alimshukuru mdau huyo wa maendeleo, kwa kufanikisha ujenzi wa kisima hicho kitakachowasaidia wafugaji hao.

Simangu alitoa wito kwa wawekezaji wengine kuiga mfano wa mdau huyo na kusaidia jamii ya maeneo wanayowekeza na kufanya shughuli zao.

"Awali wananchi walikuwa wanatembea umbali mrefu wa kilomita 20 kwenda kwenye vyanzo vilivyopo milimani na kurudi kilomita 20, kwa kutumia punda, lakini kwa sasa changamoto hiyo imemalizika," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Lorbene, Elisha Njaram, alisema changamoto ya maji kwenye kijiji hicho ilikuwa kubwa, lakini hivi sasa jamii ya eneo hilo itapata maji kwa ukaribu zaidi tofauti na awali. Njaram alisema wanawake wa eneo hilo walikuwa wanatembea umbali mrefu, kufuata huduma ya maji kwa kutumia punda, lakini wameondokana na adha hiyo baada ya mwekezaji huyo kuwachimbia kisima.

"Wilaya ya Simanjiro inakabiliwa na uhaba wa maji hasa kwenye nyanda kame, lakini wadau wa maendeleo wakishirikiana na serikali watafanikisha upatikanaji wa maji kwa sehemu kubwa," alisema.

# Ujenzi holela wasababisha mafuriko Arumeru

**Na Woinde Shizza,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amekemea ujenzi holela wa kuzuia njia za asili za kupitisha maji kunakofanywa na wananchi wake na kuwataka kufungua njia hizo ili kuepukana na mafuriko yanayowakumbuka kila mara mvua zinaponyesha.

Muro alisema hayo wakati akiongea na wananchi wa wilaya hiyo, waliokumbwa na mafuriko yaliyotokana na kunyesha mvua usiku wa kuamkia jana.

Alisema ujenzi holela ndio umesababisha mafuriko hayo, kwa kuwa baadhi ya wananchi wamejenga nyumba katika njia asili zakupitishia maji.

"Maji hayazuiwi hata siku moja tunapojenga lazima tuzingatie miundombinu ya maji, sasa ujenzi holela tuliofanya matokeo yake leo ni haya mafuriko tunayaona, vitu vimeelea na baadhi ya mali kuharibika," alisema.

Aliwataka wananchi wote waliojenga mabondeni na kuzuia njia asili za maji, kubomoa mara moja ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

"Mimi nadhani hii mara ya pili tatizo hili kutokea, mwaka jana lilitokea tena na tulikaa na kukubaliana kuvunja kuta zote ambazo zinazuia maji kupita kwenye mkondo wake, hivyo basi najua kuna watu wataathirika, lakini inabidi ili tuweze kutatua tatizo kubwa linaloweza kutokea hapo baadaye," alisema Muro

Aliwataka wananchi kufuata sheria za ujenzi wa mipango miji na kuacha kujenga kiholela ili kuondokana na adha ya majanga.

Mmoja wa wananchi aliyeathirika na mafuriko hayo, Rose Nassari, aliishukuru serikali kwa kuwatembelea na kuwapo pole pamoja na kuwapa elimu ya hasara ya kujenga kwenye mikondo ya maji.

Mafuriko hayo yamekumba katika baadhi ya kaya za vijiji vya Nduruma pamoja na Shangarai na kuharibu mali na baadhi ya mazao kama migomba, pamoja na miundombinu ya barabara.




Ofisa Tarafa ya Moipo, Joseph Mtataiko (kulia), akisoma mabango ya watumishi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, jana. Kushoto kwake ni Ofisa Mtendaji wa Mji huo, Evence Mbogo. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wadau wa ngozi waombwa elimu uchunaji kwa wafugaji

**Na Mary Mosha ,** MOSHI

WAKATI serikali ikijipanga kuingia katika uchumi wa viwanda, wadau wa sekta ya ngozi wameombwa kutoa elimu juu ya uchunaji ngozi ili kuwawezesha wafugaji kuzalisha bidhaa bora.

Umuhimu huo unatokana na baadhi ya wachunaji wa ngozi kutokuwa na elimu ya kutosha, jambo ambalo limepelekea ngozi inayochunwa kuwa na kasoro mbalimbali kama kuwa na matobo hali, hivyo kushuka thamani ikilinganishwa na inayotoka nchi jirani

Sabas Woisso, mkurugenzi wa kiwanda cha ngozi cha Himo Tanaries (HITA), alisema kumekuwapo na changamoto kubwa katika uchakataji wa ngozi, huku kasoro zilizoonekana zikichangia kushuka kwa bei ya bidhaaa hiyo kila mwaka.

Woiso aliongeza kuwa katika hatua za kwenda katika uchumi wa viwanda, lazima kujinga na kuhakikisha kuwa kunakuwa na malighafi nzuri za kutosha katika viwanda ili fedha zinazopatikana zimrudie mfugaji moja kwa moja

Kwa mujibu wa Woisso, bado kuna uelewa mdogo kwa wafugaji juu ya kutunza ngozi ili ziweze kuwa na bei katika soko la dunia, na bado katika maeneo mengi wafugaji hawana uelewa wa kutosha juu ya uchunaji pamoja na uhifadhi.

"Ng'ombe unakuta wanapigwa chapa sehemu zisizo maalumu au unaenda mchinjioni unamkuta mchunaji kalewa chakari, anatoboa toboa ile ngozi bila sababu yoyote...sasa hii inashusha thamani ya ngozi," alisema Woisso.

Aliitaka serikali kujenga mikakati katika kuinua sekta ya ngozi nchiniikiwamokuwajengea uwezo juu ya kutengeneza bidhaa za ngozi sambamba na utafutaji wa masoko.

Alisema kinachofanyika sasa kwa watengenezaji wa bidhaa za ngozi ni kujitafutia elimu wenyewe au kulazimika kutafuta wataalam nje ya nchi kitu ambacho bado ni gharama kwa wazalishaji hao. Woisso aliishukuru serikali kwa jitihada ambazo imeonyesha kwa kusisitiza kununua bidhaa za ndani kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kufanya wajasiriamali wa ndani kukuza mitaji yao tofauti na kuendeleza kuagiza kutoka nje ya nchi.

Nao baadhi ya wachinjaji katika machinjioya Kiboloroni Manispaa ya Moshi, Edwin Wenzesilaus, alisema bado elimu sio rafiki kwa wachinjaji, hali ambayo inasababisha uharibifu wa ngozi.

# Rombo wahimizwa kufanya biashara halali

**Na Mary Mosha,** ROMBO

MKUU Wilaya ya Rombo, Agnes Hokororo, amewataka wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wilayani humo waliokidhi vigezo vya kupatiwa vitambulisho kuhakikisha wanafanya biashara halali na kuepukana na magendo.

Aliyasema hayo wakati akiongea na Nipashe juu hali ya zoezi la ugawaji wa vitambulisho lilipofikia katika wilaya hiyo.

Alisema kutokana na wilaya hiyo kuwa mpakani mwa nchi jirani ya Kenya zipo changamoto za baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kupitisha bidhaa kinyume cha sheria na taratibu za nchi hawatalifumbia macho licha ya kuwa na kitambulisho.

"Ipo dhana iliyojengeka kuwa kitambulisho hicho ni cha kufanya biashara zote, kwa yeyote tutakayembaini, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aidha aliwataka kuhakikisha kitambulisho hicho kinatumiwa na mtu mmoja, na aliiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufuatilia mara kwa mara.

Meneja wa TRA wilaya ya Rombo, Hermance Nghase, aliwataka wafanyabiashara hao kuhakikisha wanatunza kumbukumbu ili kuona namna biashara zao zinavyoenda kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Wafanyabiashara wadogo mnayo nafasi kubwa ya kufanya mabadiliko katika biashara zenu na katika kipindi cha mwaka unaofuata mkalipa mapato TRA na kuongeza uchumi wenu na wa taifa kwa ujumla," alisema Nghase.

Catherine Swai, mfanyabiashara, alisema kupewa kwa vitambulisho hivyo kutaweza kuwasaidia kusimamia biashara zao na kuziboresha, huku wakiomba serikali kutoa mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wafanyabiashara hao.

"Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutusaidia wafanyabiashara wadogo, ila tunamuomba kuziagiza halmashauri hizo kutupa mafunzo na namna bora ya utunzaji wa kumbukumbu ili mwakani tuwewe kufikia malengo ya biashara zetu," alisema.

# Waomba kutatuliwa kero maji

**Na Mary Mosha,** SIHA

WANANCHI wa Kitongoji cha Mwangaza na Kaloleni, Kata ya Ngarenairobi, wilaya ya Siha, wameiomba Serikali kuwatatulia kero ya upatikanaji wa ardhi iliyopimwa ili waweze kujenga makazi bora na salama.

Kwa kufanya hivyo, wataondokana na tatizo la nyumba zao kuungua mara kwa mara kutokana na msongamano wa nyumba za mbao.

Kadhalika, wananchi hao wameiomba serikali kuwasaidia Sh. milioni 2.8 zisaidie upatikanaji wa majisafi na salama kwa kuwa wananchi wamechanga Sh.800,000 na nyingine zimeshindikana na kuiomba serikali isaidie kutatua kero ya maji.

Wananchi hao walitoa ombi hilo jana kwa Mbunge wa Viti Maalumu, Shally Raymondi Mushi, wakati alipokuwa akizungumza na wananchi namna ya kujikwamua kwenye umaskini.

Hadija Ngajiro, mkazi wa kitongoji cha Mwangaza Kata ya Ngarenairobi, alimuomba mbunge huyo kusaidia kinamama na vijana kupatiwa mikopo kwa muda muafaka na kukopeshwa viwanda vidogo vidogo ili waweze kujikomboa na umaskini. Alisema nyumba nyingi za wakazi zimekuwa zikiungua mara kwa mara kutokana na msongamano wa nyumba za mbao zilizopo, na hali hiyo inachangiwa na ardhi yao kutokupimwa na kujenga makazi bora na kuiomba serikali kuwasaidia kuwapimia viwanja ili kujenga makazi bora.

"Utakuta nyumba moja ikiwaka moto nyumba nyingine zinashika moto kutokana na msongamano wa nyumba uliopo kwani hata dharura inapotokea magari ya kutoa huduma yanashindikana kuingia kutokana na kukosekana na barabara za kuingia na kutoka katika makazi hayo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Prosper Kenani ,alisema wananchi wa kitongoji hicho wanakabiliwa na kero ya upatikanaji wa majisafi na salama na wamechanga sh. 800,000 ili kutatua kero hiyo bila mafanikio na kuiomba serikali kusaidia utatuzi wa kero hiyo.

Akijibu hoja hizo Mbunge huyo alisema serikali inazifanyia kazi kero zote zilizopo katika kata hiyo na hivi karibuni zitapatiwa ufumbuzi wake ikiwamo kero ya maji na kuwa na makazi yaliyopimwa ili wananchi waweze kutumia hati hizo kufanyia shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo kuchukulia mikopo benki.

# ama

**ALHAMISI MEI 2, 2019** AFYA NA MAZINGIRA






Ukurasa 14

**Staili ya kupunguza sukari pasipo kuathirika**

Ukurasa 15

Fahamu ilivyo muhimu 'kuteta' na mtoto tumboni

Ukurasa 17

**Bingwa anayetibu kansa matiti, naye anaumwa**

# Mabingwa mifupa wafunguka madhara wake kwa waume wanaovunjika viuno

Ukurasa 16

# Staili ya kupunguza sukari pasipo kuathirika

WATAALAMU wa afya wamekuja na mbinu sahihi ya mtu kuondokana na matumizi ya sukari, kwamba inapofanywa kwa kupunguza taratibu vijiko anayotumia kila siku, anafikia hatua nzuri.

Timu ya wataalamu kutoka vyuo vikuu vya London na Leeds, wamefanya utafiti wa wastani wa miezi 64 au sawa na miaka mitano na theluthi moja, kukaonekana matokeo chanya.

Katika mgawanyo wake, ambao waligawanywa katika makundi mawili, walioacha ghafla na walioacha taratibu. Imebainika kwamba, pamoja na punguzo hilo la sukari, bado wahusika wamendelea kufurahia kinywaji chao.

Walioacha taratibu, jumla yao wako asilimia 42 na waliopunguza ghafla ni asilimia 36

Watafiti wana maoni kwamba, mbinu hiyo ya kuacha au kupunguza matumizi ya sukari katika vinywaji vinginevyo

Hivi sasa wadau wa masuala yanayohusiana na kupiga vita vitambi, wamelichukua hilo kwa uzito mkubwa ili walidhibiti.



Kikombe cha chai. **PICHA: MTANDAO.**

## AFYA



Mtu akiwa katika uso wa kuzama mbali kihisia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Hisia saba zilizobadilika

MARA nyingi watu hufikiria hisia za binadamu ni moja duniani kote na zinafanana. Lakini ukweli ni kwamba, zinatofautiana na zinabadilika kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Pia, inaelezwa kuwa hisia mpya zinagunduliwa kadri muda unavyosonga, kwa mfano hisia inayompata mtu akiwa na hofu ya kukosa kuhudhuria shughuli aliyokuwa ameikamia.

Hiyo imevumbuliwa kutokana na ujio wa mitandao ya kijamii, anayopata mtu akiona picha mitandaoni na watu waliohudhuria hafla, anayotazamia kuhudhuria. Inaitwa FOMO (Fear of Missing Out).

Dk. Sarah Chaney, Mtaalamu wa Kituo cha Historia ya Hisia, nchini Uingereza, amebaini hisia za zamani zinazosaidia kuelewa jamii inavyoishi sasa. Hizo ni pamoja na:

> **Siku hizi hisia hiyo inajulikana kama msongo wa mawazo.**

Mosi, msongo wa mawazo; ni hisia iliyohusishwa na viongozi wa kidini, wanaoishi chini ya kiapo cha kidini.

Anapotetereka kiimani, mwathiriwa hujihisi amepoteza matumaini, wakati azma yake ni maisha takatifu.

"Siku hizi hisia hiyo inajulikana kama msongo wa mawazo," anasema Dk, Chaney.

"Lakini, hisia hiyo zamani ilihusishwa na mgogoro wa kiimani kwa watu walioamua kufuata mkondo fulani wa maisha, kwa kula kiapo cha uaminifu."

Pili, ghadhabu; mtu anapopandwa na ghadhabu, inakuwa vigumu kukaa kimya au kujituliza kwa muda huo. Inaeezwa zamani ilikuwa rahisi kuidhibiti, lakini siku hizi imekuwa vigumu.

Tatu, masikitiko; Hiyo ni hisia inayompata mtu anapotatizwa na jambo kisaikolojia.

Hadi karne ya 16, iliaminika afya ya mtu ilihusishwa na furaha aliyo nayo moyoni na hali hiyo ilionekana kupitia tabasamu lake usoni, lakini sasa sivyo.

Nne, kumbukumbu; zamani ilihusishwa na ugonjwa wa mabaharia au wahudumu wa meli katika karne ya 18.

Inaelezwa katika zama hizo mabaharia walipokabiliwa na hali ngumu safarini, walipatwa na hisia kukumbuka nyumbani, lakini zama zilizopo, watu hukumbuka utamaduni nzuri za jadi au ujana wao kwa furaha.

Tano, ni mshituko baada ya shambulio; Hilo huwatatiza sana askari, baada ya kutoka vitani. Hisia hiyo zamani ilihusishwa na wanajeshi waliopigana vita vikuu vya kwanza vya dunia.

Dk. Chaney, anasema wanaopatwa na hisia hiyo mara nyingi wanapoteza uwezo wa kusikia au mara nyingine hawaonyeshi dalili za kuwa na matatizo yoyote.

"Mwanzo wa vita, watu hao walidhani hali hiyo imetokana na wao kuwa karibu na milipuko iliyoathiri masikio yao. Lakini baadae, iligunduliwa ni hisia ya mtu binafsi wakati huo," anafafanua mtaalamu huyo.

Sita, hofu ya ugonjwa hatari; Katika karne ya 19, hisia kama hiyo ilihusishwa zaidi na msimamo wa mtu binafsi.

Katika mtazamo huo mtu anapatwa na hofu, pia maumivu makali katika mfumo mishipa. Na kupata matatizo ya akili.

Saba, msimamo wa maadili; Inatajwa ni kwa sababu muda mrefu eneo hilo lilihisishwa zaidi na msimamo wa kisaikolojia

AFYA

# Fahamu ilivyo muhimu 'kuteta' na mtoto anapokuwa tumboni

**Na Lilian Lugakingira,** Bukoba



Mjamzito akifurahi na tumbo lake. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

JE, unafahamu umuhimu wa kuongea na kucheza na mtoto akiwa tumboni?

Pamoja na jitihada za serikali na wadau wa makuzi ya watoto, wakijitihadi kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa mama na baba kuongea na mtoto akiwa tumboni, kuna mambo yanayotajwa kwenda kinyume.

Inaelezwa kwamba, bado kuna watu wasiofahamu na wasioona umuhimu huo. Wengine wanadhani ni maigizo. Kwa vipi?

**OFISA LISHE**

Ofisa Lishe Mkoa wa Kagera, Yusuph Hamis, anasema ni muhimu kuongea na mtoto akiwa tumboni, hasa kipindi mtoto anachoanza kucheza tumboni anakuwa na uwezo wa kusikia.

"Ni kipindi ambacho mzazi anapaswa aongee naye kumuasa vitu fulani, kumuusia kwamba mwanangu ukishazaliwa kuwa mtoto mzuri, msikivu na mpenda watu au kumwimbia nyimbo nzuri, hii inamsaidia mtoto kuwa mdadisi," anasema.

Anasema, hatua hiyo ya kuzungumza naye tumboni, inaufanya ubongo wa mtoto kutanuka.

Vivyo hivyo, anapozaliwa ni muhimu kumpa mtoto vitu vya kuchezea vyenye sauti na rangi, vinavyomsaidia kuwa na uwezo wa kfikiria na kuchanganua.

Hamisi anasema, ili kulihakikisha hilo linafanyika, wamekuwa wakitoa elimu kwa jamii kupitia njia mbalimbali, vikiwamo vyombo vya habari, jamii na vituo vya kutoa huduma za afya kupitia watoa huduma za afya.

"Tunazungumza nao, hasa wanawake wanapohudhuria kliniki na wanapokwenda kupata huduma nyingine. Hapo kuna uhakika wake kuwapata kwa wingi kupitia kitengo cha Early Child Development -ECD," anasema.

Hamisa anasema, kwa kutozungumza au kucheza na mtoto, kunaathari ubongo wa mtoto kuchelewa kukua na kutokuwa na uwezo wa kufikiri na kuchanganua mambo, hata anapokuwa mkubwa.

"Unapoanza kuuchangamsha akiwa mdogo, vitu kama figo, neva (nerves) na mishipa ya fahamu vinachangamka.

"Hii inamsaidia mtoto kufikirikwa upana, kuongeza udadisi na baadaye kupata wataalamu walio makini, wanaoweza kulisaidia taifa kusonga mbele," anasema.

Anatumia fursa hiyo kuwaasa wananchi kuzingatia elimu wanayopewa kuhusu namna ya kuzungumza na kucheza na mtoto hata akiwa tumboni, ili kupata watoto wenye uelewa mkubwa.

Ofisa Lishe huyo, anasema ana mpango wa kufanya tathmini, kuona elimu wanayoitoa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuzungumza na mtoto inapokewa vipi na mwitikio wake ukoje kwa sasa na kushauriana njia bora, zinazoweza kutumia ile timu kuwafikia wengi kwa urahisi.

> Utakuta mama na baba muda mwingi wanahangaika na masuala ya kazi, hawajipi muda wa kukaa na kuongea na mtoto.



Mama akitabasamu na mwanawe.

**MWANANCHI**

Jonesiah Kokwenda, mkazi wa Kijiji cha Kilimilile, Kata ya Kilimilile Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, anasema kuwa mara nyingi amekuwa akisikia kuna uwezekano wa kuzungumza na mtoto akiwa tumboni akakusikia, lakini haliamini jambo hilo.

"Mtoto yuko tumboni. Hajazaliwa, lakini naambiwa nikizungumza naye ataweza kusikia, itawezekana vipi kama si miujiza? Binafsi nadhani mtoto unaweza kuzungumza naye na kumuasa pindi anapozaliwa, kwa kuwa tayari unamuona, naye anakuona," anafafanua.

Grace Kato, mkazi wa kijiji hicho pia anaamini mzazi anapozungumza na mtoto, huwa anasikia kutoka tumboni na inaleta hatua ya kimaisha. Mama huyo anasema, amewahi kupata elimu kupitia wadau mbalimbali, ikiwamo mashirika binafsi na wahudumu wa afya ngazi ya jamii kuhusu mantiki ya kutumia elimu hiyo.

Anasema, alikuwa akitumia elimu hiyo kuzungumza na mwanawe tumboni na baada ya kuzaliwa, akiwa na imani kwamba aliyasikia yote aliyomweleza.

"Niliamini hilo kwamba mtoto ukimweleza kitu anasikia. Ndiyo maana, huwa tunaambiwa hata kama una tabia mbaya, mfano ya udokozi," anasema.

Grace anafafanua anasema: "Ukidokoa una mimba unaweza kuzaa mtoto kidokozi, kwa sababu anasikia hata akiwa tumboni."

Anatumia fursa hiyo kuwataka kinamama wenzake kuzungumza na watoto wao wakiwa tumbo ni kwa kuwaeleza mambo mema ambayo yatawasaidia kujenga maisha yao mara watakapozaliwa na kukua.

**MTAALAMU TABIA**

Sista Margaret Ishengoma, ni mtaalamu wa mabadiliko ya tabia katika lishe kutoka shirika la IMA World Health, kupitia kinachoitwa Mradi wa Mtoto Mwerevu, naye anasisitiza umuhimu wa mama na baba, kuongea na mtoto tangu akiwa tumboni

Anasema, pia wazazi wanapaswa kucheza na mtoto akiwa tumboni, ili aweze kujenga ubongo wake akiwa huko tumboni.

"Utakuta mama na baba muda mwingi wanahangaika na masuala ya kazi, hawajipi muda wa kukaa na kuongea na mtoto," anasema.

Sista huyo anasema kuwa, wazazi inabidi kuwapatia mtoto vitu vya kuchezea na anapozaliwa, kuwa si lazima viwe vya kununua madukani.

"Zamani vilitengenezwa kwa kutumia vitu mbalimbali mfano magome ya migomba, magome ya miti, cha muhimu ni kutafuta ambavyo ni salama kwa mtoto. Vitu hivi huyfanya ubongo wa mtoto kuchangamka," anasema.

Anasema, pia haifai kukuta mtoto anacheza akapigwa mateke, maana akiwa anacheza, anaufanya ubongo kuchangamka na kumkuzia sanaa ya ubunifu.

"Watanzania wengi wangekuwa wabunifu, nchi isingekuwa inaagiza mpaka njiti za kuchokonoa meno nje ya nchi kama China. Vitu vingi vimebuniwa na kutengenezwa hapa," anasema.

AFYA

# Mabingwa mifupa wafunguka madhara wake kwa waume wanaovunjika viuno

**Na Beatrice Shayo**

• Kifo cha papo kwa hapo kiko jirani • Inawezekana 'baibai' haki ya ndoa • Wa bodaboda 'wateja' wao wakuu

MOJA ya vitu vinavyochangia kuongezeka idadi kubwa ya watu kuvunjika viuno nchini, imetajwa ni watu kupata ajali mbaya na moja ya athari zake ni kushindwa kufanya tendo la ndoa.

Ni kauli ya Bingwa wa Mifupa, Kiuno na Kikombe cha Kiuno kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (Moi), Daktari Edmund Ndalama, anayesema ni tatizo linazozidi kuwa kubwa nchini.

Huku akishuari kinachotakiwa ni jambo linalotakiwa kuchukuliwa hatua madhubuti kulikabili na mambo yawekwe sawa, akitaja katika kituo chake cha kazi kila siku wanawahudumia wagonjwa watano, wenye hali isiyo nzuri.

"Tatizo la kuvunjika kiuno ni kubwa sana na inasababishwa na ajali; mtu kuanguka ama akiwa katika shughuli zake za kawaida bahati mbaya," anasema.

"Unakuwa unakandamizwa, yaani kitu kimoja unatembea kingine kinakukandamiza unavunjika kiuno," anafafanua.

Aidha, Dk. Ndalama anasema kuna aina 10 mivunjiko endapo zisipotibiwa mgonjwa anakwenda kuwekewa kiungo cha bandia.



Madaktari wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili wakimhudumia mgonjwa. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU**

### KUUMIA NYONGA

"Ukiwekewa jointi ya bandia katika umri mdogo, sio jambo nzuri. Tunajitahidi kuhakikisha mtu asiwekewe bandia," anasema Dk. Ndalama

Anaeleza kwamba, mfupa unaozunguka kiuno maarufu wanauita nyonga, mtu akiumia kutokana na ajali kubwa na mara nyingi wagonjwa wanapoteza, maisha hata kabla ya kufikika hospitali.

Anasema, kuna utaratibu wa kutumia shuka kumsaidia mgonjwa aliyevunjika kiuno na, ili ipate ahueni.

"Sehemu ya kiuno ni kitu kilichoachwa ukiangalia katika Afrika Mashariki ni kwamba Nchi ya Rwanda na Uganda hawana hayo matibabu.

"Hii ni kwa sababu wanajifunza kwa muda mrefu, pia ni ngumu sana, labda kwa vile ni hulka yetu kutokupenda kujifunza vitu vigumu,"anasema.

"Ni lazima watoke watu wa kufanya, akikosekana mtu wa kufanya, ina maana huyu aliyepata ajali katika hayo maeneo anakufa, huku unaongea akili yako inakuwa timamu, lakini unakufa kwa sababu unapoteza damu," anaeleza

Dk. Ndalama analitaja eneo hilo la matibabu, limeachwa muda mrefu, lakini sasa mafunzo yanaendelezwa na watakuwa wanawaita wataalamu kutoka nje ya nchi, kubadilishana uzoefu.

Tahadhari yake ni kwamba, mtu asipotibiwa ugonjwa huo, unaweza kufa ama kupata matatizo makubwa, ikiwamo kushindwa kufanya tendo la ndoa na kuishia kuathirika kisaikolojia.

> **Tatizo la kuvunjika kiuno ni kubwa sana na inasababishwa na ajali; mtu kuanguka ama akiwa katika shughuli zake za kawaida bahati mbaya.**



Bingwa wa Mifupa, Kiuno na Kikombe cha Kiuno, Daktari Edmund Ndalama,



Daktari mwandamizi wa mifupa, Billy Haonga.

"Utaona ni namna gani kisaikolojia unavyoathirika kwa kukosa tendo la ndoa. Hii sio kwa mwanaume tu, hata kwa mwanamke anapovunjika kiuno ya bila kutibiwa vizuri," anasema.

### AINA ZA AJALI

Daktari Mwandamizi wa mifupa, hospitalini Moi na Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (Muhas), Billy Haonga, anaorodhesha namna tofauti mtu anavyovunjika.

Katika hilo, mtu anavyovunjika na jinsi anavyohatarishwa miasha yake, kama hakutakuwepo hatua sahihi za kuokoa ma maisha yake.

"Kama mvunjiko umeenda kugusa kwenye mshipa mkubwa wa damu, hapa hatuna cha kufanya, mgonjwa atakufa pale pale alipopatia ajali.

"Ndio maana unaona mtu kagongwa (na gari), ghafla anakufa na hata kwenye ajali unaona wengine wanakufa na wengine wanapona," anasema.

Anaongezea:"Wale ambao wamekufa katika ajali, utakuta viungo muhimu vimeathirika, kama mishipa mikubwa ya damu imekatika au kuharibu mapafu au ubungo. Mishipa mikubwa ya damu ikikatia ni hatari wanakufa hapo hapo," anasema

Dk. Haonga anasema, kuna wanaovunjika mishipa midogo iliyobeba nyonga na mtu anajikuta anavuja damu taratibu. Anasema, mtu huyo huwa ana uwezo wa kufika hospitalini, lakini ni lazima apewe tiba ya haraka.

"Huyu mgonjwa ni lazima kuwepo na uharaka wa huduma ya kwanza kumshikilia, mifupa isiendelee kutanuka, kumpa maji, damu na kumpunguzia maumivu," anaeleza Dk. Haonga.

"Inahatarisha sana kuumiza viungo vya ndani kama figo, bandama, utumbo mishipa mikubwa damu na mishipa midogo midogo ikapanua mishipa ya nyonga, yaani ujazo wa ndani katika mfupa wa nyonga ukawa mkubwa.

"Hivyo, mgonjwa anaweza akatoka damu nyingi na kujaa katika hilo eneo akafa. Hii ndio 'mivunjiko' hatari kwa binadamu.

"Mifupa ya nyonga jinsi ilivyokaa ina mstari wake kama imekatika, halafu haujaunga, ina maana kwamba upande mmoja utakuwa juu na mwingine utakuwa chini.

"Tutamuona mtu anatembea na mguu mmoja mfupi na wengine kuendelea kutembea na maumivu miaka yote kama hakutibiwa vizuri," anasimulia Dk. Haonga.

### GHARAMA ILIVYO

"Kwa bahati mbaya, matibabu haya yanapatikana Tanzania katika taasisi ya Moi. Hivyo, aliyepata ajali mkoani Kigoma asipokuja Dar es Salaam, anaweza kubaki na kilema cha maisha," anatamka Dk. Haonga.

Anaainisha aina ya madhara, ni katika matokeo husika baadhi ya watu kuwa na mguu mrefu na mfupi, mguu usiokuwa na hisia, au kupata maumivu kutokana na eneo ambalo mtu kaumia linakuwa halijajiunga.

Mtaalamu huyo anasema, gharama kubwa ya tiba hiyo hiyo ni kwenye vifaa vya matibabu na kupatikna adamu iliyopotea kwa mgonjwa.

"Ni lazima damu iwepo, kwani inapokosekana, unapoteza uhai wa mgonjwa, hivyo kikubwa kinachotuathiri ni upatikanaji wa damu. Vile vyuma tunavyowawekea wagonjwa sio gharama kubwa," anasema.



Wataalamu wa maabara wakiwa kazini.

> **Ni lazima damu iwepo, kwani inapokosekana, unapoteza uhai wa mgonjwa, hivyo kikubwa kinachotuathiri ni upatikanaji wa damu. Vile vyuma tunavyowawekea wagonjwa sio gharama kubwa.**

Anasema, kuna wakati wanazaimika kutumia shuka ambalo gharama yake sio kubwa, wakati wa kutoa huduma ya kwanza, jambo la msingi watoa huduma wanajua namna ya kulitumia.

Daktari wa Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu wa Moi, William Mugisha, anasema wakiwa na mwendelezo wa matibabu tangu awali, ni kawaida daktari kufanya juhudi kuhakikisha anaiweka nyonga ya mgonjwa katika hali nzuri na inaposhindikana humfanyiwa upasuaji wa kubadilisha nyonga.

Anasema hivi karibuni, walikuwa na mkutano na wataalamu kutoka nchini India, ambao utasaidia kuwapa madaktari ujuzi na weledi wagonjwa kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu zaidi, kwani baadhi ya maeneo wanayamudu nchini.

Dk Mugisha anaasema, huwa wanashirikiana na wataalamu wa nchini India, kwa sababu ni nchi iliyopiga hatua katika tibna hiyo ya nyonga ma maeneo mengine.

### MKURUGENZI MOI

Mkurugenzi Mtendaji wa Moi, Dk. Respicious Boniface, anasema tatizo ukubwa kwa wagonjwa wanaopatiwa matibabu, imetokana na ajali za magari na pikipiki.

Anasema Moi ina watalamu wanaotibu ugonjwa huo wa nyoga, wengi wanatokea mjini kwenye barabara na kuna ajali nyingi.

Dk. Boniface, anaeleza kuwa madakatri alio noa bado ni wachache, ikilinganishwa na idadi ya wagonjwa wanaofika hospitalini kuhitaji huduma, lkaini wameweza kuwahudumia wote.

## Bingwa anayetibu kansa matiti, naye anaumwa

**Na Mariam Issimdar**

"KAMA walivyo wanawake wengi, sikukaguliwa matiti yangu. Sikudhani ingenitokea. Mimi ni mtaalamu wa kansa ya matiti," anasema Liz O'Riordan.

Mama huyo mtaalamu, anasema kwamba licha ya kupiga kampeni na kutoa elimu bora kwa miaka 20, bado aliangukia upande uleule, akikaguliwa na kukutwa ana kansa ya matiti.

Dk, O'Riordan, mwenye umri wa miaka 43 sasa, kabla ya kukaguliwa, alijiona kuwa na aina fulani ya uvimbe katika ziwa, ndipo akajihisi kuna jambo ambalo halijamlalia sawa.

Hapo ndipo kukafanya apatwe na hofu, huku akijiuliza itakuwaje katika taaluma ya kuwahudumia wenye kansa. Alihoji changamoto ya kushindwa kujua mwelekeo wake kiafya na wakati huohuo kuwatibu watu wenye shida hiyo.

Dk, O'Riordanm, anaeleza:"Ni namna gani nitashirikiana na mume wangu, pia wazazi? Ni kwa kiasi gani nitaacha kuwa dakktari wa kansa na kubaki mgonjwa?

"Nilifahamu namna ya kumwambia mtu una kansa ya titi. Sikujua, namna ya kunyanyua mdomo, kufuta chozi, kuacha kliniki, kwenda, kusubiri kumuona daktari, na kwenda katika maegesho ya gari kugugumia," anaeleza





Dk.Liz O'Riordan. **PICHA: MTANDAO.**

Daktari huyo anasema, baada ya kuwa na mjadala mrefu na mumewe, aliamua kutangaza kuugua kansa, kupitia mtandao wa kijamii.

Sasa mawazo yanamjia kwamba, pamoja na kuwa na kansa, anaamini atawasaidia wagonjwa wenzake wa kansa kwa namna tofauti, ingawaje anakiri ni jambo gumu

"Unapotoa taarifa kwa mara ya kwanza kuwa mtu ana kansa, ni habari ngumu sana katika maisha yao, lakini nilijipa moyo kwa kujiona mimi.

"Niliachwa na maumivu baada ya kukatwa titi, nilifahamu sana nao (familia) ninawachia maumivu niliyo nayo na sikupenda kulifanya hilo," anaeleza

Baada ya kuingia tena ofisini, anasema alikutana na mgonjwa wa kansa mwenye umri na aina ya kansa yake na vingi amefanana nacho.

Mwaka jana, Dk. O'Riordan's anasema alirejea matibabu ambayo ana shaka ataathirika mkono zaidi, huku akimsifu mwajiri wake kumpigania.

Msomi huyo mwenye shahada ya uzamivu, amefikia uamuzi wa kuacha kazi hiyo tangu mwaka 2017 na amegeukia upande wa pili, kuwa balozi na mwanaharakati anayezunguka sehemu mbalimbali.

"Bado nahangaishwa na uchovu na ninajaribu kurejesha akili yangu kufanya kazi yake sawa," anasem Dk. O'Riordan, mtaalamu mwandamizi ambaye kila mwaka anahudumia wagonjwa kati ya 70 na 100.

**• Makala hii ni kwa mujibu wa mtandao.**

MAZINGIRA

# Mamlaka miji zinapoteza maji, miradi kitaifa zajitahidi kuokoa



Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa (wakwanza kushoto), akitoa maelekezo kwenye chanzo cha Ikolongo, Wilaya ya Mpanda Vijijini, mkoani Katavi. **PICHA: MTANDAO.**



Mradi wa uboreshaji huduma za majisafi na usafi wa mazingira, mjini Lindi. **PICHA: BLOGU RWEYUNGA.**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KWA mrefu nchini huduma za maji safi na majitaka katika maeneo ya mijini na vijiji zimekuwa duni, kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo uwezo mdogo wa kifedha katika uendelezaji sekta ya maji.

Hali hiyo ilisababisha kabla na baada ya miaka ya 2000, hata katika baadhi ya maeneo katika miji mikuu ya mikoa na wilaya, huduma hiyo kuwa kama nyota ya jaha.

Kutokana na tatizo hilo kuwa kubwa kulingana na mahitaji makubwa ya maji kwa maisha ya kila siku ya binadamu, serikali ilianza kulivalisha njuga kuhakikisha huduma hiyo inazidi kuboreshwa.

> “uzalishaji wa maji ni wastani wa asilimia 67.9 tu ya mahitaji ya maji katika miji ya makao makuu ya mikoa.

Miongoni mwa mipango iliyowekwa, ni pamoja na kuongeza bajeti katika maendeleo ya sekta ya maji na kuanzishwa na kuimarishwa kwa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira, ili kuboredha huduma za maji.

Pamoja na mikakati hiyo, mwanzoni mwa miaka ya 2000 serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), kwa lengo la kuhakikisha huduma husika zinatolewa kwa ubora na viwango vya juu.

Licha ya juhudi hizo za serikali, hali ya utoaji wa huduma za maji ilikuwa bado kiwango cha chini katika baadhi ya maeneo, ikiwamo miji mikuu ya mikoa na wilaya ambayo mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira zilikuwapo.

Hivi karibuni Ewura ilizindua ripoti za utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini mwaka 2017/18, inayobeba tathmini ya utendaji wa mamlaka hizo.

**MKURUGENZI EWURA**

Kaimu Mkurugenzi wa Ewura, Nzinyagwa Mchany, anasema mamlaka zinazohudumia miji ya makao makuu ya wilaya na miji midogo 82, kati yake miji mikubwa iko 68 na mamlaka 14 za miji midogo.

Pia, kuna mamlaka 15 ambazo hazikufanyiwa kwa sababu hazikuwasilisha tathmini, katika mamlaka 13 hazikuwa na menejimenti na bodi ya wakurugenzi.

Kwa ujumla, utendaji wa mamlaka hizo unaelezwa kuimarika katika nyanja mbalimbali, kama vile kuongezeka kiwango cha maji kinachozalishwa, watu wanaopata maji, ubora wa maji na wateja wake, wateja wa mtandao wa majitaka, muda wa upatikanaji maji kwa siku, kuimarika uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja.

Mengine, ni kuongezeka makusanyo na ufanisi wa ukusanyaji maduhuli kulingana na vigezo vilivyowekwa na EWURA.

Vilevile, ripoti inaonyesha kwamba utendaji wa mamlaka zinazohudumia miji ya makao makuu ya wilaya na miji midogo, zimeimarika katika nyanja tofauti.

“Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 11.2. Hata hivyo, kiwango hicho cha maji kilichozalishwa ni asilimia 67.9 ya mahitaji ya maji ambayo ni mita za ujazo 452 milioni kwa mwaka wa fedha 2017/18.

”Wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji ni saa 18 kwa siku, wakati kiwango kinachotakiwa cha upatikanaji wa huduma ya maji ni saa 24 kwa siku,”anasema.

**UPOTEVU WA MAJI**

Mchany anasema, kiwango cha maji yanayopotea kimepungua katika miradi ya kitaifa kutoka asilimia 33.1 hadi kufikia aslimia 26.8, lakini katika sura ya pili, katika mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18.

Lakini, hali ni kinyume katika kipindi hicho cha mwaka wa fedha, katika mamlaka za miji maji yanapotea katika ongezeko la asilimia 40.5 katika mwaka wa fedha 2017/18 kutoka asilimia 38.4 mwaka wa fedha 2016/17.

Mkurugenzi wa Ewura anasema, uzalishaji wa maji ni wastani wa asilimia 67.9 tu ya mahitaji ya maji katika miji ya makao makuu ya mikoa.

Pia, anaendeleza asilimia 51.2 tu ya mahitaji ya maji katika miradi ya kitaifa hali inayoashiria pengo kubwa kati ya uzalishaji wa maji na mahitaji.

Aidha, mtandao wa usambazaji majisafi unakidhi asilimia 74 kwenye miji ya makao makuu ya mikoa na asilimia 55 kwa miradi ya kitaifa, ikionyesha kuwa sehemu kubwa za maeneo zinapaswa kuwa na mtandao wa usambazaji majisafi, hayana huduma hiyo itakayowezesha kuongeza idadi ya muunganiko wa wateja.

**PROF. MBARAWA**

Kuhusu suala la upotevu wa maji, Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa, anaitaka Ewura kuzilea na kusimamia mamlaka za maji zidhibiti upotevu wa maji uliopanda katika mamlaka za maji ya miji.

Prof. Mbarawa anaiagiza Ewura, kuzilea na kuzisimamia mamlaka hizo, zizalishe maji na kuhakikisha zinawafikia wananchi.

“Pia, fanyeni semina na kutoa elimu kwa wakurugenzi na wenyeviti wa mamlaka za maji namna ya uendeshaji wake, ili kujua namna ya kupunguza gharama za uendeshaji, zikiwemo za matumizi makubwa kununua dawa ya kutibu maji na za umeme,” anasema.

Anabainisha, pamoja na kuzalisha na kusambaza maji, mamlaka zinatakiwa kubaini gharama za maji hasa za vijijini kwamba ni kubwa kuliko mijini.

Sambamba na hilo, anazitaka kuweka viwango sawa vya kudhibiti ubora wa maji, pia kuwa na takwimu sahihi za huduma za maji kila wakati.

AFYA

UNAFAHAMU VISHIKWAMBI?

# Teknolojia inayotunza taarifa za mtoto, mahudhurio kliniki, chanjo

- Mfumo eletroniki mama 'aki – scan' vyote wazi
- Wazazi, wajawazito kukumbushwa kliniki zao

**Na Veronica Romwald,**

MIAKA ya nyuma, kabla ya maendeleo ya kiteknolojia, taarifa nyingi zilikusanywa kwa mfumo wa karatasi, hali ambao sasa imebadilika.

Teknolojia inarahisisha na kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi na halisi kwa wakati, pia inatumika kusaidia kutunga sera mbalimbali nchini.

Kwa kuzingatia umuhimu wa matumizi ya nyenzo za kiteknolojia katika ukusanyaji takwimu halisi na sahihi kwa wakati, sasa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Mpango wa Taifa wa Chanjo nchini, imeanza kukusanya taarifa za chanjo kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

Kuanzia sasa katika ngazi zote za vituo, vishikwambi au 'tablets, vitatumika kukusanya taarifa za chanjo. Hicho ni kifaa kinachorekodi na kuhifadhi taarifa hospitalini.

"Ni jambo ambalo tumelipigania muda mrefu tangu nilipoingia wizarani, ukiniuliza kipaumbele changu cha afya ni kipi, nitakujibu ni chanjo kwa watoto, ndiyo maana nakuwa mkali mno...pale tulipoanza kulikuwa na mikimiki unasikia chanjo huku hakuna, au kule zimeisha.

"Meneja Mpango wa Taifa wa Chanjo (Dk. Dafrosa Lyimo) alikuwa halali usingizi. Ni jambo ambalo linaniuma, unaweza kufikiri mama anajifungua leo, anaenda kumpa chanjo mtoto wake anaambiwa hakuna.

"Wakati tumechukua zaidi ya miaka 15 kuwaelimisha na kuwahamasisha wazazi kwamba chanjo ni muhimu kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa," anasema.

Anaongeza: "Ukiniambia jambo la kwanza kuchagua kati ya yote nitataja suala hili, kwa sababu upo utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) unaeleza licha ya kwamba chanjo huwakinga watoto dhidi ya magonjwa.

"Pia katika kila Dola (ya Marekani Sh. 2,330) moja inayowekezwa kwenye chanjo, inaweza kuokoa Dola 16 (Sh. 35,680) ambazo zingetumika kutibu magonjwa, katika muda ambao tungeutumia kwa ajili ya uzalishaji, shughuli za maendeleo," anabainisha waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu.

**MNYORORO BARIDI**


Mganga Mkuu wa Serikali (CMO), Profesa Mohamed Kambi, anasema katika ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2016/17, Tanzania ilikuwa nchi ya tatu barani Afrika kufikia asilimia 97 ya watoto waliopatiwa chanjo.

"Lengo letu ni kufikia asilimia 100 ya watoto wote wanaozaliwa na kuwapatia chanjo ifikapo 2020. Hii ni hatua muhimu ya kutufikisha huko. Tutahakikisha ule mnyororo wa baridi wa chanjo unakaa vizuri na tutahakikisha tunakusanya taarifa zote ili afua hizi ziende vizuri," anasema.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akipokea 'tablets' kutoka kwa Mkuu wa Masuala ya Afya UNICEF Kyaw Aung, hivi karibuni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Tulianza mchakato wa kutafuta vitendea kazi katika zahanati mpya zinazojengwa na mwaka huu, kwa kushirikiana na Shirika la Chanjo Duniani (GAVI) na UNICEF.**




**TAKWIMU KUHUSU CHANJO: VERONICA ROMWALD.**

**UNICEF**

Mkuu wa Miradi ya Afya wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Watoto (UNICEF), Kyaw Aung, anasema wataendelea kushirikiana kwa karibu na serikali kuhakikisha lengo linafikiwa.

"Tuna matumaini makubwa kwamba vifaa hivi tulivyokabidhi kwa Wizara vitaiwezesha kufikia lengo hilo la asilimia 100 ya watoto wote wanaozaliwa kupata chanjo," anasema.

Anafafanua kwamba, wamefanikiwa kuipatia serikali jumla ya majokofu 1,385 kwa ajili ya utunzaji chanjo katika vituo mbalimbali na vishikwambi 1,249 kwa ajili ya kukusanya taarifa za chanjo kwa njia ya mtandao.

Waziri Ummy anasema, kupatikana majokofu hayo kutasaidia kuongeza juhudi za usimamizi wa ubora wa chanjo hizo, kuhakikisha kunakuwapo mnyororo baridi unaohitajika.

"Ni jambo la muhimu mno, lazima kuwapo ule mnyororo baridi vinginevyo tunaweza kujikuta tunazo chanjo za kutosha lakini zisifae kwa matumizi kwa sababu ya kukosekana kwa mnyororo baridi katika uhifadhi," anaeleza.

"Tulianza mchakato wa kutafuta vitendea kazi katika zahanati mpya zinazojengwa na mwaka huu, kwa kushirikiana na Shirika la Chanjo Duniani (GAVI) na UNICEF.

"Majokofu haya yapo ya aina mbili; kuna 1,190 ambayo yanatumia nishati ya jua na 195 yanayotumia nishati ya umeme, majoko-

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Teknolojia inayotunza taarifa za mtoto, mahudhurio kliniki, chanjo

INATOKA UK.19

fu yote thamani yake ni Sh. bilioni 13.99 na gharama za vishikwambi ni Sh. bilioni 1.59, hii ni awamu ya kwanza," anafafanua.

**TAARIFA ZA KISASA**

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema taarifa zitakusanywa kupitia mfumo wa kielektroniki wa leja ya watoto (Tanzania Electronic Immunization Registry - TimR).

Anaeleza: "Tulianza mchakato wa kutafuta vitendea kazi katika zahanati mpya zinazojengwa na mwaka huu, kwa kushirikiana na Shirika la Gavi. Tumefanikiwa kununua jumla ya majokofu 1,385 kwa ajili ya utunzaji wa chanjo katika vituo mbalimbali.

"Tumenunua pia vishikwambi 1,249 kwa ajili ya kukusanya taarifa za chanjo kwa njia ya mtandao badala ya makaratasi, kuna majokofu ya aina mbili, yapo 1,190 yanayotumia nishati ya jua na 195 yanayotumia nishati ya umeme," anasema.

Anafafanua kuwa, majokofu hayo yana thamani ya Sh. bilioni 13.99 na gharama za vishikwambi hivyo ni Sh. bilioni 1.59 na kwamba hiyo ni awamu ya kwanza.

Anasema, wizara imefanikiwa kununua vitendea kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, wakiwamo mashirika ya Gavi na UNICEF.

"Tanzania tumechangia asilimia 20 ya fedha hizi. Dk. Dafrosa aliandaa andiko, likapitia michakato mbalimbali, tukapeleka Wizara ya Fedha na Mipango, kisha likapelekwa shirika la Gavi, tukaweza kupata hizi fedha," anabainisha.

Anasema, awamu ya pili kufikia Mei mwaka huu, kunatarajiwa kupokewa vishikwambi vingine 2001 vyenye thamani ya Sh. bilioni 2.6 na mwishoni mwa mwaka huu, yatapokewa majokofu kati ya 800 na 1,000 yenye thamani ya Sh. bilioni 11.5.

"Hivyo, tunategemea mpaka mwisho wa mwaka 2019, takribani asilimia 80 ya mahitaji ya majokofu tutakuwa tumetimiza kutosheleza tunahitaji majokofu yapatayo 2009," anasema.

**MFUMO ULIVYO**

Waziri Ummy anasema, taarifa zitakazokusanywa kupitia mfumo wa TimR zitatumwa wilayani na kukusanywa na mfumo (wa chanjo) ujulikanao kama 'Vaccine Information Management System - VIMS).

"Taarifa za chanjo katika VIMS zitatumwa katika mfumo wa taarifa za afya wa Wizara (DHIS2), hivyo hakuna haja ya watumishi kuingiza takwimu hizo mara mbili kama ilivyokuwa awali," anasema.

Pia, waziri anasema mfumo VIMS imeanza kutumika mikoani na wilayani na mfumo wa TimR kwa sasa unatumika katika mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Dodoma.

Anasema, wizara ilikusudia kusambaza mfumo huo wa TimR katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Mtwara, Geita, Njombe na Dar es Salaam mwezi uliopita na mikoa iliyobaki, mafunzo yataendelea mapema mwakani.



Mke wa Rais mstaafu, Mama Salma Kikwete, akimpatia chanjo ya mtoto Haula Mlondwa (umri miezi sita), kijijini cha Vigwaza, Kibaha, ikiwa ni wa Wiki ya Chanjo Kitaifa. **PICHA: MTANDAO.**

> "Hivyo, tunategemea mpaka mwisho wa mwaka 2019, takribani asilimia 80 ya mahitaji ya majokofu tutakuwa tumetimiza kutosheleza tunahitaji majokofu yapatayo 2009.

**KADI ZA KLINIKI**

Waziri anaongeza: "Mfumo huu utatusaidia kupata takwimu za chanjo za watoto kwa wakati, itamrahisishia kazi mtoa huduma.

"Kuanzia sasa, kadi zote za kliniki zitakuwa zimewekwa 'code' (namba) maalum ambayo mama atakuwa 'ana-scan' na taarifa yote ya mtoto itatokea, amezaliwa lini na anapaswa kupata chanjo gani.

"Hivyo, nawasisitiza waganga wakuu na mikoa na waratibu wa chanjo katika ngazi za mikoa na halmashauri, kuhakikisha watoa huduma wote wa chanjo wanafundishwa jinsi ya kufanya matengenezo madogo madogo ya majokofu haya na vifaa vingine, ili vidumu kwa muda mrefu kama ilivyokusudiwa," anasema.

Anasema mama atakuwa anapokea taarifa kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi, kumkumbusha kumpeleka mtoto kliniki kupata chanjo.

**WAJAWAZITO**

Waziri Ummy anasema, mfumo huo pia unakusudiwa baadaye kutumika kusajili wajawazito na kuwakumbusha wakati anaopaswa kurudi kliniki.

"Tutawaeleza baada ya miezi kadhaa ijayo, tunataka kuongeza kiwango cha wajawazito wanaohudhuria kliniki angalau mara nne, sasa hivi wanaohudhuria ni asilimia 51 tu wanahudhuria angalau mara nne, katika kipindi cha ujauzito," anasema.

Anaongeza: "Watakuwa wanahimizwa kwenda kliniki kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi.

**CHANJO YA HPV**

Rai ya waziri kwa wasichana wenye wenye umri wa miaka 14, waliopatiwa chanjo ya kwanza dhidi ya maradhi kirusi cha 'Human Papilloma' kinachosababisha saratani ya kizazi, waende kwenye kituo cha afya kwa ajili ya chanjo ya pili.

"Chanjo ya HPV ni salama, haina madhara imethibitishwa na Shirika la Afya Duniani, lakini wasichana waliochoma chanjo ya kwanza hawajarudi kupata chanjo ya pili kama inavyopaswa.

"Nawasihi wasichana wajitokeze ili kupata chanjo ya kuwakinga dhidi ya maambukizi ya saratani ya kizazi, chanjo hii inatolewa bila malipo, yoyote katika vituo vya serikali na binafsi.

"Dozi ya kwanza ya chanjo inatolewa wakati wowote msichana anapofikisha umri wa miaka 14 na dozi ya pili inapaswa kutolewa miezi sita baada ya dozi ya kwanza," anasema.

**CHANGAMOTO**

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk, Dafrosa Lyimo, anasema miongoni mwa sababu waliobaini kuchangia hali hiyo, ni kwamba wasichana wengi walichanjwa wakiwa shuleni darasa la saba.

"Kwa mara ya kwanza ilitolewa April, mwaka jana. Walipaswa kupata chanjo ya pili Desemba, mwaka jana, lakini kipindi hicho tayari walikuwa wameshamaliza darasa la saba," anasema.

Anasema kimsingi, chanjo ya kwanza huwa inaupatia mwili taarifa kwamba kuna kirusi cha HPV kimeingia ndani hivyo, ule mwili unaanza kujenga kinga.

"Tunaongeza ile chanjo ya pili, ili kuongeza ile akili ya mwili kwamba kirusi hicho kikiingia uendelee kupigana nacho, unapochukua muda mrefu ina maana yule askari aliyepaswa kupigana anaanza kusahau," anafafanua Dk. Dafrosa na kufafanua:.

"Hivyo tunawahimiza wazazi na walezi wawapeleke watoto wao kituo cha afya wakapate chanjo hii, kwa sababu wakitimiza dozi yote wanakuwa wamepata kinga kamili.



## Tanesco yatoa msamaha wa riba kwa wateja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limetoa msamaha wa riba kwa wateja wake wote ambao wanadaiwa na Shirika hilo badala yake kila mteja atatakiwa kulipa kiasi kamili anachodaiwa.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja Masoko wa Tanesco makao makuu, Mussa Chowo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Afya na Usalama mahali pa kazi ambayo kitaifa yanafanyika mkoani Mbeya.

Alisema Shirika hilo linawadai wateja wake Sh. bilioni 300, hivyo waliamua kuondoa riba ili warejeshe madeni yao kwa wakati na kiasi hicho kiweze kupatikana.

Chowo alisema msamaha huo wa riba umeanza rasmi jana (Mei Mosi).

"Shirika la Tanesco limeamua kutoa msamaha kwa wateja wake baada malimbikizo makubwa ya madeni yaliyopo na wadeni makubwa ni kutoka katika ofisi za serikali na wananchi, lengo letu ni kurejesha fedha tunazowadai ambazo ni Sh. bilioni 300 tunawasisitiza kulipa kwa wakati," alisema Chowo.

Aidha, Chowo alisema Shirika linaendelea kuwahamasisha wananchi kuendelea kutumia nishati ya umeme kwa ajili ya maendeleo ya jamii na taifa na kusisitiza kuendelea kupata elimu ya matumizi ya nishati hiyo.

Naye Ofisa Afya na Usalama wa Tanesco, Nelson Mnyanyi, alisema katika kuadhimisha Siku ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi, wamejipanga kutoa elimu ya mashuleni na taasisi nyingine katika kukabiliana na majanga yatokanayo na umeme.

Mnyanyi alisema mbali na kutoa elimu, pia ushauri kwa wazazi kuwa makini na watoto kutoshika au kuchezea nyaya za umeme katika maeneo yao.

# JPM awataka viongozi kupunguza malalamiko kwenye jamii

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

RAIS Dk. John Magufuli, amewataka viongozi wa Serikali wakiwamo mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya, wabunge na madiwani, kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua ili kupunguza malalamiko na manung'uniko kwenye jamii.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa anazungumza na wananchi katika Chuo cha Ualimu cha Mpunguso, wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, muda mfupi baada ya kuzindua majengo mapya ya chuo hicho yanayojengwa na serikali kwa zaidi ya Sh. bilioni tisa.

Aliamua kutoa maelekezo hayo baada ya kuona idadi kubwa ya wananchi wakiwa wamebeba mabango yenye malalamiko ya aina mbalimbali huku wakizuiwa na baadhi ya maofisa wasiyaonyeshe kwenye mikutano.

Alisema kitendo cha wananchi kubeba mabango hayo kwenye mikutano yake kinaonyesha kuwa kuna baadhi ya wasaidizi wake hawajatimiza majukumu yao ipasavyo na wananchi wameona wakimbilie kwake.

"Msiwazuie watu kuonyesha mabango yao hapa, wanataka kunionyesha mimi ili niwasaidie baada ya kushindwa kusaidiwa na wasaidizi wangu, nimeyasoma baadhi kuna watu wanagombea mipaka ya ardhi, wengine migogoro ya ndoa na wengine wanadai ya mirathi," alisema Magufuli na kuongeza:

"Mimi nataka ile migogoro ambayo imeshindikana kutatuliwa na ninyi wasaidizi wangu ndio inifikie mimi, sasa mnaanza kuwazuia wasinionyeshe mabango, wasikilizeni wananchi wanachotaka ili wasiniletee mabango," aliongeza.

Alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila na wakuu wa wilaya kupanga ratiba za kuwasikiliza wananchi kero zao katika maeneo yote aliyopita na kuona wananchi wakiwa wamebeba mabango. Kuhusu ujenzi wa Chuo cha Mpuguso, Rais Magufuli aliwaagiza mawaziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kusimamia ili ujenzi huo ukamilike haraka.

Aliwataka kuhakikisha ujenzi huo unakamilika vizuri na kwa thamani halisi ya Sh. bilioni tisa zilizotolewa na serikali kwa ajili ya miundombinu.

Vilevile aliiagiza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kuboresha barabara inayoanzia barabara kuu ya Tanzania - Malawi kwenda katika chuo hicho yenye urefu wa kilomita 2.6 kwa kiwango cha Changalawe na baadaye waanze kujenga kwa kiwango cha lami.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, alisema ujenzi unaofanyika chuoni hapo unahusisha kumbi za mihadhara, mabweni ya kulala wanafunzi na nyumba za watumishi.

Alisema ujenzi huo utasimamiwa vizuri na kwamba awali ujenzi huo ulikuwa unasuasua kufuatia mkandarasi wa awali kutofanya kazi haraka na kuamua kumtimua na kutafuta mwingine ambaye ndiye anaendelea mpaka sasa.

"Tunaishukuru serikali kwa kuamua kuboresha miundombinu ya chuo hiki kutokana na umuhimu wake, ni chuo kikubwa na kinazalisha walimu wengi sana, sisi tutahakikisha tunasimamia vizuri ili kiendane na hadhi yake," alisema Chalamila.

Mbunge wa Jimbo la Rungwe, Saul Amon, alisema wananchi wa Halmashauri ya Rungwe wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa vituo vya afya na maji.

Alisema halmashauri hiyo ina kata 29, lakini zenye vituo vya afya ni mbili pekee na kuomba waongezewe vituo ili kuwasogezea huduma wananchi hao.




Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Elisha Gaguti (wa tatu kulia), akikata utete kuzindua wa duka jipya la Tigo la kuhudumia wateja, mjini Bukoba jana. Wanaoshuhudia ni baadhi ya wafanyakazi wa Tigo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamuomba rais aende kuona shughuli wanazofanya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Ifupa katika Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ambao wamekuwa wakijitolea kuuza mali zao na kuchangishana fedha kila wiki kwa ajili ya kujenga Kituo cha afya, wamemuomba Rais Dk. John Magufuli kufika katika kijiji hicho na kujionea shughuli wanazofanya.

Wananchi hao walisema wanajua kuwa rais yuko mkoani Mbeya kwenye ziara ya zaidi ya siku nane hivyo wanaomba atembelee kijiji hicho ambacho kipo umbali wa zaidi ya kilomita 80 na kujionea kituo cha afya ambacho wamejenga kwa nguvu zao.

Walitoa ombi hilo juzi walipokuwa wanafanya harambee ya mwisho wa mwezi wa Aprili na kusema wamepambana kwa muda mrefu kujenga kituo hicho na sasa wanaomba msaada kutoka serikalini na kwa wadau mbalimbali.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Agostino Mwalela, alisema tangu wameanza kujenga kituo hicho wamekuwa wakichangishana kwa kuuza vitu mbalimbali ikiwamo mazao na mifugo.

Alisema awali walipata msaada wa Sh. milioni 25 kutoka kwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginand Mengi ambao uliwasaidia kukamilisha baadhi ya majengo na sasa wanaendelea kwa nguvu zao kujenga majengo mengine.

"Tunamshukuru sana mzee Mengi, alitusaidia sana, lakini kwa sasa tunamuomba rais wetu kwa sababu bado yupo Mbeya atutembelee na sisi ili ajionee kazi ambazo wananchi wake tunafanya," alisema Mwalela.

Alisema kwenye harambee wanazofanya hakuna mtu anayelazimishwa, lakini kutokana na wanavyopata shida ya matibabu kila mtu anaamua kujitoa kwa moyo ili kituo hicho kikamilike.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walieleza namna ambavyo wanapata shida ya matibabu na hivyo kulazimika kujitolea kujenga kituo hicho.

Mmoja wa wananchi hao, Rose Julius, alisema wanawake wa kijiji hicho kwa muda mrefu wamekuwa wakipata shida ya huduma za afya wanapotaka kujifungua hivyo kituo wanachojenga kitakuwa mkombozi.

Alisema wamekuwa wakilazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 80 kutoka kijijini hapo kwenda kupata matibabu jijini Mbeya hali ambayo alidai inahatarisha maisha ya wagonjwa hasa wajawazito.

"Tunaomba Serikali Kuu itusaidie maana kwa sasa tumepambana sana na kwa hatua tuliyofikia tunaona tunaelekea kwenye ukombozi wa kimatibabu," alisema Rose.

Naye Neoda Range, alisema wananchi wengi wa kijiji hicho wamekuwa wakijitolea zaidi kipindi cha mavuno ambacho kila mtu anakuwa na uwezo wa kujitolea.

Alisema hali inakuwa hivyo kwa sababu kijiji hicho ni cha wakulima ambao hutegemea kipindi cha mavuno ndio wapate vitu vya kuuza ili wapate hela za kuendelea na kituo hicho.

Chifu wa eneo hilo, Fred Jonas, aliwaomba wadau mbalimbali kuiga mfano wa Dk. Mengi kuwasaidia wananchi wanaojitolea kufanya shughuli za maendeleo.





# Wasiolipa 27,000/- za umeme kukiona

**Na Mwandishi wetu,** KONDOA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema hatasita kupiga mnada wa kuku kwa mtu atakayeshindwa kulipia Sh.27,000 ya kuunganishiwa umeme kwenye nyumba yake.

Aidha, amelitaka Shirika la Umeme nchini (Tanesco) kupokea fedha kidogo kidogo za wananchi wanaotaka kuunganishiwa umeme vijijini.

Kalemani alitoa kauli hiyo baada ya kufanya ziara ya kuwasha umeme katika Kijiji cha Mauno pamoja na kituo cha Afya cha Busi, wilayani Kondoa.

Alisema itakuwa si vyema mtu kuwa na kuku halafu akashindwa kuuza na kulipa kuunganishiwa umeme kwenye nyumba yake.

"Mimi nikirudi hapa nitakuja nikakuta kuna mtu hajaunganishiwa umeme kisa hajalipa 27,000 na nikajua ana mifugo na kuku, nitakamata hao kuku wake nitapiga mnada na ataunganishiwa umeme,"alisema.

Aidha, Waziri huyo aliwataka wakazi wa vijiji vya Mauno na Busi ambao maeneo yao hawajajenga kuweka mti unaofanana na nguzo ili wasogezewe huduma ya umeme kwa haraka.

"Kama bado hujajenga na unatarajia kujenga eneo lako weka hata mti unaofanana na nguzo ya umeme ili usogezewe huduma,"alisema.

Kadhalika, Dk. Kalemani alimwagiza Meneja wa Tanesco wilaya ya Kondoa na mkandarasi kuhakikisha wanamalizia kusambaza huduma ya umeme kwenye vijiji vyote vilivyosalia ndani ya wiki moja.

"Hakuna sababu ya kusuasua kuwasha umeme katika maeneo hayo kwa kuwa nguzo na nyaya wanazo za kutosha,"alisema.

Naye, Mbunge wa Kondoa Vijijini ambaye pia ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, aliwataka wananchi kuhakikisha wanaunga mkono juhudi za serikali za kuwapelekea huduma ya umeme kwa kutumia fursa hiyo kuingiza umeme katika nyumba zao.

Aliishukuru serikali ya awamu ya Tano kwa jitihada kubwa inazozifanya kupeleka maendeleo kwa wananchi na kujali wananchi wanyonge na wenye hali ya chini.

# Shirika lataka somo la ulinzi wa watoto

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KUTOKANA na kuwapo kwa matendo ya unyanyasaji na ukatili kwa watoto, Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Compassion International Tanzania, limeomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuweka somo la ulinzi wa mtoto kwenye mitaala ya elimu.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Shirika hilo, Agness Hotay, wakati akitoa salamu kwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya miaka 20 ya shirika hilo tangu lianze kuhidumia watoto wahitaji nchini Tanzania.

Alisema kuwa shirika hilo lilianzishwa kwa malengo ya kuwasaidia watoto wenye uhitaji wanaotoka katika familia ambazo hazina uwezo kwa lengo la kuwafanya watoto hao waweze kuishi maisha yenye furaha.

Kwenye salamu yake, Mkurugenzi huyo alisema kuwa shirika linawajibu wa kuhakikisha kuwa kila mtoto bila kujali jinsia, dini au kabila anauthibitisho kuwa anapendwa, analindwa na kujulikana.

Alisema uwakili wa shirika ni pamoja na kumtetea mtoto na kusimamia stahiki za mtoto husika ili kuhakikisha kuwa anafikia ndoto anazotarajia.

Alisema kuwa tangu kuanza kwa shirika hilo nchini na kutimiza miaka 20 sasa limeweza kufikia vijana 135,750 ambapo mpaka sasa vijana 99,671 bado wapo kwenye huduma na 36,133 wameisha maliza na kutoka kwenye mpango wa kuhudumiwa na Compassion Tanzania.

"Kupitia makanisa ambayo ni washirika wenza na Compassion International Tanzania yameweza kutoa ajira zaidi ya 1,300 hivyo kushiriki katika kuondoa uhaba wa ajira kwa kutengeneza ajira na kuongoza pato la taifa.

"Shirika limeweza kuwezesha makanisa kutengeneza miundombinu, kuhamasisha ujenzi wa madarasa, uchimbaji wa visima, ujenzi wa vyoo vya kisasa na jiko, uanzishwaji wa karakana za mafunzo mbalimbali, uanzishwaji wa VIKOBA na ujalisiriamali," alieleza Mkurugenzi.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi na Watu wenye Ulemavu, Stella Ikupa, aliwataka vijana kutumia fursa zilizopo kujipatia maendeleo.

Aliwasihi viongozi wa dini kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu ili jamii iweze kuwapa haki sawa na watu wengine.

"Naomba niwasisitize viongozi wa dini kutoa elimu ya uelewa kwa jamii ili wasiwachukulie watoto wenye ulemavu kama sehemu ya mkosi hata ifike hatua hata kwenye mahusiano mtu mwenye ulemavu asikose kuoa au kuolewa kwa kigezo cha kuwa na ulemavu," alisema Ikupa.

Aidha alisema kitendo cha shirika hilo kujitolea kuwahudumia watoto wenye uhitaji ni sehemu ya kulifanya taifa kuwa na watu ambao wamelelewa katika maadili mazuri na wenye kufanya kazi kwa uhadilifu.



Waziri wa Madini, Doto Biteko (katikati), akiongoza kikao cha kazi na viongozi waandamizi wa wizara hiyo, na Tume ya Madini, kilichofanyika Ihumwa, jijini Dodoma juzi. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo na (kulia kwake) ni Katibu Mkuu wizara hiyo, Prof. Simon Msanjila. **PICHA: WM**

# Waziri Mkuu Majaliwa aipa mtihani UCSAF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameuagiza uongozi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kuhakikisha asilimia sita ya vijiji ambavyo havijafikiwa na mawasiliano, vinapata huduma hiyo kabla ya mwaka 2020.

Pamoja na hayo, ameagiza mfuko huo kubainisha maeneo yenye changamoto za mawasiliano nchini ili serikali iweze kupeleka huduma hiyo kabla ya Desemba mwaka 2020.

Aidha, amewaonya Watanzania wanaotumia vibaya uwepo wa teknolojia kwa kukashfu watu au kusambaza video chafu na kwamba serikali haitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria. Majaliwa alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 10 tangu kuanzishwa kwa UCSAF ambayo yaliambatana na maonyesho mbalimbali na kuzindua minara katika baadhi ya vijiji ambavyo havikuwa na mawasiliano.

Aliutaka mfuko huo kuendelea kufuatilia kwa karibu sehemu zilizojengwa minara ya mawasiliano kwa kutumia ruzuku ya serikali ili kuhakikisha wananchi katika maeneo hayo wanaendelea kunufaika na upatikanaji wa huduma bora za mawasiliano. "Agizo la tatu kampuni zinazotoa huduma za mawasiliano ziendelee kushirikiana na UCSAF ili uweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa na la nne wananchi nchini waendelee kuwa walinzi wa miundombinu ya mawasiliano ikiwamo minara iliyojengwa kwenye maeneo yao ili waendeleee kunufaika na uwekezaji uliofanywa na serikali," alisema.

Majaliwa pia aliagiza wizara yenye dhamana ya mawasiliano na Tamisemi kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri utakaowezesha kampuni zote za simu nchini kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ikiwamo kushiriki shughuli za maendeleo na kulipa tozo mbalimbali kwa wakati.

Majaliwa pia aliwataka watendaji wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na wale wa Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuondoa vikwazo vyote vilivyozuia kampuni za simu kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Alizipongeza kampuni za simu hapa nchini za Vodacom, Airtel, Viatel, Tigo, TTCL, na Zantel kwa ushirikiano wa muda mrefu na serikali ambayo imesaidia mafanikio ya UCSAF.

Awali, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alisema kuwa mwaka wa fedha 2019/20, Serikali inatarajia kutangaza zabuni za ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano kwa ajili ya kata 250.

Alifafanua serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha kuwa vijiji vyote vinafikiwa na huduma ya mtandao wa mawasiliano ndani ya kipindi kilichopangwa.

Naye, Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Peter Ulanga, alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa Mfuko miaka 10 iliyopita, asilimia 94 ya nchi imeunganishwa na miundombinu ya mawasiliano, ambapo kata 703, vijiji 2,501 na watu milioni 5 nchini kote wamefikiwa na huduma hiyo.







Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kakola, Kata ya Bulyanhuru, katika Halmashauri ya Msalala, wilayani humo mkoani Shinyanga, wakati wa uzinduzi wa ulipaji kodi za majengo, uliofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Kakola A na B, juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# ZEC yawaita wapigakura uhakiki daftari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), imewataka wapigakura waliomo ndani ya daftari la kudumu la wapigakura kufanya maandalizi mapema kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao muda ukifika.

Kazi ya uhakiki itafanyika sambamba na kazi ya kuandikisha wapigakura wapya katika daftari hilo kwa mujibu wa ratiba itakayotolewa na tume.

Akizungumza katika semina ya wanafunzi wa shule za sekondari za Wilaya ya Magahrib "A" Unguja, Ofisa uchaguzi wa wilaya hiyo, Ali Rashid Suluhu, alisema wapigakura wote watapaswa kuhakiki taarifa zao za kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi ambacho kitawawezesha kuhakiki taarifa zao katika daftari la kudumu la wapigakura kwa kuwa bila kuhakiki taarifa huwezi kupiga kura kwa uchaguzi ujao.

Akizungumzia kuhusu uandikishaji wa wapiga kura wapya, ndugu Suluhu aliwata wazazi na walezi kuwahamasisha vijana ambao wamefikia umri wa miaka 18 ambao hawana vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi kufanya jitihada za makusudi kupata vitambulisho hivyo ili na wao waweze kuandikishwa kuwa wapigakura muda ukifika.

"Wapo vijana wengi wameshafikia umri wa miaka 18, lakini hawana vitambulisho vya Mzazibari mkaazi, hivyo bila ya kuwa na kitambulisho hicho watakosa haki yao ya kupiga kura,"alisema.

Naye Msaidizi Ofisa uchaguzi Wilaya ya Kaskazini "A", Miza Pandu Ali, alisema, ZEC itaweka wazi majina ya wapigakura katika vituo vyote vya kujiandikisha baada ya kumaliza kazi ya uandikishaji wa wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za wapigakura waliomo katika daftari. Alieleza lengo la kuweka wazi majina ya wapigakura ni kuwapa fursa kujiridhisha kuhusu usahihi wa taarifa zao na kuweka pingamizi kwa wapigakura ambao hawana sifa za kuandikishwa katika eneo husika.

Alisema kwamba wakati wa uandikishaji tume haitofanya shughuli za uendelezaji wa daftari kwa wapigakura wanaoomba kubadilisha na kusahihisha taarifa zao pamoja na wapigakura waliopoteza shahada zao na badala yake shuhuli hizo zitafanyika katika ofisi za uchaguzi za wilaya mara baada ya kukamilika kwa kazi ya uandikishaji na uhakiki wa taarifa

Wanafunzi wa shule hiyo waliiomba ZEC kuendelea kutoa elimu ya wapigakura ili kila mwananchi aweze kutumia haki yake ya kupiga kura muda ukifika

# Utafiti watakiwa kubaini watoto mahitaji maalum

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amewataka maafisa wa elimu jumuisho na Stadi za maisha kufanya utafiti ili kujua hali halisi ya watoto wenye mahitaji maalumu.

Akizungumza na watendaji wa idara hiyo Mjini Unguja, alisema unakuwapo utafiti kutawasaidia kujua mahitaji ya watu hao ili na kupata urahisi katika kutoa mahitaji yao ikiwamo kupata elimu bora.

Naibu waziri huyo aliwataka watendaji hao kuweka mpango kazi maalum ambao utawasaidia endapo atatokea mfadhili wa kutaka kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum kupata kwa urahisi katika kutoa misada yao.

Aidha, aliwataka wafanyakazi wa idara hiyo kuwa na ushirikiano ambao utasaidia kuwashughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalum ili nao waweze kutimiza ndoto zao.

Hata hivyo, Simai aliwaahidi watendaji hao kuyashuhulikia matatizo yao yote yanayowakabili hatua kwa hatua ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji wa kazi.

Watendaji wa idara hiyo wameiomba Wizara ya Elimu kuhakikisha inatengeneza sera ya elimu mjumuisho ambayo itawashirikisha na wanafunzi wenye mahitaji maalum ili nao waweze kujifunza.

Mkurugenzi wa idara hiyo, Mpaji Suleiman, alisema ipo haja ya kuwapa mafunzo walimu katika shule mbalimbali ili waweze kuwasaidia wanafunzi wasioona na viziwi ambayo itawasaidia nao kupata haki yao ya msingi ya elimu.

Maafisa wa idara hiyo waliwaomba wadau wa elimu kutoa michango yao kwa kuboresha huduma ya elimu kwa watu wenye mahitaji maalum kwa kuwa wanakabiliwa na matatizo mengi katika kuwasaidia watu hao.

# CCM yatoa msimamo Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi, amesema CCM inaamini Muungano wa Serikali mbili ya Zanzibar na Tanganyika ndio chimbuko la Maendeleo yaliyofikiwa katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Alisema siri ya kudumu kwa muungano huo hadi kufikia miaka 55 ni kutokana na kujikita katika undugu wa damu badala ya maslahi binafsi ya kila nchi, hali iliyopelekea kuwepo kwa kuaminiana, kushauriana na kuheshimiana katika kutatua changamoto za Muungano huo.

Akizungumza visiwani Zanzibar kuhusu miaka 55 ya muungano na utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020, alisema huwezi kuutaja Muungano huo bila kueleza Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 pamoja na uhuru wa Tanganyika wa mwaka 1961, ambavyo ndio chachu ya ukombozi, utu na ustawi wa kijamii kwa wananchi wa pande zote za Muungano.

Alisema waasisi wa Muungano huo ambao ni Marehemu Mzee Abeid Aman Karume na Hayati Mwalimu Julius Nyerere, waliamua kuunda mfumo huo kwa kutafakari kwa kina maendeleo na fursa za kijamii za wananchi waliowaongoza kwa wakati huo.

Alieleza kwamba haikuwa kazi rahisi nchi ndogo ya Zanzibar kukubali iungane na nchi kubwa ya Tanganyika lakini kupitia mashauriano ya vikao vya Wazee na ridhaa ya wananchi wenyewe yalizaa matunda ya kufikia mwafaka wa kuingia katika mfumo huo ili kushirikiana katika masuala ya kiuchumi, kisiasa, kimaendeleo na kijamii.

Alisema Muungano huo ulikuwa na changamoto zaidi ya 15 zilizotatuliwa hatua kwa hatua ambapo hivi sasa zimebaki nne na 11 tayari zimetafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Aliwapongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kwa kusimamia ipasavyo utatuzi wa changamoto hizo za Muungano hatua iliyoendelea kuleta ufanisi katika masuala ya kiuchumi.

Alisema changamoto nne zilizobaki nazo zikitafutiwa ufumbuzi zitaibuka zingine kutokana na asili ya maisha ya binadamu kwani kila siku watu wanazaliwa na mahitaji yanaongezeka kutokana na mahitaji ya wakati husika.

"Katika utawala wa Dk. Shein na Dk. Magufuli changamoto hizi zimetatuliwa kwa kasi kubwa sana na zilizobaki zitatuliwa wakati wowote kwa njia ya vikao vya pande zote mbili," alisema.

Alieleza kuwa wananchi waendelee kuamini kwamba Serikali zao zipo makini katika kusimamia maslahi yao na masuala mbali mbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa chini ya Muungano huo.

Alisema kuna baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu katika Sekta za umma wamekuwa wakichafua hadhi ya Muungano kutokana na vitendo vyao vya rushwa na urasimu usiokuwa na sababu za msingi katika utoaji wa huduma.

Alizitaja sababu za kuwapo kwa muungano ni ulinzi na usalama wa nchi zote mbili pamoja na kutoa uhuru kwa wananchi wa pande zote mbili kuishi sehemu yoyote ya Muungano bila kusumbuliwa.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 15 April**

Tues 30 April

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | The Decor rpt |
| 12:30 | Mizengwe rpt |
| 12:45 | Aibu Yako |
| 13:00 | Series rpt: Life is a teacher |
| 13:45 | Series rpt: Iljimae |
| 14:15 | Local pgm rpt: Business Edition |
| 15:00 | Bundesliga kick off |
| 15:30 | Out and About rpt |
| 16:00 | Capchat rpt |
| 17:00 | Usafiri wako rpt |
| 17:30 | Meza huru |
| 19:00 | Innovation |
| 19:30 | Jagina |
| 19:30 | Ripoti Maalum |
| 20:00 | Series: Life is a teacher |
| 20:45 | Series: Iljimae |
| 21:30 | Capital Prime |
| 22:00 | Turning the Spotlight rpt |
| 22:30 | Iron Chef rpt |
| 23:30 | Al Jazeera |

**Wed 01 May**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Movie: Decoys |
| 10:30 | Movie: Street Kings |
| 12:00 | Turning the Spotlight rpt |
| 12:30 | Culinary delight rpt |
| 13:00 | Series rpt: Life is a teacher |
| 13:45 | Series rpt: Iljimae |
| 14:30 | Local Pgm: The Monday Agenda Rpt |
| 15:15 | Capchat rpt |
| 16:15 | CNN International |
| 17:00 | Innovation rpt |
| 17:30 | Movie: Pterodacyl |
| 19:00 | Sports Gazette |
| 19:30 | Chetu ni chetu |
| 20:00 | Series: Life is a teacher |
| 20:45 | Series: Iljimae |
| 21:30 | Capital Prime News |
| 22:00 | Dakika 45: |
| 22:45 | The Décor |
| 23:15 | Al Jazeera |

**Thurs 02 May**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | Sports Gazette |
| 12:30 | Out n' about rpt: |
| 13:00 | Series rpt: Life is a teacher |
| 13:45 | Series rpt: Iljimae |
| 14:30 | Business Edition rpt |
| 15:00 | Korean Drama rpt: Emperor of the sea |
| 16:00 | Dakika 45 rpt |
| 17:00 | In good shape |
| 17:30 | Meza Huru |
| 19:00 | Turning the spotlight |
| 19;30 | Tanzania yetu |
| 20:00 | Series: Life is a teacher |
| 20:45 | Series: Iljimae |
| 21:30 | Capital Prime News |
| 22:00 | Capchat rpt |
| 23:00 | Al Jazeera |

**Frid 03 May**

| | |
|---|---|
| 06:00 | Al Jazeera |
| 08:00 | CNN International News |
| 09:00 | Al Jazeera |
| 10:00 | Kumekucha |
| 10:30 | Kumekucha Michezo |
| 11:30 | Kumekucha Kishindo |
| 12:00 | Innovation rpt |
| 12:30 | The Decor rpt |
| 13:00 | Series rpt: Life is a teacher |
| 13:45 | Series rpt: Iljimae |
| 14:30 | Chetu ni chetu rpt |
| 15:00 | Korean Dram rpt: Emperor of the sea |
| 16:00 | CNN International |
| 16:30 | The Monday Agenda rpt |
| 17:30 | Meza Huru |
| 19:00 | Drive it |
| 19:30 | Eco@Africa |
| 20:00 | Aibu yako |
| 20:15 | Local Pgm: Business Edition |
| 20:45 | Series: Iljimae |
| 21:30 | Capital Prime News |
| 22:00 | Malumbano ya hoja rpt |
| 00:00 | Al Jazeera |

**Sat 04 May**

| | |
|---|---|
| 08:00 | CNN International |
| 09:00 | Drive It rpt |
| 09:30 | Turning the Spotlight rpt |
| 10:00 | Culinary delight rpt |
| 10:30 | Innovation rpt |
| 11:00 | Out n'about rpt |
| 11:30 | Sports Gazette rpt |
| 12:00 | Usafiri wako rpt |
| 12:30 | Eco@Africa rpt |
| 13:00 | Business edition rpt |
| 13:30 | Korean Drama rpt: Emperor of the sea |
| 14:30 | Telenovela rpt: Iljimae |
| 17:15 | Tanzania Yetu rpt |
| 17:45 | Bundesliga kick off |
| 18:15 | Capchat rpt |
| 19:15 | Mizengwe |
| 19:30 | The Decor |
| 20:00 | Iron Chef. |
| 21:00 | Out n' About |
| 21:30 | Movie: The Cradle |
| 23:00 | Grapes of Justice rpt |
| 01:00 | Al Jazeera |

**Sun 05 May**

| | |
|---|---|
| 08:00 | CNN International |
| 09:00 | In good shape |
| 10:00 | Capchat rpt |
| 11:00 | Sports Gazette rpt |
| 11:30 | Iron chef rpt |
| 12:00 | Jagina rpt |
| 12:30 | Bundesligga Kick Off rpt |
| 13:00 | Shamba lulu |
| 13:30 | Series rpt: Life is a teacher |
| 15:15 | Aibu yako |
| 15:30 | Drive it rpt |
| 16:00 | Dakika 45 rpt |
| 16:45 | Mizengwe rpt |
| 17:00 | The Decor rpt |
| 17:30 | Meza huru |
| 19:00 | Turning the Spotlight rpt |
| 19:30 | Cookery pgm: Culinary Delights |
| 20:00 | Korean Drama rpt: Emperor of the sea |
| 21:00 | Shift |
| 21:15 | Capchat live |
| 22:15 | Series rpt: Iljimae |
| 00:00 | Al Jazeera |

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 29 April**

| | |
|---|---|
| 5:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 6:00 | Habari |
| 6:40 | Kumekucha |
| 7:30 | HABARI |
| 8:00 | Kumekucha Michezo |
| 8:55 | Habari za saa |
| 9:00 | Kumekucha Kishindo |
| 9:30 | Isidingo |
| 9:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Igizo: Elininyo |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Kimya Milele |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Jungu kuu rpt |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Mjue Zaidi |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza Huru |
| 16:30 | Watoto Wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:10 | Aibu yako rpt |
| 18:15 | Mapishi rpt |
| 18:30 | Kesho Leo |
| 19:00 | Afya ya Jamii |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:05 | Dakika 45 |
| 22:00 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | Al Jazeera |
| 02:00 | CNN International |

**TUESDAY 30 April**

| | |
|---|---|
| 5:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 6:00 | Habari |
| 6:40 | Kumekucha |
| 7:30 | HABARI |
| 8:00 | Kumekucha Michezo |
| 8:55 | Habari za saa |
| 9:00 | Kumekucha Kishindo |
| 9:30 | Isidingo |
| 9:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Hawavumi lakiniwamo |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Hawavumi lakini wamo |
| 11:15 | Igizo: Mtego |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Afya ya jamii rpt |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Uchumi na biashara |
| 13:30 | Kipindi Maalum rpt : TFDA |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Mizengwe rpt |
| 14:15 | Telenovela: Destiny (Destino) rpt: |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza Huru |
| 16:30 | Watoto wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | The great queen Seonduk |
| 19:00 | Jarida la wanawake |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Tanzania yetu |
| 21:30 | Kipindi Maalum: Chetu ni chetu |
| 22:00 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | CNN International |

**WEDNESDAY 01 May**

| | |
|---|---|
| 5:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 6:00 | HABARI |
| 6:40 | Kumekucha |
| 7:30 | HABARI |
| 8:00 | Kumekucha Michezo |
| 9:00 | Kumekucha Kishindo |
| 9:30 | Isidingo |
| 9:55 | Movie:Cut off prt 1& 2 |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Jarida wanawake rpt |
| 13:00 | Dakika 45 |
| 14:00 | Telenovela rpt: Destiny (Destino): |
| 15:00 | Movie: DNA |
| 16:30 | Watoto Wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Mapishi rpt |
| 18:30 | Ijue Sheria |
| 19:00 | Kipindi Maalum: TFDA |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Aibu Yako! Hata wewe? |
| 21:10 | Kipindi Maalum : Tanesco |
| 21:40 | Kesho leo rpt |
| 22:00 | Kipindi Maalum: Tatu mzuka |
| 22:10 | Telenovela: Destiny (Destino) |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | Al Jazeera |
| 2:00 | CNN International |

**THURSDAY 02 May**

| | |
|---|---|
| 5:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 6:00 | HABARI |
| 6:40 | Kumekucha |
| 7:30 | HABARI |
| 8:00 | Kumekucha Michezo |
| 8:55 | Habari za saa |
| 9:00 | Kumekucha Kishindo |
| 9:30 | Isidingo |
| 9:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Igizo: Riziki |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Igizo: Elininyo |
| 11:15 | Kesho leo rpt |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al jazeera |
| 12:30 | Ijue Sheria |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Sanaa na wasanii |
| 13:30 | Tanzania yetu |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Telenovela rpt: Destiny (Destino) |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza Huru |
| 16:30 | Watoto Wetu |
| 17:00 | The Base |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Mapishi |
| 18:30 | Jagina |
| 19:00 | Usafiri wako |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Malumbano ya hoja |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | CNN International |

**FRIDAY 03 May**

| | |
|---|---|
| 5:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 6:00 | HABARI |
| 6:40 | Kumekucha |
| 7:30 | HABARI |
| 8:00 | Kumekucha Michezo |
| 8:55 | Habari za saa |
| 9:00 | Kumekucha Kishindo |
| 9:30 | Isidingo |
| 9:55 | Habari za saa |
| 10:00 | Watoto wetu |
| 10:30 | Hawavumi lakini wamo |
| 10:55 | Habari za saa |
| 11:00 | Hawavumi lakini wamo |
| 11:30 | Usafiri wako |
| 11:55 | Habari za saa |
| 12:00 | Al Jazeera |
| 12:30 | Kipindi Maalum rpt: Tanesco |
| 12:55 | Habari za saa |
| 13:00 | Jagina rpt |
| 13:30 | Chetu ni chetu rpt |
| 13:55 | Habari za saa |
| 14:00 | Telenovela rpt: Destiny (Destino) |
| 14:55 | Habari za saa |
| 15:00 | Meza huru |
| 16:30 | Watoto wetu |
| 17:00 | The Base |
| 17:30 | Ibada ya kiislamu |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Igizo: Mizengwe |
| 18:30 | Shamba lulu |
| 19:00 | Uchumi na biashara |
| 19:30 | Isidingo |
| 20:00 | Habari |
| 21:05 | Kipima joto |
| 23:00 | Habari |
| 23:30 | The Base |
| 00:30 | CNN International |

**SATURDAY 04 May**

| | |
|---|---|
| 5:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 6:00 | HABARI |
| 6:40 | Kumekucha |
| 7:00 | Habari |
| 8:00 | Al Jazeera |
| 9:00 | Watoto wetu |
| 10:00 | Mjue Zaidi rpt |
| 11:00 | Chetu ni chetu rpt |
| 11:30 | Usafiri wako |
| 12:00 | Shamba lulu |
| 12:30 | Telenovela rpt: Destiny (Destino) |
| 14:45 | Igizo rpt: Riziki |
| 15:15 | Igizo rpt: Elininyo |
| 15:45 | Igizo rpt: Mizengwe |
| 16:00 | Igizo rpt: Kimya Milele |
| 16:30 | Igizo: Mtego rpt |
| 17:00 | Shamsham za Pwani |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Mapishi |
| 18:30 | Igizo: Elininyo |
| 19:00 | Sanaa na wasanii |
| 19:30 | Jungu Kuu |
| 20:00 | Habari |
| 21:00 | Igizo: Kimya Milele |
| 21:30 | Hawavumi lakini wamo |
| 22:30 | Isidingo rpt |
| 01:00 | CNN International |

**SUNDAY 05 May**

| | |
|---|---|
| 5:30 | Uwanja wa Mazoezi |
| 6:00 | HABARI |
| 6:40 | Kumekucha |
| 7:00 | Habari |
| 8:00 | Al jazeera |
| 09:00 | Watoto Wetu |
| 10:00 | Isidingo |
| 11:45 | Aibu Yako |
| 11:50 | Hawavumi lakini wamo rpt |
| 12:50 | Bongo Movie rpt: It wasn't me 2 |
| 14:00 | Tamasha la Michezo |
| 15:00 | Mwangaza |
| 16:00 | Korean drama: The great queen Seonduk |
| 16:45 | Mjue zaidi |
| 17:30 | Kipindi cha kikristo |
| 18:00 | Jiji Letu |
| 18:15 | Mapishi |
| 18:30 | Mizengwe rpt |
| 18:45 | Matukio ya wiki |
| 19:30 | Igizo: Mtego |
| 20:00 | Habari |
| 21:05 | Mizengwe |
| 21:00 | Bongo Movie: |
| 22:00 | Telenovela rpt: Des- |


5 EATV

eNewz

LEO JIONI SAA 12:00



ALHAMISI

11:00 DADAZ (live)
12:00 Mpya
15:00 FUNGUKA
16:00 Bongo Hits
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Bongo Hits

eNewz Kupata fununu, udaku na habari zote za mjini kuhusu wasanii na maisha yao, ulimwengu wa wasanaa, burudani na pia matukio yaliotokea siku kama hiyo kwenye historia ya sanaa.

eastafrica RADIO

05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

HABARI KIMATAIFA

# Ebola yaua 27 kwa siku moja DRC

**KINSHASA,** Congo

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imesema watu 27 wamefariki kutokana na maambukizi ya ugonjwa wa Ebola katika Jimbo la Kivu Kaskazini.

Imesema idadi hiyo ni kubwa kuwahi kutokea kuliko zote katika siku moja, na kufanya idadi ya vifo vya maambukizi ndani ya kipindi cha wiki moja kufikia 126.

Kabla ya vifo vya watu hao 27, idadi ya maambukizi ilikuwa watu 110, wiki chache zilizopita na wizara ya afya ilieleza kuwa mlipuko wa wiki iliyopita mashariki mwa nchi, katika mikoa ya kivu na Ituri, unasambaa kwa kasi kutokana na mashambulizi ya makundi ya waasi yanayotatiza juhudi za madaktari na msaada wa jumuiya ya kimataifa.

Msimamizi wa juhudi za kukabiliana na Ebola mjini Butembo, Dk. Jean Christopher Shako, alisema japo maafisa wake wamejitolea kuangamiza ugonjwa huo, msaada wa jamii wanaotumikia ni mdogo na wengi hawaamini kwamba kuna Ebola. Anasema kwamba wanafanya kazi kwa matumaini.

"Tunapambana na ugonjwa huo kwa uwezo wetu wote. Tuna matumaini kwamba utamalizika. Sote tuwe na imani kwa Mungu, tumwombe Mungu tushinde ugonjwa huu", alisema Dk.Shako

Vituo vitano vya kutibu wagonjwa wa Ebola vimeshambuliwa katika muda wa miezi miwili iliyopita, huku afisa wa ngazi ya juu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) akiuawa kwa kupigwa risasi na watu wenye silaha siku 10 zilizopita.

Waliofanya mauaji hayo wanadaiwa kujulikana lakini wanaripotiwa kupewa kinga na makundi ya wapiganaji na watu kutoka katika jamii, wanaopinga juhudi zinazochukuliwa kukabiliana na ugonjwa huo.

"Huyo daktari aliuawa na watu gani, wakati kikao alichokuwa anahudhuria kilikuwa kinajulikana na serikali? Vyombo vya usalama vilijua kwamba kikao hicho kilikuwa kinafanyika. Walikuwa wapi? Watu wanajiuliza maswali mengi wakitaka kujua waliomua daktari huyo," alisema Issa Misango mkazi wa Butembo na kuongeza

"Kama ni wapiganaji wa mai mai au ni wale wale walinzi wa jeshi. Watuambie. Inakuaje walijua hadi mahali alikuwa amekaa wakati wa mkutano, wakaingia moja kwa moja na kumuua?".

Alisema idadi kubwa ya watu katika maeneo yenye Ebola, wana imani kwamba Ebola ni fikra tu iliyoanzishwa na kuenezwa na serikali pamoja na jumuiya ya kimataifa.

Mlipuko wa sasa wa virusi vya Ebola, unasababisha mgonjwa kutapika, kuhara na kutokwa damu, ndio wa pili kwa ukubwa baada ya wa mwaka 2013 na 2016 uliotokea Afrika magharibi na kuuwa watu 11,000. **VOA**

# Shirika la Ndege Kenya latangaza kupata hasara

**NAIROBI,** Kenya

SHIRIKA la Ndege Kenya (Kenya Airways) limetangaza kupata hasara ya Dola za Marekani milioni 75 kwa mwaka wa fedha uliopita.

Hasara hiyo ni sawa na shilingi za Kenya bilioni 7.59 ambazo zilirekodiwa katika kipindi cha miezi 12 hadi mwishoni mwa mwaka 2018.

Hata hivyo, kiwango hicho cha hasara ni kidogo kuliko hasara ya mwaka jana ambayo ilikuwa ni Sh. bilioni 9.44 katika kipindi cha mwaka 2017. Taarifa hiyo ilichapishwa katika ukurasa wa jarida maarufu la maswala ya uchumi na fedha:

Kampuni hiyo inasema kuwa hasara hiyo imetokana na ongezeko kubwa ya bei ya mafuta, mishahara ya juu, na viwango vya juu vya gharama za usafiri wa ndege vilivyowekwa na mmiliki.

Hata hivyo, kulikuwa na ongezeko la mapato ya kiasi cha Sh. bilioni 114.45 ikilinganishwa na mwaka jana ambapo yalikuwa ni Sh. bilioni 106.2. Pia mapato hayo ni chini ya mapato yao ya Sh.116 bilioni waliyopatikana mwaka 2016.

**Mipango mibovu ya safari na ushirikiano inayoweza kusababisha hasara kubwa ya mapato hususani kutokana na kutoongezwa kwa safari katika nchi za Afrika.**

Shirika hilo la ndege la kimataifa limekuwa likitumia suala la hasara linayoipata kujaribu kuchukua utawala wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Jomo Kenyatta, lakini Wakenya wengi wamekuwa wakielezea kutokukubaliana na hoja hiyo.

Kulingana na ripoti ya tume ya seneti iliyochukua jukumu la kuelewa mzozo wa hasara katika shirika hilo mwaka 2015, iliyoongozwa na Seneta Anyang' Nyong'o ilitaja sababu tano za kupata hasara.


Lakini wachambuzi wa masuala ya uchumi wanasema hakuna aliyejali kuzitafutia suluhu.

Sababu tano zilizotajwa za hasara katika Shirika la Ndege Kenya ni: Maamuzi mabaya ya uwekezaji katika ununuzi na uuzaji wa ndege, makubaliano ya ununuzi wa mafuta yanayosababishia hasara kampuni na hivyo kuisababishia kampuni kuwa na madeni makubwa.

Pili, uuzaji wa tiketi za bei ya juu zisizo na ushindani kwenye soko, jambo linalosababisha kuwapoteza wateja na mapato.

Tatu, Mipango mibovu ya safari na ushirikiano inayoweza kusababisha hasara kubwa ya mapato hususani kutokana na kutoongezwa kwa safari katika nchi za Afrika.

Nne, Matatizo ya sera ya wafanyakazi inayosababisha mizozo ya wafanyakazi Tano, Kufutwa mara kwa mara kwa safari, hivyo uhusiano mbaya na baadhi ya Wakenya wamekuwa wakielezea hisia zao juu ya hasara inayoendela kulikumba shirika la ndege la taifa lao kenya Airways. **BBC**



Kiongozi wa juu wa kundi la Dola la Kiislamu (IS), Abu Bakr al-Baghdadi, ambaye ameonekana kwenye mkanda wa video kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2014. **PICHA: ALLIANCE**

# Sudan kufanya tena maandamano

**KHARTOUM,** Sudan

WAANDAMANAJI Sudan wametoa wito wa kufanyika maandamano makubwa wakisisitiza kuwa jeshi halina nia thabiti ya kukabidhi madaraka kwa raia.

Wamesema ni muda wa wiki tatu umepita tangu Omar al Bashir aondoke madarakani. Wito huo unakuja wakati hali ya wasiwasi ikiongezeka kuhusiana na muundo wa baraza jipya la pamoja kati ya raia na jeshi.

Kuhusu muundo wa baraza jipya la pamoja kati ya raia

Na jeshi litakaloiongoza nchi ya Sudan, pande hizo mbili bado zinakinzana kuhusiana na wawakilishi katika baraza hilo jipya ambalo linatarajiwa kuchukua nafasi ya baraza la kijeshi.

Jeshi limekuwa likitaka baraza lenye wajumbe10 ikiwa nipamoja na wawakilishi saba wa jeshi na raia watatu.

Kutokukubaliana huko kumesababisha muungano kwa ajili ya uhuru na mabadiliko kutangaza maandamano ya watu milioni moja leo, huku wakisisitiza kutaka utawala wa kiraia.

"Baraza la kijeshi halina nia thabiti juu ya kukabidhi madaraka kwa utawala wa raia," alisema Mohamed Naji al-Assam ambaye ni kiongozi wa chama cha wanataaluma wa Sudan (SPA) kilichoongoza maandamano.

Alisema baraza la kijeshi linasisitiza kwamba baraza la pamoja linapaswa kuongozwa na wanajeshi likiwa wana wawakilishi wa kiraia.

Alisema kuwa jeshi limekuwa likitaka kupanua madaraka yake kila siku na jumuiya ya kimataifa inapaswa kuunga mkono uchaguzi wa watu wa Sudan.

Aliongeza kuwa wananchi wanahisi kutokana na vitendo vyote vya baraza la kijeshi la mpito hadi wakati huu kwamba halina nia ya dhati kuhamisha madaraka kwa raia.

"Sasa tunaona muda umepita wakati madaraka ya baraza la kijeshi yanaongezeka na hii ni hatari kwa mapinduzi ya Sudan," alisema Mohamed Naji al-Assam.

Akizungumza na waandishi habari, Madani Abbas Madani ambaye ni kiongozi mwingine wa maandamano amelishutumu baraza la kijeshi kwa kutumia lugha ya kuongeza mivutano ambayo haishawishi ushirikiano. **DW**

# ‘Mazungumzo kuchagiza ushirikiano serikali, tasnia habari’

**Na Mashaka Mgeta,** DODOMA

USHIRIKIANO na mazungumzo vimetajwa kuwa miongoni mwa nyenzo muhimu zitakazofanikisha kuondoa tofauti zilizopo kati ya waandishi wa habari na serikali na hivyo kuwawezesha watu kupata taarifa sahihi.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa kamati ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari, Neville Meena, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana.

Maadhimisho ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari yatafanyika leo na kesho, jijini hapa, yakiwa na kaulimbiu: “Vyombo vya habari kwa demokrasia; Tasnia ya habari na uchaguzi katika nyakati za upotoshaji wa taarifa.”

Meena ambaye pia ni Katibu wa Jukwaa la Wahariri (TEF) alisema kumekuwapo nafasi finyu ya uhusiano mwema na mazungumzo yanayohusu changamoto zinazoikabili tasnia na waandishi wa habari, hivyo ni wakati sasa kwa pande mbili hizo kukutana kwa vile wote wanaitumikia jamii moja.

Meena alitoa mfano wa namna serikali ilivyoshirikiana na wadau wa tasnia ya habari katika hatua mbalimbali za maandalizi ya maadhimisho hayo na kwa wakati wote wamekuwa wakizungumza lugha moja.

“Sisi wadau wa tasnia ya habari tumepata ushirikiano mkubwa kutoka serikalini kupitia Idara ya Habari (Maelezo), tunaamini kwamba ushirikiano na mazungumzo ya pamoja yanapofanyika, ni wazi kwamba tutapata suluhu ya changamoto zinazoikabili tasnia na waandishi wa habari,” alisema.

Kwa upande mwingine, Meena alisema kumekuwapo ongezeko la washiriki wa maadhimisho hayo unaozijumuisha asasi za utetezi wa demokrasia na haki za binadamu.

Naye Patrick Kipangula, kutoka Maelezo alisema ipo haja kwa waandishi wa habari kujikita katika misingi ya sheria, kanuni na taratibu zinazoiongoza tasnia ya habari ili kuepuka matatizo yanayoweza kuzuilika.

Kipangula alisema maadhimisho ya mwaka huu yanafanyika kwa kaulimbiu inayoendana na wakati ambako taifa linatarajia kuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Nancy Kaizilege kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa (Unesco) alisema tasnia ya habari ina umuhimu wa pekee katika kuchagiza kasi ya maendeleo ikiwamo Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Naye Makamu wa Rais wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari (UTPC), Jane Mihanji, alisema licha ya waandishi wa habari kukabiliwa na changamoto zinazotokana na sheria zilizopo, umuhimu wa tasnia hiyo kwa umma hauepukiki.



Prof. Aldin Mutembei wa Taasisi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha kuhitimu kidato cha sita kwa Mwanafunzi David Keasi, wakati wa mahafali ya kidato cha sita ya Shule ya Sekondari ya Thomas More Machrina, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mwanzilishi wa shule hiyo, Prof. Justinian Galabawa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mambo 10 yaliyotikisa Bajeti

INATOKA UK. 4

serikali imeendelea kuwa inapunguza utegemezi.”

Akieleza zaidi namna washirika wa maendeleo walivyo bado na imani na serikali, Waziri Ndalichako alisema mpaka anahitimisha bajeti ya wizara hiyo, Serikali ya Uswis imetoa msaada wa jumla ya Sh. bilioni 14.9 kwa ajili ya kuendeleza ujuzi.

Alisema fedha hizo hazipo kwenye kitabu cha bajeti cha sasa na haziwezi kuonekana kwa sababu ni makubaliano ambayo wameingia hivi karibuni na Mei 31, watazindua rasmi mpango huo.

“Lakini nitoe taarifa zaidi kwamba kupitia Global Partinership in Education, mfuko huu umetoa Dola milioni 90 kwa Tanzania mwanzoni mwa mwezi wa Aprili ambayo ni sawa na Sh. bilioni 200 za Tanzania. Huo ni msaada kutokana na utawala bora nchini,” alisisitiza.

Aidha, waziri huyo amepangua hoja za wabunge wanaohoji kupungua kwa bajeti ya wizara hiyo akisema: “Kumekuwa pia na dhana kwamba bajeti ya wiazara imepungua mwaka uliopita ilikuwa trilioni 1.407 na mwaka huu ni trilioni 1.388, naomba niwahakikishie serikali hii ya awamu ya tano iko makini sana na bajeti ya Wizara ya Elimu ndio maana ina mambo mengi mazuri yamefanyika.

“Bajeti ya Wizara ya Elimu haijapungua, isipokuwa tumekuwa na mabadiliko kidogo katika Program yetu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R), kiasi cha Sh. bilioni 90, 883, 40 za lipa kulingana na matokeo tumezipeleka katika fungu namba 56 la Ofisi ya Rais (Tamisemi), kwa hiyo kama zingebaki katika fungu namba 46, bajeti yetu ingesomeka trilioni 1.478.”

Kuhusu ushauri uliotolewa na wabunge kwamba serikali iangalie uwezekano kuvipanga vyuo vikuu vya Tanzania katika madaraja kama ilivyo kwa Marekani na Ulaya, Waziri Ndalichako amesema serikali haiwezi kufanya hivyo.

“Sisi katika elimu ya juu, vyuo vyetu vingi bado ni vichanga na kwa maana hiyo serikali ina wajibu wa kuvilea na kuhakikisha kwamba vinakua. Leo hii tukianza kuweka madaraja ukasema Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) iwe daraja la kwanza, ukasema labda kwa mfano Chuo Kikuu cha Mzumbe kiwe daraja la tatu, tayari utakuwa unawapa Watanzania hapa kwamba hapa sio mahali pazuri pa kwenda,” alisema.

Kuhusu madai kwamba serikali inachelea kukipandisha hadhi zaidi, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Julius K. Nyerere, alisema ni bahati mbaya majengo ambayo yalitolewa kwa serikali yalitolewa kwa maneno na haijapata kama serikali hati.

Kuhusu suala la wanafunzi wenye mahitaji maalum, alisema serikali inalichukulia kwa uzito mkubwa na kwa kutambua matatizo makubwa yaliyopo katika shule hizo kwa kutenga Sh. bilioni 11.2 katika bajeti ya 2019/20 kwa ajili ya kununua vifaa visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Malalamiko kuhusu muda wa kumaliza elimu ya msingi, alisema muda wa elimu ya msingi ni miaka saba na wala haujabadilika.

Alisema kwa sasa serikali haina mpango wowote wa kubadilisha muda huo, kwa sababu serikali imejikita zaidi katika kutatua changamoto.

# Madaktari watakiwa kusomea usingizi

**Na Mary Geofrey**

RAIS wa Chama cha Wataalam wa kutoa dawa za usingizi na ganzi wakati wa upasuaji kwa wagonjwa mahututi (Sata), Dk. Mpoki Ulisubisya, amewataka madaktari wanaosoma ngazi ya uzamili kusoma fani ya usingizi na ganzi kwa sababu haina madaktari bingwa wa kutosha.

Dk. Ulisubisya aliyaeleza hayo jana katika mkutano wa sita wa Chama cha wana taaluma ya kutoa dawa za usingizi na ganzi kwa wagonjwa mahututi uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema nchini kuna madaktari wa usingizi na ganzi takribani 50 na wanaohitajika ni 200 kwa ajili ya hospitali ya rufaa na wilaya.

“Huduma ya usingizi na ganzi ni haki ya msingi ya mgonjwa yoyote anayetakata huduma hiyo, hivyo chama kinatoa ushauri kwa madaktari wanaosoma ngazi uzamili kuchukua fani ya usingizi kwa sababu kwa sasa wapo madaktari takribani 50 tu hivyo wanahitajika 200 kwa kuanzia na tunatakiwa kuwa na daktari mmoja angalau katika hospitali moja ya rufaa,” alisema.

Alisema kila kitengo cha huduma ya matibabu wanatakiwa kuwa na wataalam wa kutoa huduma za usingizi na ganzi ili kuokoa maisha ya wagonjwa.

Alisema mpaka sasa idadi kamili ya madaktari wa usingizi nchini ni 40 na kwamba wanatarajia kufikia 50 watakapohitimu wanaosoma sasa.

Alisema lengo la kuwa na wataalam hao ni kwa ajili ya kuokoa maisha ya wagonjwa mahututi ambao wanakuwa wameumia vibaya, wanatakiwa kupewa msaada wa haraka wa muhimu kama usingizi na ganzi kwa usalama wao.

“Wagonjwa wanaofikishwa Hospitali wakiwa mahututi, wanahitaji

## HABARI MICHE



### LIONEL MESSI

| | |
|---|---|
| **KUZALIWA:** | Juni 24, 1987 |
| **MAHALI:** | Rosario, Argentina |
| **KIMO:** | Mita 1.70 (5 ft 7) |
| **KLABU:** | Barcelona |
| **NAFASI:** | Mshambuliaji |
| **JEZI:** | Namba 10 |
| **LA LIGA 18-19:** | Mabao 34 |
| **UEFA 18-19** | Mabao 10 |



# GUARDIOLA, KLOPP VITANI TUZO YA KOCHA BORA

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England imetoa orodha ya makocha wanne wanaowania tuzo ya Kocha Bora wa Aprili, huku Jurgen Klopp wa Liverpool na Pep Guardiola wa Manchester City wote wakiwamo.

Timu hizo mbili zipo kwenye mbio moja ya ubingwa wa Ligi Kuu, huku kukiwa kumebakiwa na mechi mbili kwa kila timu kabla ya ligi hiyo kufikia tamati.

Orodha hiyo imetolewa katika tovuti ya Ligi Kuu na Klopp na Guardiola watachuana na Scott Parker wa Fulham na Nuno Espirito Santo wa Wolverhampton Wanderers.

City ya Guardiola ilipata ushindi mzuri hivi karibuni dhidi ya Manchester United na Tottenham Hotspur na kujiimarisha wao wenyewe kileleni mwa msimamo wa ligi, pia ikishinda dhidi ya Cardiff City, Crystal Palace na Burnley. Na Liverpool walipata ushindi dhidi ya Southampton, Chelsea, Cardiff na Huddersfield Town na kubakia nafasi ya pili kwenye msimamo huo.

Hata hivyo, Aprili ilianza vibaya kwa Scott Parker na Fulham, ambapo wameshuka daraja baada ya kipigo cha mabao 4-1 kutoka kwa Watford.

Tangu hapo imepata ushindi dhidi ya Everton, Bournemouth na Cardiff ikiwa inajaribu kumaliza msimu vizuri.

## Alves ampa darasa Neymar

**PARIS,** Ufaransa

DANI Alves amemshauri mchezaji mwenzake wa Paris Saint-Germain, Neymar ajaribu kujizuia na kuwa mtulivu baada ya kukwaruzana na shabiki baada ya kufungwa kwa penalti kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa, Coupe de France, dhidi ya Rennes.

Alves na Neymar wote walikuwapo kwenye mchezo huo na Alves amebainisha kwamba ameshindwa kumzuia Neymar kwa tabia yake ya hivi karibuni.

"Ulikuwa muda usiopendeza," alisema. "Tulipoteza na yeye alionekana kuwa mwenye hasira zaidi.

"Nafikiri haukuwa wakati muafaka kwa yeye kujaribu kuzozana na shabiki. Kuna wakati hutakiwi kujihusisha kwa namna yoyote ile, ni afadhali kukaa kimya tu na kujizuia.

"Naamini kwamba unaweza kufanya makosa na baadaye ukajizuia na kujiimarisha wewe mwenyewe.

"Hakukuwa na ulazima wa yeye kufanya vile kwa shabiki, alitakiwa kukaa kimya na kujiepusha naye. Neymar ni mtu wa aina yake, na kuna wakati anashinda kujizuia."





## Trippier: Tutabadili matokeo Uholanzi

**LONDON,** England

BEKI wa Tottenham, Kieran Trippier amesema kwamba kikosi chao kinaamini kwamba bado kina nafasi ya kufuzu kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya kufungwa kwenye mchezo wa kwanza na Ajax.

Spurs walifungwa bao 1-0 na kwenye mchezo wa kwanza kwa bao la Donny van de Beek na sasa watasafiri kwenda Uholanzi kwa ajili ya mchezo wa marudiano.

"Bado tuna nafasi, naamini tunaweza kufuzu kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nina matumaini mchezo wetu unaofuata unaweza kubadili matokeo na kwa uhakika kabisa tunaweza kubadilisha kitu fulani.

"Kwa kuwa tulifungwa 1-0, hivyo tuna nafasi ya kubadilisha matokeo kwenye mchezo unaofuata wiki ijayo.

"Sonny [Heung-Min Son] atakuwa amerudi kweye mchezo ujao na naamini kila kitu kitakuwa sawa na kikosi kitakuwa kipo kamili.

"Jumatano ijayo mambo yanaweza kubadilika, kama tulivyofanya dhidi ya Man City na mambo yalibadilika kabisa."

Spurs itacheza mchezo wa marudiano na Ajax Jumatano ijayo na mshindi atafuzu fainali ya michuano hiyo.

## HABARI MICHEZO



# MADRID KUPUNGUZA MSHAHARA WA POGBA

**MADRID,** Hispania

PAUL Pogba atalazimika kupunguza mshahara wake kama ataondoka Manchester United kwenda Real Madrid kipindi hiki cha majira ya joto, kwa mujibu wa ESPN FC.

Taarifa kutoka nchini Hispania zinasema kwamba, miamba hao wa dimba la Santiago Bernabeu wamejiandaa kumlipa mshahara wa pauni 290,000 kwa wiki kama atakubali kujiunga nao kutoka pale Old Trafford.

Habari zaidi kutoka Manchester zinasema kwamba Pogba mwenye umri wa miaka 26 hatauzwa, kwani bado wana mipango naye ya muda mrefu kuendelea kukipiga hapo kwa 'Mashetani Wekundu'.

Wote Pogba na kocha wa Madrid, Zinedine Zidane wamekuwa wakizungumza mara kwa mara kuhusu uwezekano wa Mfaransa huyo kutua kwenye jiji la Madrid.

Lakini kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer amesema mara kadhaa kwamba, kiungo huyo aliyesajiliwa kwa dau la pauni milioni 89 kutoka Juventus atakuwa sehemu ya kikosi chake msimu ujao.

Hata hiyo, chanzo kimoja kimeuambia mtandao wa ESPN FC kwamba baadhi ya wachezaji wenzake na Pogba atalazimisha uhamisho kama klabu hiyo itashindwa kufuzu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sare ya bao 1-1 na Chelsea Jumapili iliyopita imeiacha United kuwa kwenye wakati mgumu wa kumaliza ligi katika nne-bora.

# Pochettino akiri makosa Spurs ikichapwa na Ajax

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amebainisha kwamba hakutumia mbinu nzuri wakati Tottenham ikifungwa 1-0 na Ajax kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ajax walipata bao kupitia kwa mchezaji wake, Donny van de Beek na hivyo kujiweka kwenye nafasi nzuri kuelekea mchezo wa pili wa nusu fainali hiyo.

"Niliangalia vizuri na nakubali kwamba nilifanya makosa," alisema Pochettino akiiambia BT Sport.

"Lakini kulikuwa na njia nyingi. Sina furaha kwa matokeo haya kwani kilichotokea ni tofauti kabisa na matarajio yangu.

"Ila kikubwa ni kwamba, mbinu nilizotumia kwenye mchezo huu hazikuwa sawa, nilifanya makosa.

"Haikuwa mbinu ambazo nilitakiwa kuzitumia, maana nilifanya makosa na kuwaruhusu Ajax kucheza mpira wanavyotaka na tulipopata nafasi, lakini kiukweli tulishindwa kabisa kuzitumia.

"Mimi ni kocha na napenda kukubali makosa, lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha najisahihisha kuelekea mchezo unaofuata."





# *Mama Rabiot alia na Rais wa PSG*

**PARIS,** Ufaransa

MAMA na wakala wa kiungo wa Paris Saint-Germain, Adrien Rabiot, amemshutumu mwenyekiti na Afisa Mtendaji, Nasser Al-Khelaifi kwa 'kuipa sumu' timu kutokana na jinsi anavyomfanyia mwanawe.

Licha ya matarajio makubwa, PSG imekuwa na msimu mbaya zaidi tangu msimu wa 2011-12 ikiwa chini ya zama za Kampuni ya Qatari Sports Investment baada ya kupoteza kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa.

Pia ilitolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora na Manchester United licha ya mchezo wa kwanza kuongoza kwa 2-0 na Veronique Rabiot amemtupia lawama Al-Khelaifi.

"Rais Al-Khelaifi hafanyi maamuzi ya haki na kila mmoja analijua hilo," alisema akiliambia Shirika la Habari la Agence France Presse.

"Kwa kufanya hivyo ni kama ametia sumu kwa timu kitu ambacho kitakuja kuigharimu muda si mrefu na nina uhakika kabisa hili litakuja kuleta shida hapo baadaye.

"Wakati unapofanya maamuzi kwenye maisha, matokeo yake hayawezi kuwa madogo au ya kati.

"Kushindwa kuelewa kuwa wewe ni rais wa timu na unatakiwa kuwatendea haki wachezaji wote, hilo ni tatizo kubwa. Na sijui hata anaiendeshaje timu kubwa kama hii."

# DO SOKA
# MAG ULAYA




# LUIZ ATIA NENO MBINU ZA SARRI

## ●●● Wengi walisema Chelsea haitawali mchezo, inacheza tu mashambulizi ya kushtukiza na...

**LONDON,** England

DAVID Luiz amekuwa kisiki imara katika mbinu za Maurizio Sarri, na beki huyo wa Chelsea anasema yuko katika "upendo" na falsafa ya soka la Italia.

**Kocha huyo wa zamani wa Napoli, Sarri, amekuwa akihaha kushinda vita dhidi ya mashabiki hapo Stamford Bridge katika msimu wake wa kwanza na mashabiki wamekuwa wakionyesha hasira kuhusu mbinu zake.**

Wakiimba 'f*** Sarriball' walisikika wakati wa mechi ya Kombe la FA wakipokea kipigo dhidi ya Manchester United na walipotokea nyuma na kushinda dhidi ya Cardiff City, huku Sarri akizidi kusisitiza kumchezesha Jorginho kama kiungo mkabaji badala ya N'Golo Kante pia wamekuwa wakihoji.

Na bado David Luiz, ambaye amekuwa akipewa nafasi ya kuanza mara kwa mara chini ya Sarri msimu huu, anapendelea mbinu za sasa za kocha huyo wa Chelsea kuliko za mtangulizi wake.

"Namna anavyocheza soka ni namna ninavyopenda soka," beki huyo wa kimataifa wa Brazil aliiambia Sky Sports News. "Ni namna ninavyofurahia soka, na si tu kucheza bali hata kutazama. Ninapenda falsafa zake.

"Watu wengi walisema Chelsea haitawali mchezo - ama Chelsea inacheza tu mashambulizi ya kushtukiza na kupaki basi.

"Sasa tunatawala mechi zote na wanatukosoa kwa sababu hawadhani tunashinda mechi kwa kumiliki.

"Falsafa zake ni za kushangaza. Anajaribu kucheza soka; hii inachukua muda. Tunajaribu kujizatiti haraka iwezekanavyo."

Ingawa mbinu zake zimekuwa zikizua maswali, Sarri bado ameiongoza Chelsea kufika fainali ya Kombe la Ligi [EFL Cup] ambapo ilichapwa na Manchester City kwa mikwaju ya penalti wakati huu pia ikiwa nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, EPL lakini pia ikitinga nusu fainali ya Europa League.

Na ikimaliza nafasi nne za juu na kutwaa ubingwa wa Europa utakuwa ni msimu wa kuvutia, kwa mujibu wa David Luiz.

"Nadhani ni namna nzuri ya kumaliza msimu," aliongeza.

"Lakini msimu mzuri kwa Chelsea mara zote ni kupigania kila kombe.

"Kama utatwaa ubingwa wa Europa League na kumaliza nafasi nne za juu itakuwa ni vizuri. Bali klabu kubwa mara zote inafikiri na lengo. Tunataka kutwaa kombe."

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMTEGA POGBA

REAL Madrid haiko tayari kumlipa Paul Pogba mshahara wa pauni 290,000 kwa wiki, na hiyo inamaanisha kiungo huyo wa Manchester United atalazimika kukubali mshahara wake upungue kama atataka kujiunga na klabu hiyo ya Hispania. ***(ESPN)***

### LIGT, RAIOLA WATOFAUTIANA

BEKI wa Ajax, Matthijs de Ligt (19), anataka kuona anajiunga na mchezaji mwenzake, Frenkie de Jong katika kikosi cha Barcelona msimu ujao, lakini wakala wake, Mino Raiola angependa nyota huyo ahamie Manchester United, Juventus au Bayern Munich. ***(Mundo Deportivo)***

### SILVA: SIONDOKI CITY

KIUNGO wa Manchester City, Bernardo Silva (24), amesema hafikirii kuondoka katika klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England, licha ya kuwapo na tetesi za kutakiwa na mabingwa wa Hispania, Barcelona. ***(Manchester Evening News)***

### NKUNKU ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imeelezwa kuwa inatakiwa kulipa ada ya pauni milioni 17.2 kwa ajili ya kumnasa mshambuliaji, Christopher Nkunku kutoka Paris St-Germain, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Evening Standard)***

### EMERY ATAJA VIFAA

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, amewataja mabeki wa kati anaowahitaji kuwa ni pamoja na nyota wa Leicester, Harry Maguire, Toby Alderweireld (Spurs), Dejene Dakonam wa Getafe na Kurt Zouma kutoka Chelsea ambaye yuko kwa mkopo katika klabu ya Everton. ***(Sun)***

### CITY YAACHANA NA CHILWELL

MANCHESTER City imesitisha uamuzi wa kumsajili beki wa kushoto wa Leicester City na England, Ben Chilwell (22), kwa sababu imeridhika na kiwango cha nyota wake, Benjamin Mendy na Oleksandr Zinchenko. ***(Manchester Evening News)***

### BARCA YAMTEGA MATA

KIUNGO mchezeshaji wa Manchester United, Juan Mata (31), atalazimika kupunguza kiasi cha mshahara anaopata kila wiki kama anataka kutimiza ndoto zake za kuichezea Barcelona. ***(Sun)***

### SESSEGNON ANUKIA SPURS

TOTTENHAM inaongoza vita ya kuwania saini ya nyota wa Fulham, Ryan Sessegnon, ambaye pia anawindwa na Paris St-Germain, Juventus na Borussia Dortmund baada ya klabu yake maarufu kama Cottagers kushuka daraja. ***(Evening Standard)***

### FERNANDES KUTUA CITY

MANCHESTER City imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes na tayari imeshaanza mazungumzo na klabu yake ili kumnasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(A Bola)***

### DARMIAN KURUDI ITALIA

INTER Milan inajiandaa kumrejesha beki wa Manchester United, Matteo Darmian (29), nchini Italia, na tayari klabu hiyo ya England iko tayari kumwachia nyota huyo kwa dau la chini ya pauni milioni tisa. ***(Gazzetta dello Sport, via the Sun)***

HABARI MICHEZO

# Dilunga afunguka kuamua mechi JKT

**Na Somoe Ng'itu**

MFUNGAJI wa bao pekee katika mechi dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, kiungo wa Simba, Hassan Dilunga, amesema timu yake inafahamu inachohikitaji katika Ligi Kuu Bara ambayo inaelekea ukingoni.

Dilunga aliliambia gazeti hili kuwa Simba imekuwa ikicheza kwa kupambana katika muda wote wa dakika 90 kwa sababu inahitaji kushinda ili itengeneze mazingira mazuri ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo ambao wanaushikilia.

Kiungo huyo alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu kwa pande zote mbili kwa sababu JKT Tanzania ni moja ya timu nzuri kwenye ligi hiyo na ina uzoefu.

"Mchezo sijauamua mimi, mchezo tumeuamua timu nzima, ni juhudi za pamoja za timu nzima tuliyoionyesha nini tunatafuta,...tunafanya juhudi katika kila mechi, ingawa mechi zetu ziko karibu karibu, tunajua nini tunachokitaka, tulikutana timu nzuri kwa nzuri," alisema Dilunga.

Kiungo huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar alisema kuwa licha ya kuwa na ratiba ngumu, lakini bado wanajipanga kupambana ili kuendelea kuwafurahisha mashabiki wao.

"Kikubwa tunawaambia mashabiki wasiwe na haraka, wasiwe watu wa kukata tamaa, tunajua tunachokihitaji, tunataka ubingwa," Dilunga aliongeza.

Naye Kelvin Nashon wa JKT Tanzania, alilalamika kuwa mwamuzi wa mchezo huo hakuchezesha kwa haki na hiyo ilitokana na kuchukua haraka pale Simba inapochezewa faulo tofauti na inavyotokea kwa upande wao.

"Mipango yetu tuliyoingia nayo ilifanikiwa, mapungufu yalikuwa ni madogo madogo, kwa ujumla tumecheza vizuri, Simba ni timu kubwa, komavu, ilitulia na kupambana, na hatimaye ilifanikiwa kupata ushindi, bado ushindani ni mkubwa katika ligi, tumeachana pointi chache," alisema nyota huyo.

# REFA MSTAAFU FIFA AGUSWA MAREFA KUVURUNDA LIGI KUU

**Na Somoe Ng'itu,** Aliyekuwa MUSOMA

WAKATI kumekuwa na sintofahamu kuhusu ubora wa waamuzi wanaochezesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Ligi Daraja la Kwanza, mwamuzi mstaafu wa Fifa, Paschal Chiganga, amesema enzi zake hakuwahi kuyumba wala kutetereka katika mchezo wowote aliopewa kuchezesha.

Chiganga kutoka Musoma, Mara ambaye ndiye alichezesha mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, aliliambia Nipashe katika mahojiano maalumu mapema wiki hii kuwa anasikitika kuona waamuzi wa sasa wanashindwa kufanya vema kazi yao.

Mwamuzi huyo mstaafu alisema enzi zao waamuzi walifanya kazi kwa uadilifu mkubwa kwa sababu walikuwa wanahitaji kutangaza vema majina ya mikoa wanayotoka.

**"Tulichezesha kwa uadilifu mkubwa sana, kwa mfano mimi, kama nachezesha mechi za hapa nchini niliwaza kufanya vizuri ili kuutangaza vema mkoa wangu wa Mara au kama naenda kucheza michezo ya kimataifa, nilikuwa nafikiria kulitangaza vizuri jina la Tanzania," alisema Chiganga ambaye kwa sasa ni mkufunzi wa waamuzi na msimamizi wa waamuzi.**

Alisema licha ya changamoto za usafiri zilizokuwa zinawakabili wakati huo, hakuwahi kupanda ndege akiwa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara au Ligi Daraja la Kwanza kwa sababu ya kiasi kidogo cha posho walichokuwa wanalipwa.

Aliongeza kuwa kazi ya uamuzi inatakiwa kufanywa kwa uadilifu mkubwa na hilo wamekuwa wakilisisitiza katika madarasa yote wanayoyafanya hapa nchini kwa lengo la kuwaendeleza waamuzi wapya.

Hata hivyo, Chiganga alisema anafurahi kuona waamuzi wa Tanzania sasa wanapata mechi nyingi za kimataifa na anapokutana nao anawakumbusha vitu muhimu na vya msingi katika kazi yao.

Chiganga ambaye alikuwa msimamizi wa waamuzi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya wenyeji Biashara United dhidi ya Simba, alianza kuchezesha soka tangu mwaka 1993, alistaafu kazi hiyo mwaka 2009.



Mwamuzi mstaafu wa Fifa, Paschal Chiganga, akifuatilia kwa makini mechi dhidi ya Biashara United na Simba iliyopigwa katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume wiki hii, akiwa sambamba na Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Somoe Ng'itu. **NA MPIGAPICHA WETU**

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 33 | 24 | 5 | 4 | 52 | 23 | 77 |
| 2. Simba | 28 | 23 | 3 | 2 | 58 | 11 | 72 |
| 3. Azam | 33 | 19 | 9 | 5 | 49 | 20 | 66 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 34 | 12 | 12 | 10 | 30 | 31 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. KMC | 33 | 9 | 15 | 9 | 33 | 25 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 11. Singida Utd | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 33 | 9 | 12 | 12 | 28 | 35 | 39 |
| 13. JKT Tanzania | 33 | 9 | 12 | 12 | 20 | 28 | 39 |
| 14. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Biashara United | 33 | 9 | 10 | 14 | 25 | 31 | 37 |
| 17. Alliance | 33 | 9 | 10 | 14 | 24 | 36 | 37 |
| 18. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 19. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 20. 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# Mgombea Yanga aahidi neema

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA wa nafasi ya Uenyekiti katika Uchaguzi Mkuu wa Yanga, Mbaraka Igangula, amesema endapo atachaguliwa atahakikisha mchakato wa klabu yao kujiendesha kwa mfumo wa kampuni unakamilika kwa sababu anaamini utaharakisha maendeleo.

Uchaguzi Mkuu wa Yanga unatarajiwa kufanyika Jumapili kwenye Ukumbi wa Bwalo la Polisi Oysterbay, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Igangula alisema atausimamia mchakato huo mara tu atakapoingia madarakani huku pia akipanga kuajiri wataalamu wenye ujuzi wa masuala ya kampuni na si kuendesha klabu kwa "mazoea".

Igangula alisema amejitosa kuwania nafasi hiyo kwa lengo la kuifanyia "mambo makubwa" klabu hiyo na kamwe hataweka mbele maslahi binafsi na badala yake ataiendeleza timu hiyo kongwe hapa nchini na Afrika Mashariki.

Alisema akiwa kama kiongozi mzoefu aliyeiongoza Yanga kwa mafanikio kuanzia mapema mwaka 2000, atasimamia amani na kurejesha umoja ambao ndio msingi wa mafanikio ya klabu hiyo.

"Umoja ambao ndio utamaduni wa Wanayanga, haupo tena kutokana na klabu kukosa viongozi waadilifu, hivyo kunahitajika mabadiliko chanya ili wanachama warejeshe imani kwa uongozi na klabu kwa ujumla," alisema Igangula.

Alisema endapo wanachama watampa ridhaa ya kuwaongoza, atahakikisha anaukarabati Uwanja wa Kaunda ndani ya muda mfupi ili uweze kutumika kwa ajili ya mazoezi ya timu yao na kuokoa fedha wanazotumia kulipia viwanja mbalimbali vya kukodi.

"Tutakuwa na mpango wa muda mfupi ambao tutaukarabati uwanja wetu pale klabuni, huku tukiwa na mpango wa muda mrefu wa kujenga uwanja nje ya mji, hata ikiwezekana Kibaha, Pwani ambao utakuwa na hosteli, maduka na ofisi mbalimbali," alisema.

Aliongeza pia ataanzisha bima ya afya itakayowalenga wanachama, saccos, vicoba na mfuko wa kufa na kuzikana, kama sehemu ya kuimarisha umoja, upendo na mshikamano baina ya wanachama na viongozi wa klabu hiyo.

Aliahidi kulipa wachezaji na benchi la ufundi kwa wakati, kudhibiti mikataba mbalimbali, mapato na kuzuia ufisadi ili kila mmoja ndani ya Yanga aweze kufurahia kuwa sehemu ya wanafamilia wa klabu hiyo huku akiwataka wezi wa mali za klabu hiyo kukaa chonjo.

# Michezo

Alhamisi Mei 2, 2019

Nipashe




## Luiz atia neno mbinu za Sarri

HABARI UK.30



WANGU...

Kipa wa Ajax, Andre Onana (kulia), akiruka kuudaka mpira na kuvaana na mabeki wa Tottenham, Jan Vertonghen (nyuma) na Toby Alderweireld (kushoto), kwenye mechi ya nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa juzi usiku. Ajax ilishinda 1-0. **HABARI UK. 29**

# Stars ya Afcon hii

## ●●● Amunike awaita Ajibu, Kapombe, Kelvin John kulingurumisha...

**Na Somoe Ng'itu**

NAHODHA na mshambuliaji wa Yanga, Ibrahim Ajibu, beki wa Simba, Shomary Kapombe na straika chipukizi wa Serengeti Boys, Kelvin John 'Mbappe' wameitwa katika kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kitakachoingia kambini kujiandaa na Fainali za Afrika (AFCON 2019) ambazo zitafanyika kuanzia Juni 21 hadi Julai 13, mwaka huu nchini Misri.

**Kapombe alikuwa majeruhi tangu Novemba mwaka jana alipoumia akiwa katika kikosi hicho cha Stars huku Gadiel Michael wa Yanga ambaye mapema wiki hii aliumia wakati timu yake ikicheza mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC naye akiitwa katika kikosi hicho.**

Mbali na wachezaji hao, pia Kocha Mkuu wa Taifa Stars Mnigeria Emmanuel Amunike, amemrejesha beki wa zamani wa Simba, Abdi Banda kutoka Baroka FC ya Afrika Kusini pamoja na nyota, Adi Yusuph anayeichezea Solihull Moors ya England.

Amunike alisema pia kikosi hicho kitapeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya Kombe la Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Kikosi kamili cha Stars: Makipa ni Aishi Manula (Simba), Metacha Mnacha (Mbao FC), Suleiman Salula (Malindi), Aron Kalambo (Prisons), Claryo Boniface (U-20) wakati mabeki ni Hassan Kessy (Nkana FC), Vicent Philipo (Mbao FC), Kapombe, Gadiel, Banda (Baroka), Ally Mtoni (Lipuli), Mohammed Hussein (Simba), Aggrey Moris (Azam), Kelvin Yondani (Yanga), Erasto Nyoni (Simba), David Mwantika (Azam), Ally Ally (KMC) na Kennedy Wilson wa Singida United.

Viungo ni Feisal Salum (Yanga), Mudathir Yahya (Azam), Yahya Zaydi (Ismailly), Jonas Mkude (Simba), Ajib, Fred Tangalu (Lipuli), Shabani Chilunda (Tenerife), Frank Domayo (Azam), Shiza Kichuya (Enppi), Simon Msuva (Difaa El- Jadid), Rashid Mandawa (BDF), Mbwana Samatta (Genk), Thomas Ulimwengu (JS Saoura), John Bocco (Simba), Farid Mussa (Tenerife), Ayoub Lyanga (Coastal Union), Kassim Khamis (Kagera Sugar), Miraji Athumani (Lipuli), Kelvin John (U-17) na Yussuf.

Katika Fainali za Afrika, Stars ambayo haijashiriki mashindano hayo kwa miaka 39 iliyopita, imepangwa Kundi C, pamoja na timu za Algeria, Senegal na majirani zao, Harambee Stars ya Kenya.

Hata hivyo, Stars ambayo ilikuwa chini ya Mbrazil Marcio Maximo ilishiriki fainali za kwanza za CHAN zilizofanyika mwaka 2008 nchini Ivory Coast.

Ili kujiwinda na michuanio hiyo, Stars inatarajia kwenda kuweka kambi Ulaya na tayari imefahamika itacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Misri, itakayochezwa Juni 13 jijini Cairo.

# Simba waipigia hesabu Sevilla

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuichagua Simba kuivaa Sevilla, uongozi wa Wekundu wa Msimbazi hao umesema utatumia fursa waliyoipata kucheza na timu hiyo maarufu ya Ligi Kuu ya Hispania (La Liga), Sevilla kuwapa uzoefu wa kimataifa wachezaji wake.

Simba itacheza na Sevilla Mei 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam huku timu hiyo ya Hispania ikitarajiwa kutua nchini Mei 21 chini ya udhamini wa Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya SportPesa Tanzania.

Afisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, akizungumza na mwandishi wetu jana kufuatia Simba kupata nafasi hiyo kwa kutumia kigezo cha kufanya vizuri kwenye mashindano ya SportPesa Cup, alisema mbali ya kutotwaa ubingwa wa SportPesa, lakini wameweza kufanya vizuri zaidi kulinganisha na timu zote na uteuzi wao utaongeza ushindani katika mashindano hayo yajayo.

Alisema TFF imetumia kigezo sahihi na wamepokea nafasi hiyo kwa furaha na wataitumia vizuri, pia kupata ushindi dhidi Sevilla.

"Simba kwa sasa ipo katika kiwango cha juu na kucheza na Sevilla kutasaidia kujua viwango vya wachezaji wetu katika mechi za kimataifa," alisema Manara na kuongeza:

"Mechi hii inaiweka Tanzania katika historia kubwa sana katika soka. Historia zinaonyesha kuwa miaka ya nyuma, timu mbalimbali kutoka nje ya mipaka ya Afrika zilikuja hapa Tanzania na kucheza na Yanga na Simba, miaka ya hivi karibuni hakukuwa na ujio huo zaidi ya mwaka 2017 ambapo SportPesa iliileta timu ya Everton na kucheza timu ya Gor Mahia ya Kenya."

# Yanga dimbani leo bila Kindoki

**Na Somoe Ng'itu**

MBIO za kuwania ufalme wa soka Tanzania zinatarajia kuendelea kwa Yanga kuwakaribisha "Maafande" wa Prisons kutoka Mbeya katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Yanga ambayo imewazidi watani zao Simba pointi tano, leo itashuka dimbani bila ya kipa wake chaguo la kwanza kwa sasa, Klaus Kindoki ambaye ana kadi tatu za njano pamoja na beki wao wa kati, Kelvin Yondani ambaye amefungiwa mechi tatu na majeruhi, Gadiel Michael.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema kuwa maandalizi ya mchezo huo yanakwenda vizuri kwa sababu wanaamini nafasi ya kutimiza malengo yao kwa msimu huu bado wanayo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >